

**Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA TISA**

**Kikao cha Tano - Tarehe 19 Aprili, 2005**

*(Mkutano Ulianaza Saa Satu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua*

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 60

**Fedha Zinazotengwa kwa Ajili ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI**

**MHE. LUCAS L. SELELII (K.n.y. MHE. AZIZA SLEYUM ALI)** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali hutenga fedha kwa ajili ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI:-

(a) Je, Fedha hizo zinawafikia waathirika kwa utaratibu gani na ni waathirika wangapi waliosaidiwa na mfuko huo na wapo katika Mikoa gani na ni nani anayewafikishia fedha hizo?

(b) Je, hadi sasa ni kiasi gani cha fedha kimeshatumika kuwasaidia walioathirika?

(c) Je, ni kiasi gani cha fedha kwa ujumla kimetumika tangu Tume hiyo ilipoanzishwa hadi sasa?

(d)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swal la Mheshimiwa Aziza Sleyum Ali, Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali hutoa fedha kwa ajili ya kudhibiti UKIMWI nchini. Fedha hizo hupitia kwenye Wizara mbalimbali na katika Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (*TACAIDS*). Fedha hizo ni kwa ajili ya kuwasaidia wananchi wote,

wasio na virusi vya UKIMWI wasiambukizwe virusi na wenyе virusi, wagonjwa wa UKIMWI na walioathiriwa vinginevyo na UKIMWI waweze kusaidiwa.

Kwa hiyo, walengwa wa fedha hizi ni Watanzania wote kwa nia ya kudhibiti UKIMWI na fedha huwafikia kwa hali na mali. Matangazo, maelezo na habari juu ya UKIMWI zinapotolewa na zinapowafikia walengwa basi fedha hizo zilizotolewa na Serikali zinakuwa zimefanya kazi iliyokusudiwa. Wagonjwa wa UKIMWI wanapotibowi na mayatima na waathirika wengine wanaposaidiwa, fedha inakuwa imetekeleza lengo lililokusudia.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua nafasi hii kulikumbusha Bunge lako Tukufu, kwamba maendeleo ya wananchi wote, pamoja na waathirika na UKIMWI yapo mikononi mwa Halmashauri za Mamlaka za Serikali zao za Mitaa, ni kwa sababu hiyo Serikali, kwa ridhaa ya uongozi wa Mamlaka hizo, imeamua kuweka jukumu la kudhibiti UKIMWI mikononi mwao.

Fedha hazitolewi bila kuwa na mpango maalum, zinatolewa kwa lengo lilioombewa katika mpango uliotayarishwa. Kwa hiyo, fedha inapotolewa inajulikana inakwenda kwa nani, kwa makusudi gani na mpokeaji ni nani. Kwa kawaida Halmashauri za Mamlaka za Serikali za Mitaa, asasi za kiraia ikiwa ni pamoja na asasi zisizo za Kiserikali, asasi za wenyе virusi vya UKIMWI Mashirika ya kidini na kadhalika hutayarisha maombi na kuyatuma *TACAIDS*. Ingawa si kila anayeomba hupewa, Mikoa yote imefikiwa na fedha hizo na uamuvi wa nani apewe au asaidiwe ni wa asasi iliyooomba kadri ilivyoomba na kukubaliwa. Halmashauri zote zimeagizwa na zimepewa mafunzo maalum ya jinsi ya kuwashirikisha wadau wake wote, pamoja na wenyе virusi kuchanganua hali ya UKIMWI katika eneo lao ili kutayarisha mipango bora inayowanufaisha walengwa wote pamoja na waathirika. Sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Aziza Sleyum Ali, Mbunge, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

- (a) Fedha hupelekwa kwa mwombaji moja kwa moja au kupitia kwa Halmashauri yake. Kwa kuwa fedha zinaelekezwa zaidi kwenye asasi au kwenye makundi badala ya mtu mmoja mmoja na kwa kuwa mara nyingi walengwa hawapewi fedha taslim mikononi, si rahisi kujua idadi kamili ya waliofaidika. Ikumbukwe kwamba wengi wamepata huduma za jumla katika Mikoa yote.
- (b) Fedha ya kudhibiti UKIMWI ikiingia katika taasisi yoyote ile inawafaidia wote waathirika na wasiowaathirika. Hadi sasa fedha iliyopelekwa Mikoani tangu mwaka 2001 ni sh. 4,412,362,416/. Fedha hii inajumuisha matumizi yaliyoambatana na udhibiti wa UKIMWI kwa jumla na huduma kwa waathirika mbalimbali wakiwemo watoto.
- (c) Tangu kuanzishwa kwa Tume hiyo, *TACAIDS* hadi Desemba 2004 jumla ya sh. 20,126,207,154 zimetumika nchini kwa shughuli zinazohusiana na udhibiti wa UKIMWI.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Spika, nakubaliana kabisa na majibu ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu.

(a) Ukiangalia tatizo la Ukimwi liko zaidi katika Vijiji na kwa sasa vipimo vinavyojulisha ugonjwa wa UKIMWI, vinapatikana katika Hospitali za Wilaya. Je, Waziri haoni kwamba fedha hizo ziwe zinapelekwa kwenye zahanati na vituo vya afya ili vipimo hivyo viweze kupatikana ngazi za vijiji au katika vituo vya afya ili kupunguza adha ya kwenda katika Hospitali za Wilaya kupata vipimo kwa wananchi wa kawaida?

(b) Katika sehemu (a) ya muuliza swali ameulizia juu ya fedha ambazo zinakwenda moja kwa moja kwa waathirika, wajane na watu jinsi ambavyo wameathirika na UKIMWI. Je, Waziri haoni ni wakati mzuri kuwapatia fedha waathirika wa UKIMWI ambaao hawana uwezo kwa sababu tiba siyo dawa tu, ni pamoja na vyakula ambavyo atavitumia. Haoni busara kuwapa fedha ili waweze kujikimu kupata chakula kwa ajili ya kupambana na ugonjwa huo? (*Makofî*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Lucas Selelii, Mbunge wa Nzega, kama ifuatavyo:-

Ni kweli baadhi ya vipimo muhimu vya UKIMWI viko katika maeneo ya miji, lakini sehemu kubwa Serikali imejitahidi kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali zisizo za Kiserikali kupeleka vipimo vya awali vya kugundua virusi vya UKIMWI katika maeneo mengi sana hata katika maeneo ya vijiji kwa sehemu kubwa. Wote tunashuhudia baadhi ya taasisi nyingi sana ambazo zimejitolea zinapima UKIMWI katika maeneo mengi ya Vijiji na sehemu nyingine wanafanya bila malipo yoyote.

Lakini viro vifaa vingine vikubwa zaidi ambavyo vinahitaji umeme na utaal amkubwa ambavyo kwa kweli mpaka sasa viko katika maeneo ya miji. Lakini bado kwa kushirikiana na viongozi wote wa Halmashauri za Wilaya, tunawahamasisha wananchi wajitokeze kwa hiari yao wenyewe kwenda kupima katika maeneo mbalimbali, angalau nasema vipimo vingi vya kuthibitisha kama mtu ana virusi au hana virusi vya Ukimwi sasa hivi viko katika maeneo mengi hata katika maeneo ya vijiji. Lakini ni kweli kama alivyosema katika swali la pili Mheshimiwa Lucas Selelii wako wajane na waathirika wengi wa UKIMWI. Lakini ni ukweli kama nilivyoyibju swali langu la msingi ni kwamba fedha tunazipeleka na zinawahudumia hawa walengwa ambaao ni wajane, waathirika wa Ukimwi na yatima. Lakini hatupeleki fedha hizi kwa mtu mmoja mmoja.

Hawa waathirika wana vyama vyao, kwa hiyo, *TACAIDS* inakutana nao na imeshawaelekeza namna ya kuomba hizi fedha na aina ya miradi ambayo wanaweza wakaombea fedha ili waweze kupata na wahudumie watu wao kwa kuwanunua madawa na huduma nyinginezo. Tunajua kabisa kwamba dawa siyo tiba pekee kwa waathirika wa UKIMWI, hata lishe ni tiba. Kwa hiyo, Serikali inatoa fedha kwa waathirika hawa wa UKIMWI kwa huduma mbalimbali kama zinavyoombwa na taasisi zao kupitia kwenye taasisi hizo.

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kuniruhusu kuuliza swali moja kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa Halmashauri ya Mji ni mojawapo ambao wamewasilisha mipango mbalimbali kwenye Tume ya Kudhibiti Ukimwi kwa ajili ya kupata mgao wa fedha mbalimbali ambazo zinasaidia katika kukabili janga hili la Ukimwi. Kwa kuwa hadi hivi sasa mipango mingi ya Halmashauri haijapewa fedha hizi japo karibu mwaka wa Bajeti unaisha na kama tulivyoshuhudia mwaka jana *TACAIDS* walirejesha hela nyingi sana kwenye Bajeti ambazo hazikutumika. Sasa Waziri, atawaeleza nini wananchi wa Bukoba na hususan Halmashauri ya Mji wa Bukoba, ni lini itapata fedha hizi za mpango ambayo imetayarishwa na tayari iko *TACAIDS* na *TACAIDS* haijatueleza tatizo lolote kuhusu mipango hiyo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, Mbunge wa Bukoba Mjini, kama ifuatavyo:-

Ni kweli *TACAIDS* imeshatoa fedha kwa Halmashauri kadhaa, lakini zipo baadhi ya Halmashauri nyingine ambazo hazijapewa kwa sababu mbalimbali. Sababu ni kwamba baadhi ya maandishi/michanganuo iliyopelekwa kwenye *TACAIDS* haikuridhisha Tume kuweza kutoa fedha. Hivi sasa Tume inawasaliana na Halmashauri hizo, ikiwemo Bukoba, najua kesi ya Bukoba, ili waweze kukaa pamoja na kuandika maandishi ambayo yataiwezesha Halmashauri ya Mji wa Bukoba kupata hizo fedha. Naamini kama wakielewana na naamini watalewana, fedha hizi zitatolewa.

**SPIKA:** Maswali kwa Ofisi ya Rais, Tawala na Mikoa na Serikali za Mitaa.

**WABUNGE FULANI:** Umemruka Mheshimiwa Monica Mbega.

**SPIKA:** Nimemruka Mheshimiwa Monica Mbega sikumwona Bungeni kwa hiyo, nikafikiri amegairi lakini kuna mtu wa kumwulizia swali lake. Mheshimiwa Estherina Kilasi.

Na. 61

#### **Kampeni Dhidi ya Ukimwi**

**MHE. ESTHERINA KILASI (K.n.y. MHE. MONICA N. MBEGA)** aliuliza:-

Kwa kuwa, ugonjwa wa UKIMWI unazidi kuongezeka siku hadi siku na mamia ya Watanzania wanaendelea kupoteza maisha yao kila siku kutokana na ugonjwa huo. Je, kampeni mbalimbali za mapambano dhidi ya UKIMWI zimesaidia kwa kiasi gani kupunguza maambukizi tangu zilipoanza?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI) alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Monica N. Mbega, Mbunge wa Iringa Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, jitihada kubwa zimefanywa na zinaendelea kutekelezwa katika mapambano dhidi ya UKIMWI tangu ulipogundulika hapa nchini mwaka 1986. Tulianza na mpango wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI (*NACP*) na kuimarisha kampeni hizo kwa kuanzisha Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (*TACAIDS*) mwaka 2000. Masuala ya Ukimwi sasa yanazungumzwa na kujadiliwa nchi nzima, ikiwa ni pamoja na kuonyesha athari zake.

Mheshimiwa Spika, kampeni za kupambana na kuongezeka kwa ugonjwa wa UKIMWI zimesaidia sana.

1. Wananchi wanajua habari muhimu kuhusu ugonjwa huu na jinsi virusi vinavyoambukizwa.
2. Viongozi katika asasi zote wanajadili masuala ya UKIMWI kadiri ya fursa zao.
3. Kitaifa, kigugumizi juu ya janga la UKIMWI kimepungua na unyanyapaa wa waathirika pia umepungua sana.
4. Msimamo wa Serikali umeungwa mkono na wahisani kwa kutoa misaada kwa wingi na kwa uwazi.
5. Vijana wamehamasika sana na wamekuwa wakishiriki katika mapambano kwa fani mbalimbali kama ISHI na kadhalika.
6. Serikali imeanzisha mpango wa kutoa dawa za kupunguza makali ya UKIMWI kwa waathirika bila malipo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ingawa utafiti haujafanywa kwa nchi nzima, tunaamini kuwa ufahamu juu ya UKIMWI umewafanya wananchi walio wengi kuwa waangalifu zaidi dhidi ya maambukizi. Dalili kubwa ni jinsi watu wanavyojitokeza kwa wingi kupima afya zao. Hali kadhalika ni ule uwazi wa kujadili masuala ya ngono unaoanza kujitokeza baina ya wanaume na wanawake. Yote hayo ni mafanikio ya kampeni hizi. Ongezeko tunaloliona sasa katika jamii ni la wagonjwa ambao waliambukizwa miaka iliyopita na sasa wanaanza kuumwa.

**MHE. ESTHERINA KILASI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina maswali mawili.

(a) Kwa kuwa nchi jirani zimefanikiwa kupunguza sana kasi uenezaji wa Ukimwi kwa mfano Uganda kwa kutangaza pale vifo vinapotokea kwamba mgonjwa aliyefariki, amefariki kwa ugonjwa fulani wanakuwa wazi na pale madaktari wanapopima kueleza

wazi kwamba mgonjwa anayeumwa anaumwa UKIMWI. Je, ni lini Serikali itaamua sasa kuanza rasmi kutangaza vifo vya wagonjwa kwamba wamesababishwa na Ukimwi na si vinginevyo? (*Makofi*)

(b) Kwa kuwa utoaji wa dawa za kurefusha maisha ya waathirika wa UKIMWI imekuwa ni tatizo kwa Makao Makuu ya Wilaya zote na hasa baada ya Wizara ya Afya kuamua kuteua baadhi tu ya hospitali kutoa madawa ya kurefusha maisha ya waathirika wa Ukimwi. Je, ni lini Serikali sasa itaanza kutoa madawa ya kurefusha maisha kwa waathirika kwenye Hospitali zote za Wilaya ili wananchi waweze kufaidika na huduma hizi za dawa za Ukimwi. Ahsante. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA AFYA (K.n.y. WAZIRI MKUU):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali ya Mheshimiwa Estherina Kilasi, kama ifuatavyo:-

Kuhusu suala la kutoa taarifa ya kwamba mgonjwa fulani amekufa kwa ugonjwa wa Ukimwi, bado linabaki ni suala la maadili ya madaktari, *medical ethics* haziruhusu kwa daktari kutangaza ugonjwa wa mgonjwa. Kwa hiyo, bado suala linabaki ni jukumu la ndugu na jamaa kuamua kufanya hivyo na siyo madaktari. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu Serikali kutoa dawa za kurefusha maisha kwa baadhi tu ya Hospitali za Wilaya, naomba nijibu swali hili kwamba Serikali kupitia mpango wake wa matatizo imeweka awamu katika kutoa matibabu. Kwa kuwa nchi hii ni kubwa na watu wengi haingewezekana kutoa matibabu kwa nchi nzima kwa wakati mmoja. Hivyo ni vituo 32 ambavyo vimeanza matibabu ni nia na matakwa ya Serikali kwamba tutakuwa tunaongeza vituo hivi kadri fedha zinavyopatikana hatimaye kufikisha matibabu haya nchi nzima. Kwa mwaka huu tunategemea wagonjwa 44,000 kuwekwa katika matibabu na mpango wa matibabu umepangwa kufikisha matibabu kwa watu 500,000 katika kipindi cha miaka 5. (*Makofi*)

Na. 62

### **Ubadhirifu wa Fedha za Umma**

**MHE. MGANA I. MSINDAI (k.n.y. MHE. RAPHAEL N. MLOLWA)** aliuliza:-

Kwa kuwa, taarifa ya mwaka 2002 ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Hesabu za Serikali za Mitaa, inaonyesha kwamba Halmashauri nyingi ama zilipata hati zenyet dosari na kwa kuwa msukumo wa sasa wa maboresho unafanya Halmashauri kupokea toka Serikali Kuu mabilioni ya fedha na wakati huo Halmashauri nyingi hazina wahasibu wenye sifa stahili na kwamba ipo sheria ya fedha inayokataza taasisi ya umma kuajiri watumishi wasio na sifa stahiki kusimamia mabilioni ya fedha za umma;

(a) Je, Serikali haioni kwamba inakiuka sheria hiyo na kwamba taarifa zake za kila mwaka kulaani ubadhirifu wa fedha katika taasisi za umma ni kiini macho tu, kwani inajua chanzo cha msingi wa tatizo hilo?

(b) Je, Serikali ina mipango gani mahsusini yenyе matumaini ya kuondokana na tatizo hilo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Raphael N. Mlolwa, Mbunge wa Kahama, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kwa mujibu wa kifungu cha 7 (1) cha Sheria ya Bodi ya Uhasibu na Ukaruzi Na. 33 ya mwaka 1972 iliyorekebishwa na sheria Na. 2, 1995 kinakataza mtu ye yote asiye na sifa kuitwa au kuiita Mhasibu au Mkaguzi. Sheria hiyo inataka wahasibu na wakaguzi wote kupata mafunzo stahili na kusajiliwa na Bodi ya Wahasibu na wakaguzi (*NBAA*). Kwa mantiki hii mtu asiye na sifa za uhasibu hapaswi kusimamia masuala ya fedha wala kuiita Mhasibu.

Mheshimiwa Spika, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali katika hesabu za mwaka 2003, ametoa taarifa inayooonesha kama ifuatavyo: Halmashauri 39 zilipata hati safi, Halmashauri 50 zilipata hati lenye masharti, Halmashauri 27 zilipata hati chafu na Halmashauri moja haikukaguliwa kutokana na kucheleta kuwasilisha hesabu kwa wakaguzi.

Hali hii ya usimamizi wa fedha ambayo inaonekana kusonga mbele inatokana na ukweli kwamba Halmashauri zipatazo 112 zina watanza hazina wenyе sifa za Chuo Kikuu au zaidi na Halmashauri 5 zina watanza hazina walio na sifa za chini ya Chuo Kikuu. Aidha hivi sasa Halmashauri zilizo nyingi zina Wahasibu kati ya watu hadi wanen walio chini ya mweka hazina jambo ambalo linadhahirisha jinsi suala la kujitosheleza taaluma ya uhasibu nchini linaendelea kuwekewa kipaumbele na Serikali.

Vile vile Serikali inaendelea kutoa mafunzo kwa Wafanyakazi wa Idara ya fedha ikiwa ni mwaka wa tatu mfululizo kuanzia mwaka 2002/2003. Halmashauri ambazo hazina waweka hazina wenyе sifa ni pamoja na Mtwara/Mkindani, Ngorongoro, Kilosa, Kilombero na Karatu. Juhudi za kuhakikisha zinapatiwa waweka hazina zinafanywa na Halmashauri kwa kushirikiana na Ofisi yangu na punde zoezi hilo litakapomilizika tuna hakika nao watapata wenyе sifa. Pamoja na kwamba wakuu hawa wa Idara hawana sifa za kiwango cha Chuo Kikuu bado Halmashauri za Wilaya ya Karatu, Kilombero na Ngorongoro zilipata hati safi wakati Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa ilipata hati lenye masharti. Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara/Mikindani ndiyo hesabu zake hazikukaguliwa kwa wakati kwa zaidi ya miezi 8.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikisisitiza Halmashauri zote kuzingatia Sheria na Kanuni za Fedha. Serikali inachukua hatua hizo ili kuimarisha utendaji na siyo

kwamba ni kiini macho. Ni matamshi ya dhati na pale inapobainika kwamba upo ubadhirifu hatua kali zimekuwa zikichukuliwa dhidi ya wahusika.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa na mipango mbalimbali katika kupunguza tazito la utendaji kazi kwa Wahasibu na Wakaguzi katika Halmashauri nchini. Kwa mfano tangu mwaka 2002 hadi 2004 kupitia Wizara ya Fedha, Serikali imekuwa ikiwafundisha wahasibu toka kila Halmashauri katika Vyuo vya Uhasibu vya Arusha, Dar es Salaam na *IFM* kwa gharama ya Serikali Kuu. Aidha mpango wa uboreshaji mfumo wa Serikali za Mitaa tangu mwaka 2000-2004 umefundisha jumla ya wahasibu 128, kuhusu menejimenti ya fedha na utumiaji na utunzaji wa fedha kwa kutumia mfumo wa kompyuta (*Epicor System*). Uamuzi huu wa Serikali umesaidia sana kwani kwa mujibu wa taarifa hizo za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali kwa Hesabu za Serikali za Mitaa zinaonyesha kuongezeka kwa hati safi toka hati 3 mwaka 2001 hadi 39 mwaka 2003. Aidha hati chafu zimepungua toka hati 68 mwaka 2001 hadi 27 mwaka 2003. Ni matarajio yangu kuwa mafunzo haya yataendelea kuboresha utendaji kwa wahasibu na kupunguza kero zilizopo hivi sasa. (*Makofî*)

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kunipa nafasi niliulize swalii. Vile vile nashukuru kwa majibu mazuri yaliyotoka kwa Naibu Waziri. Kwa kuwa kuna baadhi ya Halmashauri ikiwemo Halmashauri ya Mji wa Kigoma Ujiji pamoja Mwanga Mkoani Kilimanjaro bado zinatumia wahasibu wa ushirika. Kwa kuwa wahasibu waliosomea Chuo cha Ushirika elimu yao haiendani na Halmashauri za Wilaya, Je, Serikali itahakikisha Wilaya zote zinapata wahasibu wenye sifa? (*Makofî*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, sikueleza sana juu ya aina ya wahasibu tulionao katika Halmashauri zetu. Lakini nakubali kabisa kwamba alilolisema Mheshimiwa Msindai ni kweli, lakini tunawahesabu kwa kipindi hiki ambacho bado tunajizatiti kwamba wanafanya kazi inayofanana na wahasibu kwa kutokana na viwango vyao ambavyo walivyonyavyo hivi sasa. Lakini ni dhahiri kabisa kama nilivyosema kwamba lengo ni kuwa wahasibu amba kwa kweli wanatakiwa kufanya kazi hiyo katika Halmashauri zetu amba wamebobea katika masuala ya uhasibu.

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO (K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MIKOZA):** Mheshimiwa Spika, naomba niongezee majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri kuhusu taaluma ya uhasibu inayotolewa na Chuo cha Ushirika Moshi. Nataka kulihakikisha Bunge lako Tukufu kwamba Chuo cha Ushirika Moshi, kinafundisha taaluma ya uhasibu wa juu. Kwa hiyo, kazi zote za uhasibu zinazofanywa na watu hawa zinastahili. (*Makofî*)

**MHE. BEATUS R. MAGAYANE:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Serikali, kwa kuwa kigezo kimojawapo muhimu kwa Serikali kutoa ruzuku isiyokuwa na masharti kwa Halmashauri ni pamoja na kupata hati safi. Je, Serikali haioni kwamba itakuwa inawaonea wananchi kwenye Halmashauri ambazo hazitapata hati safi kutokana na ukweli kwamba hazina watendaji wenye sifa zinazotakiwa? (*Makofî*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, mimi nafarijika kwa sababu katika maelezo yangu nimeeleza waziwazi ni Halmashauri ngapi tuna wahasibu wenye sifa zinazotakiwa na nikasema ni Halmashauri tano ndizo zina wahasibu ambao wako kidogo chini ya kiwango cha Chuo Kikuu. Lakini nikasema kwa makusudi kwamba katika hizi tano, 4 ni kati ya Halmashauri ambazo zimepata hati safi na moja ya masharti. Kwa hiyo, la msingi hapa ni kwamba hati safi kwa sehemu kubwa inatokana na Halmashauri zenyewe zinavyofanya kazi za kusimamia masuala ya fedha kwa namna ambavyo itawezesha kupata hati safi.

Kwa hiyo, mimi naomba Waheshimiwa Wabunge, mimi nadhani tubanane zaidi kwenye Halmashauri zetu. Halmashauri nyingi kabisa zina wahasibu wenye sifa lakini bado zinapata hati chafu. Hilo nadhani ndiyo swali la kujiuliza iweje kwenye Halmashauri ambayo mhasibu yupo mwenye sifa lakini mmepata hati chafu. (*Makofi*)

Na. 63

#### **Wananchi Waliohamishwa Kutoka Eneo la Ng'ande.**

**MHE. MOHAMED A. ABDULAZIZ** aliuliza:-

Kwa kuwa, wananchi waliokuwa wanaishi kwenye eneo la Ng'ande Kata ya Rahaleo - Mjini Lindi wamehamishwa kutoka kwenye makazi hayo kwa madai kwamba eneo hilo ni la Hospitali ya Mkoa yaani Sokoine Hospitali na kwa kuwa wananchi hao wameishi kwenye eneo hilo kwa zaidi ya miaka 60 bila kujulikana kwamba eneo hilo ni la hospitali na kwa kuwa wananchi hao walikuwa na nyumba, mazao ya kudumu pamoja na mali nyingine mbalimbali:

- (a) Je, Serikali inatoa kauli gani kuhusu fidia kwa mali za wakazi hao waliohamishwa hasa ikizingatiwa kuwa wananchi hao wameishi kwenye eneo hilo kwa muda mrefu hata kabla ya kujengwa Hospitali hiyo?
- (b) Kulingana na kiwango cha uungwana walichokionyesha wananchi wa Ng'ande cha kuhamza bila kusukumwa wala kusababisha vurugu za aina yoyote kwa manufaa ya Taifa lao. Je, Serikali itakuwa tayari kuwathibitishia wananchi hao kwamba eneo hilo litatumika kwa ajili ya hospitali tu na sio kwa ajili ya ujenzi wa makazi au hoteli?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Abdulaziz, Mbunge wa Lindi Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, eneo la Hospitali ya Mkoa wa Lindi ya Sokoine, lilipimwa mwezi Januari 1957 na michoro yake kupata kibali cha Mkurugenzi wa Ramani Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi. Aidha, wakati eneo hilo linapimwa yalikuwepo majengo machache ya Hospitali. Katika mchoro uliopo (*detail picking*) wa mwaka 1957 haionyeshi kama kulikuwa na nyumba yoyote katika eneo husika kwa wakati huo. Wananchi baadaye walianza kuingia katika eneo hilo kidogo kidogo na kuanza kupanda mazao ya kudumu bila kibali cha mmilikaji wa eneo.

Mheshimiwa Spika, mnamo mwezi Julai, 2003 wananchi wa eneo la Ng'ande walihamishwa kutoka eneo hilo kwani kuwepo kwao katika eneo la Hospitali kulikuwa kunaathiriri shughuli mbalimbali kama vile usalama na upanuzi wa hospitali. Hata hivyo wananchi wote waliohamishwa wote wamepatiwa viwanja vya kujenga makazi mapya katika eneo la Muhimbili katika Kata ya Rasbura hapa Lindi Mjini. Hivyo suala la Serikali kulipa wananchi hao fidia katika mazingira niliyoyaeleza ni jambo ambalo haliwezekani.

(b) Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru wananchi wote waliohamishwa kutoka eneo la Ng'ande kwa uungwana wao kwa kukubali kuhama bila vikwazo. Ni wazi kwamba walielewa vizuri umuhimu wa kutekeleza maelekezo ya Serikali kwa manufaa yao na Taifa kwa ujumla. Napenda kuwathibitishia wananchi hao kwamba eneo waliohamishwa litatumika kwa ajili ya shughuli za hospitali kama ilivyoidhinishwa na Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi.

**MHE. HENRY D. SHEKIFFU:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba wananchi hawa wa Lindi wamekubali kuondoka katika eneo hilo kwa busara tu. Lakini lipo tatizo kubwa ambalo linakabili maeneo mengi.

Wananchi wanaingia katika maeneo bila kujua na wale viongozi waliowekwa katika maeneo hayo hawawaelekezi wananchi hao kwamba maeneo haya yametengwa kwa shughuli maalum. Baadaye wananchi wanakuja kupata hasara kubwa sana kwa uzembe uliofanyika kwa viongozi waliokuwa katika maeneo hayo. Je, Serikali inaonaje kuwalipa fidia wananchi hawa kwa sababu makosa siyo yao ni ya wale walopewa Mamlaka? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, masuala haya ya fidia kutokana na shughuli mbalimbali ambazo zinajitokeza ambazo zinaathirika wananchi zina taratibu zake za kisheria na ndiyo maana misingi hii wakati wote ndiyo inayozingatiwa.

Katika suala hili nilivyolieleza na maeneo mengine ambayo vile vile yamejitokeza ikiwa na pamoja na watu wanaojenga katika maeneo ya hifadhi ya barabara msingi ni ule ule tu kwamba ilimradi sheria imewekwa kuhakikisha kwamba maeneo haya yaliyotengwa ni jukumu lao vile vile wananchi kabla hujaingia katika maeneo hayo jaribu kucheki kuititia Wizara ya Ardhi, vyombo vinavyohusika, viongozi waweze kukusaidia kuweza kujua kwamba uko katika eneo ambalo ni salama.

Lakini kwa msingi wa swali la Mheshimiwa Shekiffu ni dhahiri kabisa kwamba Halmashauri nazo zinapaswa kufanya kazi hiyo kwa dhati ili kuhakikisha kwamba wananchi wake hawapati matatizo kama haya. (*Makofit*)

Na. 64

### **Mikopo kwa Vyombo vy'a Usafiri kwa Walimu**

#### **MHE. KABUZI F. RWILOMBA aliuliza:-**

Kwa kuwa mwaka 1998 kulikuwa na mpango wa Serikali kupitia *TSC* wa kuwakopesha walimu vyombo vy'a usafiri na kwa kuwa ni badhi tu waliokopeshwa vyombo hivyo na wengine baada ya utaratibu kuvurugika walirudishiwa fedha zao mwaka 2003 kupitia agizo la Bunge na kwa kuwa wapo wengine ambao hawajarudishiwa fedha zao kama vile Hamis Kisidi ambaye anadai shilingi 800,000/=, shule ya msingi Kalembo na Antipas Moshi wanaodai sh.1,006,000/= wa shule ya msingi Nyerere (Dodoma na wengine wengi):-

- (a) Je, Serikali itawalipa lini fedha zao?
- (b) Kwa kuwa sasa ni muda mrefu umepita na thamani ya shilingi inashuka kila siku. Je, Serikali itakuwa tayari kulipa pamoja na madai ya riba ya asilimia 10% kila mwezi kwa kipindi chote kwa kutowajibika ipasavyo?

#### **WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA aliijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge naomba kwanza kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Inua Hadhi ya Walimu ulikuwa ni mfuko wa hiari ambapo mwalimu yejote aliyetaka kujiunga na mfuko huo alitakiwa kulipa kiingilio pamoja na mchango wake moja kwa moja kupitia benki.

Mheshimiwa Spika, takriban walimu wote wenyewe madai ambao walikuwa wanaudai mfuko wa Inua Hadhi ya Walimu walilipwa madai yao kulingana na uhakiki uliofanywa na Tume iliyoteuliwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo wapo walimu wachache ambao hawakulipwa kutokana na upungufu wa vielelezo au kukosekana kwa vielelezo muhimu ili kuthibitisha madai yao. Walimu wote waliokuwa wanaudai Mfuko walitakiwa waete vielelezo walivyolipia benki (*pay in slip*) kwani ndio njia pekee ya uthibitisho wa malipo yaliyofanywa.

Mheshimiwa Spika, idadi ya walimu wa Mkoa wa Dodoma waliokuwa wanaudai Mfuko na vielelezo vyao kuhakikiwa na Tume ni 30 tu. Waliolipwa ni 28 na walimu 2

ambao ni Antipas Moshi ambaye hakulipwa kutokana na kukosa risiti za fedha alizolipia benki na Hamis Kisidi hakukamilishiwa madai yake kutokana na kushindwa kukamilisha vielezo vya benki.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya naomba sasa kujibu swal la Mheshimiwa Rwilomba, Mbunge wa Busanda, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwa rejea ya maelezo yangu hapo juu, Tume kwa wakati wowote iko tayari kulipa madai ya walimu wanaodai fedha zao kutoka katika mfuko huo ili mradi tu wanatekeleza sharti la kuwasilisha vielelezoo vinavyotakiwa.

(b) Mheshimiwa Spika, kama nilivyokwisha sema mfuko huu ulikuwa ni wa hiari na mwalimu ye yote ali yependa alijunga kwa hiari yake, hivyo Serikali haiwezi kulipa riba au fidia ye yote kutokana na mpango huu, kwa sababu, ucheleweshaji wowote ulio jitokeza unatokana na wahusika kutokuwasilisha vielelezoo vyao mapema.

**MHE. PAUL E. NTWINA:** Nakushukuru Spika kunipa nafasi kuuliza swal dogo sana la nyongeza. Kwa kuwa mpaka sasa Serikali imelipa madai ya karibuni kabla ya Tume ile ya Mheshimiwa Msindai na wenzake kupita. Je, madai yale ya mwanzoni yatlipwa lini ambayo ni mengi? Tume ya Omar Kwaangw'. (*Makofî/Kicheko*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Spika, Tume ya Mheshimiwa Omar Kwaangw' na Mheshimiwa Msindai ilikuwa inahakiki madai mengi sio hii ambayo inahusiana na swal nililojibu hapo awali. Lakini kuhusiana na Mfuko huu wa hiari, Tume iliyofanya hiyo hakiki ni nyingine na ni walimu wachache sana ambao hawajalipwa ambao kwa kiasi kikubwa wamekosa kulipwa kwa sababu wao wenye hawajaleta vielelezoo vinavyotakiwa.

Kuhusu madai ya walimu mengine ambayo hayajalipwa Serikali itaendelea kuwalipa watumishi wake wote kulingana na uwezo na pamoja na uhakiki ambao umefanywa kila mara.

**MHE. ISMAIL J. R. IWVATTA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nikushukuru kunipatia nafasi niulize swal la nyongeza. Namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri. Kutokana na maelezo ya Mheshimiwa Waziri ni kwamba walimu wahusika ambao hawajalipwa hawakuweza kuonyesha stakabadhi zao za kulipia pesa benki (*pay in slip*) kwa sababu hawa walimu inawezekana ni kwa bahati mbaya sana wamezipoteza hiso. Lakini kwa kawaida kupitia benki kuna kitu kinaitwa *Bank Statement* inaweza ikapatikana na ikaonyesha rekodi inayoonyesha kwamba pesa iliingizwa tarehe fulani. Kwa nini Serikali isiwe na uungwana wa kutumia hiso rekodi za benki kwa maana ya *Bank Statement* ili hawa walimu wakapata haki zao? (*Makofî*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Spika, naomba kutumia mfano wa mwalimu *Antipas Moshi* ambaye hakuwa na risiti alizolipia fedha benki baada ya mwalimu huyo kuomba madai

yake au alipwe madai yake, Serikali ilimshauri aende benki kupata statement hiyo na tunangojea alete hiyo statement ili tuweze kumlipa lakini bado hajarudi.

Nina hakika si rahisi kwa mtu mwingine ambaye hajalipa hizo fedha benki kwenda benki kuomba stakabadhi bali yule aliyepeleka fedha zake ndiyo ambaye atapewa stakabadhi hiyo ama siyo kutatokea wizi ambao utakuwa umetokea kwa sababu ya kutokufuata taratibu za malipo ya fedha benki.

Na. 65

### **Mita za Mafuta Kwenye Vituo vya Mafuta**

**MHE. ZUHURA SHAMIS ABDALLAH** aliuliza:-

Kwa kuwa zipo tetesi kuwa mita za kusoma kiwango cha mafuta katika vituo vya mafuta Dar es Salaam hazipo katika viwango sahihi hivyo husababisha wanunuzi wa mafuta hayo kuwa na hofu ya kuibiwa kwa njia hiyo:-

Je, ni taasisi gani inayohakiki na kujua usahihi wa mita hizo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zuhura Shamis Abdallah, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, inawezekana baadhi ya mita za kusoma viwango vya mafuta kwenye badhi ya vituo vya mafuta hazipo katika viwango sahihi. Tatizo hili linaweza kutokana na uchakavu wa mashine yaani (*pump*) pamoja na mita zenyewe.

Mheshimiwa Spika, ikigundulika hivyo mwenye kituo cha mafuta hushauriwa kubadilisha mita hizo mara moja na asipotekeleza ushauri huo huchukuliwa hatua za kisheria. (Sheria ya Vipimo ya Mwaka 1982) inahusika na suala hili.

Aidha, napenda kutoa ushauri kwa wanunuzi wa mafuta kuwa mara wanapopata tatizo hili watoe taarifa mara moja kwa vyombo husika ili hatua za kurekebisha tatizo hilo zichukuliwe mara moja. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, tasisi inayohakiki na kujua usahihi wa mita katika vituo vya kuuzia mafuta ya petroli nchini ni wakala wa vipimo yaani (*weights and measures agency*) chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Spika, wakala wa vipimo wana Ofisi kila Mkoa nchi nzima kwa ajili ya kuhakiki viwango vya vifaa mbalimbali, zikiwemo mita za kusoma ujazo wa mafuta katika vituo vya kuuzia mafuta ya petroli.

Kazi hii ya kuhakiki hufanyika mara moja kwa mwaka nchi nzima, lakini kama wakala wakipokea taarifa zinazoashiria kiwango duni cha mita kusoma ujazo halisi za mafuta katika kituo/vituo vya mafuta basi wakala huo uhakiki hufanyika upya na kwa haraka.

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Spika, ningependa kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na matatizo haya ya mita yanayozungumziwa. Je, Waziri anaweza kutuambia na ingawa hakuna udhibiti wa bei ya mafuta lakini Waziri anaweza kutueleza kwa nini kunakuwa tofauti mno kati ya kituo na kituo kwa mfano kituo kimoja kinaweza kuwa kinauzwa bei lita moja sh.1,000 wakati kingine kinauzwa 650 kwa nini kunakuwa na tofauti, huu si unyonyaji?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kama ambavyo Mheshimiwa Mzindakaya mwenyewe amesema kwa kuwa hakuna udhibiti wa bei kwa maana ya kwamba tuko katika mfumo wa uchumi wa soko na moja ya mambo ya uchumi wa soko ni ushindani. Na endapo katika kituo kimoja kuna mafuta anauza sh.1,000 na kingine 950 basi nenda kwenye kituo cha mafuta kinachouza 950 ndiyo faida ya ushindani huo. Hiyo ndiyo sababu yake kwa kweli ni vizuri kwamba kuwe na ushindani kama huu ili watumiaji waweze kufaidika.

**MHE. SEMINDU K. PAWA:** Nashukuru sana Mheshimiwa Spika, kunipa nafasi hii kuuliza swali moja tu la nyongeza. Kwa kuwa Waraka ule ulioko Wizara ya Viwanda na Biashara unafanya kazi mzuri sana kupima kabla ya tahadhari. Lakini hili tukio la swali nauliza la msingi ni tukio la wizi wa watu kuwaibia mafuta pungufu, je suala hili tunapogundua je baada ya kupeleka katika wakala ule uliotajwa tunaruhusiwa kupeleka Polisi kwa sababu ni suala la wizi na kugushi?

**WAZIRI WA BIASHARA NA VIWANDA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kwamba yule ambaye anauza mafuta kwa kutokuzingatia sheria ya vipimo basi hayo anafanya kosa la jinai na inastahili kupelekwa Mahakamani kwa kuititia Polisi. Ahsante. (*Makofî*)

**MHE. ELIACHIM J. SIMPASA:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika. Licha ya kwamba bei zinatofautiana ili mnunuzi aweze kununua kituo gani. Je, vituo ambavyo havionyeshi kabisa bei kila mahali ni sifuri tu mpaka mwisho. Huu ndiyo utaratibu unaamua namna gani kununua, hiyo ndiyo biashara ya namna gani? Hujui bei ya bidhaa imeandikwa sifuri kutoka mwanzo mpaka mwisho. Kituo kimojawapo kipo pale *Nyerere grounds* kwenye *Nyerere Trade Fair* pale, ni sifuri tu, pentroli sifuri, dizeli sifuri, kila kitu sifuri, ni nchi gani inafanya biashara ya namna hiyo? (*Makofî*)

**WAZIRI WA BIASHARA NA VIWANDA:** Mheshimiwa Spika, hilo nalo ni kosa kisheria kwa kutumia Sheria ya *Fair Competition Act* ya mwaka 2003. Kwa hiyo, suala hili nalo linaweza kufikishwa Mahakamani.

**Ujambazi Siha**

**MHE. DR. MAKONGORO M. MAHANGA (K.n.y. MHE. AGGREY D. J. MWANRI)** aliuliza:-

Kwa kuwa, mwaka 2002 majambazi yalivamia duka la mwananchi mmoja katika kijiji cha Koboko jimboni Siha na kumjeruhi mke wake na vile vile kupora kiasi cha sh.1,000,000/= na zaidi na kwa kuwa majambazi wengine waliwavamia wananchi waishio katika Kata ya Siha Magharibi na kufyatua risasi zilizowafanya wananchi kujihami kwa kuwaa majambazi hao:-

- (a) Je, uchunguzi wa Polisi ulibaini nini katika matukio hayo mawili?
- (b) Je, Serikali imechukua hatua gani za kuhakikisha kwamba vitendo kama hivyo vinavyohatarisha amani na usalama wa raia na mali zao havitokei tena?
- (c) Je, wananchi wanatakiwa kuchukua tahadhari gani ili matukio ya aina hiyo yasiendele kutokea?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mbunge wa Siha, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba mwaka 2002 kulitokea matukio ya ujambazi wa kutumia silaha katika Jimbo la Siha. Tukio la kwanza lilitokea katika kijiji cha Koboko ambako majambazi watano (5) wakiwa na silaha aina ya bastola waliwavamia wafanya biashara wawili na kuwapora fedha na mali zenyet thamani jumla ya sh.1,184,000/=. Polisi kwa kushirikiana na raia wema walifanikiwa kuwatia mbaroni watuhumiwa wawili ambao baada ya kufikishwa Mahakamani walipatikana na hatia na kupewa kifunguo cha miaka thelathini (30) jela.

Katika tukio la pili, majambazi wapatao saba (7) wakiwa na bunduki aina ya *short gun* walivamia duka la mwananchi mmoja na kupora mali yenyet thamani ya sh.100,00/= Wananchi kwa ujasiri mkubwa waliwazingira majambazi hao na watano kati yao waliuawa, vile vile bunduki moja, bastola moja, na risasi moja vilikamatwa. Uchunguzi wa Polisi katika matukio yote haya unaonyesha kwamba majambazi wote walioitiwa mbaroni katika matukio yote mawili ni wenyeji wa kijiji cha Kashashi, Kata ya Siha Mashariki, ni vijana wenyeji wa eneo hilo na walifanya ujambazi huo kwa nia ya kupata mali.

Ili kudhibiti vitendo vya ujambazi vinavyohatarisha amani na usalama wa raia na mali zao, Serikali inatoa wito kwa wananchi wa Siha na kwingineko hapa nchini kuchukua hatua zifuatazo:-

- (i) Kuimarisha ulinzi wa sungusungu katika kila sehemu na hivyo kuweza kulisaidia Jeshi la Polisi kuendesha doria mitaani na vijijini.
- (ii) Kutoa taarifa mapema katika vituo vya Polisi wanapokuwa na mashaka na mtu yoyote.
- (iii) Halmashauri za Wilaya na Miji na Manispaa ziimarishe mipango endelevu ya kusaidia vijana wasio na ajira ili waweze kujiajiri kupitia kilimo, biashara ndogo ndogo na utoaji wa huduma ili wajipatie mapato halali na kujiepusha na njia haramu za kujipatia mapato.

Mwisho Mheshimiwa Spika, tunatoa pongezi kwa Mheshimiwa Mwanri na kwa wananchi wa Jimbo la Siha kwa mipango yao mizuri ya ulinzi iliovezesha majambazi kutiwa mbaroni katika matukio yote mawili. Moyo huo wa ujasiri udumishwe na uigwe na wananchi wengine katika maeneo mengine nchini. (*Makofii*)

**MHE. DR. MAKONGORO M. MAHANGA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ningependa kuuliza swali moja la nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa matumizi ya silaha na majambazi kama ilivyojidhihirisha katika jimbo la Siha pia linakumba maeneo mengine kama jimbo la Ukonga ambapo majambazi kwa kutumia silaha wamekuwa wakitishia na kuwaua na kuwanyang'anya wananchi mali zao na kwa kuwa juhudzi za jeshi la polisi ikishirikiana na sungusungu na wananchi pamoja na kazi mzuri iliyofanyika, bado kuna tatizo kubwa. Je, Serikali itakubali kwamba Jeshi la Polisi sasa ukiacha sungusungu na wananchi lishirikiane na jeshi la wananchi kufanya operesheni maalum ya kutokomeza ujambazi kwa kipindi fulani katika maeneo yetu hasa mijini? (*Makofii*)

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba tunalo tatizo la majambazi kutumia silaha na tatizo hili ni tatizo linalozikabili nchi karibu zote za Ukanda huu wa Maziwa Makuu kutokana na migogoro iliyomo ndani ya badhi ya nchi katika ukanda wetu ambazo zina vita vya wenyewe kwa wenyewe na wakimbizi wanakwenda huku na huku, wanakuja na silaha.

Ni tatizo ambalo ni la Tanzania, lakini vile vile ni la nchi zote za Ukanda wa Maziwa Makuu. Kwa hapa nchini kama alivyosema Mheshimiwa Makongoro wananchi wema na Jeshi la Polisi wanafanya juhudzi kubwa sana kupambana na majambazi hao, kukamata naona karibu kila mara mnaona huwa tunachoma silaha na mwezi Mei 2005 tutachoma zingine 1,000 ni katika hizi ambazo tunazikamata.

Kwa hiyo, juhudzi hizi zitaendelea, tunaomba wananchi waendelee kutoa ushirikiano kwa polisi na kutumia jeshi la wananchi na utaratibu upo wa kawaida. Mara kwa mara Serikali ikiona inafaa huwa tunakaribisha vyombo vyote vya ulinzi pamoja na

Jeshi la Wananchi katika kufanya opeshereni maalum. Kwa hiyo, ukifika wakati huo hilo litafanyika, liko ndani ya utaratibu.

**MHE. HALIMENSHI K. R. MAYONGA:** Nakushukuru Mheshimiwa Spika kunipa nafasi niweze kuuliza swali moja tu la nyongeza. Kutokana na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa aliywahi kuwa Waziri wa Mambo ya Ndani, Bwana Mrema aliweka utaratibu wa wale wanaofichua majambazi kupata zawadi.

Sasa je, si wakati muafaka ili kupunguza kasi hiyo ya watu wanaoficha silaha kinyemelanyemela wanaojificha kwenye vikundi vya watu waowafahamu. Je, zawadi hizo haziwezi kufahamika kikamilifu ili kupunguza kasi hiyo hasa Mkoani Kigoma na Kagera ambako wameshatubomoa bomoa tunaenda kwa hofu. Je, linawezekana hilo? Hapo sasa. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, utaratibu aliousema Mheshimiwa Mbunge wa kutoa zawadi kwa wananchi ambao wanasaidia Polisi ama kukamata jambazi ama kukamata silaha. Utaratibu upo. Liko fungu maalum linaitwa *criminal investigation fund* yaani mfuko malum wa kupambana na majambazi. Mfuko huu unatoa zawadi.

Kwa hiyo, kuititia Bunge hili tukufu ningependa sasa kuwatangazia wananchi wote na wa Kigoma na kila mahala kwamba yule anayeisaidia Polisi tukakamata silaha, au tukakamata jambazi, hizo zawadi, mfuko wa *CIF* upo na tutawapa. Kwa hiyo, tunawakaribisha watoe hizi taarifa zawadi zipo.

Na. 67

#### **Huduma Muhimu kwa Askari Polisi**

#### **MHE. YAHYA KASSIM ISSA** aliuliza:-

Kwa kuwa askari wanapokaa *Ditach* mara nyingi wanakuwa hawana mawasiliano ya simu au redio na vile vile wanakuwa hawana usafiri na kwa kuwa hata mlo wao huwa duni, hawapewi chai wala hawana fedha za matumizi mengine:-

- (a) Je, ni sababu zipi zinazosababisha askari hao kuwa na mlo duni?
- (b) Je, kwa nini suala la mawasiliano kwa askari hao lisipewe umuhimu unaostahili?

#### **NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Yahya Kassim Issa, Mbunge wa Chwaka, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, askari wote waliopo Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar wanafanya kazi kwa mujibu wa Sheria (*Police General Orders Cap. 322*) na vile vile kufuata kanuni za fedha (*Financial Orders*) zinazoweka bayana haki, wajibu na maslahi ya askari wanapokuwa kazini.

Aidha, askari waliopo katika Mikoa ya Tanzania Zanzibar hawakai huko wakiwa *Detach*, kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge, bali wako huko kufanya kazi za Polisi kama walivyo askari wengine popote nchini na sio sahihi kwamba wanakosa mlo na fedha za matumizi kwa sababu wanapata mishahara na posho ya resheni kama askari wenzao wote wanavyopata katika maeneo mengine.

(b) Mheshimiwa Spika, suala la mawasiliano kwa jeshi la polisi linapewa umuhimu mkubwa sana kwa sasa kwa mfano kwa hivi sasa kila kituo kitapewa *radio* kubwa na askari wanaopangwa doria sehemu mbalimbali wanaitumia radio za mikononi ili kutoa taarifa muhimu kupitia radio kubwa iliyuopo kituoni.

Aidha, mawasiliano katika vituo vyote vya jeshi la Polisi yataendelea kuboreshwa kwa kadri hali ya uchumi itakavyokuwa nzuri zaidi. Mwaka jana mwishoni Desemba Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alizindua mtambo wa kisasa wa mawasiliano ya Jeshi la Polisi uliogharimu shilingi 2.7 bilioni.

Mtambo huu utaanza kutoa huduma katika Mkoa wa Dar es Salaam, Unguja na Pemba. Baadaye huduma ya mtambo huu utasambazwa katika Mikoa yote nchini kwa awamu. Hatua hii italifanya Jeshi letu la Polisi kuwa na mawasiliano ya hakika, bora na ya kisasa kabisa katika eneo letu lote la Afrika Mashariki na Kati.

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kipindi cha Bajeti Waziri aliahidi kwamba usafiri utapatikana. Je, suala hili limefikia wapi?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge kwamba katika hotuba ya bajeti ya Wizara yetu tulisema kwamba katika mwaka huu wa fedha tutanunua magari kwa ajili ya jeshi la polisi ili kutatua matatizo yanayowapata ma-*OCD* na watendaji wengine katika Wilaya mbalimbali.

Mpango huu tumeanza kuutekeleza kama ambavyo mtakuwa mmeshaona Waheshimiwa Wabunge sasa hivi ma-*RPC* ma-Kamanda wa Mikoa yote Tanzania azma hivi karibuni wameletewa magari mapya tena safari hii wameletewa magari ya kisasa *Land Cruiser* ili waweze wakafanya kazi zao vizuri. (*Makofsi*)

Hivi karibuni tumefungua, tumetangaza tenda kwa ajili ya kununua magari 250 ambayo tunatazamia yatatoka kati ya sasa na Juni. Magari haya ndiyo tulioahidi kwamba sasa yatakuja kutatua matatizo kwenye Wilaya kwa maana ma-*OCD* wote watapata magari imara kabisa na *OCID* ambao mwaka jana hawakupata magari sasa hivi watapata magari pamoja na vikosi vingine kama *FFU*, vile vile watapata magari haya ambayo yako njiani. (*Makofsi*)

**MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kunipatia nafasi hii kuuliza swali dogo la nyongeza. Majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nauliza kama hivi ifuatavyo:-

Alisema kwamba hawa Polisi wanapata pesa zao kulingana na utaratibu wa malipo ya fedha lakini, je, lalamiko la Polisi kuwa hizi pesa ambazo wanazipata hawazipati kwa wakati ili wakakidhi yale mahitaji ya kifedha hasa?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, utaratibu wa askari kulipwa fedha zao kwa mfano, mishahara inakwenda vizuri. Ila tu kuna baadhi ya Mikoa na wala si yote, ile posho inayoitwa *Ratio Allowance* ambayo nayo vile vile inalipwa kila mwezi.

Kuna baadhi ya Mikoa ni kweli tumeshapata hayo malalamiko kwamba kinachelewa chelewa. Nataka kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba hili tatizo au malalamiko tumeyapata na tumeshatoa maelekezo kwa Makamanda wa Mikoa michache ambayo ina tatizo hili ili waweze kulirekebisha ni tatizo la kiutendaji au kwa sababu hizi pesa huwa zipo ni tatizo la kiutendaji tutalirekebisha.

Na. 68

#### **Mafanikio yatokanayo na Mifuko ya Afya**

**MHE. SEMINDU K. PAWA** aliuliza:-

Kwa kuwa kazi nzuri na ubunifu wa Serikali kuititia Wizara hii katika masuala mbalimbali ya huduma za afya kwa wananchi kama vile mfuko wa Bima ya Afya, uchangiaji wa tiba, chanjoi na kampeni mbalimbali za magonjwa ya milipuko na magonjwa ambata:-

- (a) Je, hadi Serikali inapojobu swali hili inaliambia nini Taifa juu ya mafanikio yaliyopatikana kutokana na mfuko wa bima ya afya ya jamii, uchangiaji tiba na kupungua kwa milipuko ya magonjwa na chanjo?
- (b) Je, Serikali imechukua hatua gani juu ya matatizo yaliyojitekeza katika uendeshajji, ubadhirifu na kutokuwa makini kwa baadhi ya watendaji wake?

#### **NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Afya napenda kujibu swali la Mheshimiwa Semindu Pawa, Mbunge wa Morogoro Kusini Mashariki, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kuwepo kwa Mfuko wa Bima ya Afya na Mfuko wa Afya ya Jamii kumewezesha wananchi wengi ambao ni wanachama wa Mifuko hiyo na familia zao kwenda kwenye vituo vya kutolea huduma za afya mapema wanapokuwa katika hali ya kuugua kwa vile hawahitajiki kulipia tena gharama za matibabu.

Kwa mantiki hiyo, magonjwa ya milipuko hutambuliwa na kudhibitiwa mapema pindi yanapotokea. Aidha, kuwepo kwa uchangiaji wa Tiba kumewezesha vituo vingi vya kutolea huduma kununua vifaa na dawa za ziada na kufanya ukarabati mdogo mdogo, mambo yaliyopeleka kuboreka kwa huduma kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Spika, utaratibu uliopo wa kutoa msamaha umewezesha makundi yote yenye kustahili, kupata matibabu mapema na hivyo kupunguza kasi ya uambukizaji.

Aidha, Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara yangu imeendelea kutoa chanjo bila malipo kwa watoto chini ya miaka mitano na akina mama wajawazito ili kupunguza tatizo la magonjwa ya kuambukiza.

(b) Mheshimiwa Spika, Halmashauri husika ndiyo msimamizi mkuu na mdhibiti wa dawa, vifaa na fedha walizochangia wananchi. Hivyo, Halmashauri kupitia Kamati za Afya za Halmashauri na Kamati za Afya za vituo vya kutolea huduma za kusimamia na kufuutilia matatizo yanayojitokeza katika uendeshaji, ubadhirifu na utendaji kazi wa matumishi wake na kuchukua hatua zinazostahili kwa wahusika.

**MHE. SEMINDU K. PAWA:** Mheshimiwa Spika, namshukuru kwa majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Nina maswali madogo tu mawili ya nyongeza.

Serikali inaweza ikakubaliana na mimi kufnya marekebisho kwa kuwa Mfuko wa Bima ya Afya unahusiana na familia, kutofanya marekebisho kwa mke na mume wanaokatwa mshahara nani anayefaidi mkakati wa mwenzake na kuongeza idadi ya watoto ni wanne tu? Hiyo (a).

Pili, kuhusu milipuko kwamba milipuko hudhibitiwa mapema, sasa inatokea kuna tabia imezuka hivi sasa inapotokea milipuko tu mnakimbilia Mama Lishe. Nani aliwaambia kipindupindu kinaletwa na pilau? (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Semindu Pawa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, wakati ambapo mke na mume wote ni wafanyakazi, na wanakatwa kuchangia mfuko wa Bima ya Afya, aidha mke au mume anaruhusiwa kuweka watu mbali na wale watoto wake wanne ambao wanaruhusiwa. Kwa maana hiyo endapo baba atakuwa ni mfanyakazi wa Serikali na ye ye ameshaandikisha watoto wa nne ambao anao. Basi, mama anaruhusiwa kuandikisha ndugu na jamaa wengine kwa mujibu ya idadi inayotakiwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu tabia ya Maafisa wa Afya kumwaga vyakula vya Mama Lishe wakati wa milipuko, nataka niseme kuwa utaratibu na utendaji mzuri ni kutoa elimu kwa wahusika ili wahakikishe kwamba milipuko hiyo haiendelei. Kwa hiyo, hapa suala kubwa ni kutoa elimu kwa umma ili kuhakikisha kwamba watu wanajikinga. Lakini inapotokea kwamba tayari hali ya tahadhari kwa maana ya *cuarantee* imeshatangazwa. Halafu bado kuna watu wanauzu vyakula kinyume na utaratibu vyakula ambavyo havina usafi unaotakiwa basi, inakuwa hakuna njia zaidi ya kuhakikisha kwamba vyakula hivyo vinateketezwa.

**MHE. WILLIAM J. KUSILA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa, katika Zahanati nyingi vijijiini na hata Hospitali za Wilaya suala la makundi maalum katika jamii yaliyosamehewa kulipa gharama za uchangiaji wa matatibu bado haliheshimiwi. Makundi kama vile watoto wenye umri chini ya miaka mitano, akina mama wajawazito, vikongwe bado wanadaiwa kuchangia gharama za matibabu.

Je, Serikali itachukua hatua gani ili kuhakikisha kwamba suala hili linaheshimiwa na utaratibu uliopangwa unafuatwa ili kuondoa usumbufu wanaoupata makundi haya ambayo yamesamehewa kuchangia gharama za matibabu? (*Makofî*)

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kusila kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, suala la Msamaha wa Matibabu kwa Makundi Maalum ni Sera ya Serikali. Kwa hiyo, haina budi kuheshimiwa. Isipokuwa tu tatizo liko katika Usimamizi wa Sera hii. Kwa mara nyingine tena naomba nieleze kwamba sasa hivi tumeanzisha Kamati za Afya iwe katika ngazi za Halmashauri kwa maana ya Wilaya zote. Lakini vile vile kuna Kamati za Afya za Vituo vinavyotoa huduma za afya.

Kwa hiyo, hatuna budi wananchi kupeleka malalamiko yao kwa Kamati hizi za afya za vituo vinavyohusika ili hatua za kinidhamu zichukuliwe pale ambapo watendaji wanakiuka utaratibu huu. Naomba nirudie kusema kwamba Sera ya Misamaha ni Sera ya Serikali na ni lazima iheshimiwe na hivyo tunawaomba Waheshimiwa Wabunge tushirikiane ili kuhakikisha kwamba makundi yanayostahili msamaha wanapata msamaha kama inavyotakiwa. (*Makofî*)

**MHE. JOEL N. BENDERA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa, wananchi wengi kama Sera ya Afya inavyosema wanachangia afya katika Zahanati, Vituo vya Afya na Hospitali za Wilaya. Lakini uko utata kwamba wanapotaka kutumia zile fedha wanazochangia ili kununua dawa au hata sabuni katika Zahanati kunakuwa na urasimu mpaka upitie Wilayani au Mkoani.

Je, Serikali inaweza kueleza ni utaratibu gani ambao unatakiwa ufuatwe ili kuondoa kero ambayo wanaipata Zahanati zetu vijijiini katika kutumia hela ambazo wanachangia wenyewe ili waweze kununua madawa ya kuwasaidia? (*Makofî*)

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibuswali la nyongeza la Mheshimiwa Bendera kama ifuatavyo:-

Nadhani Mheshimiwa Mbunge anakusudia fedha zinazochangwa katika mfuko wa afya ya jamii. Kama ndivyo ni kwamba fedha zinazoingia katika Mfuko wa Afya ya Jamii zina madhumuni ya kutoa huduma za afya kwa maana ya kuonwa na daktari kupata dawa na endapo kunahitajika upasuaji basi kufanyika kazi kama hizo. Bila shaka utaratibu unataka kwamba mgonjwa, akishalipa fedha yake, basi anapopata matatizo ya kuumwa aende kwenye kituo kilicho karibu yake ili haweye kupata matibabu. Na ndio maana ninarudia kusema kwamba kuna Kamati za Afya katika maeneo hayo endapo kuna utata wowote mgonjwa kunyimwa matibabu au dawa basi anatakiwa apeleke malalamiko yake katika Kamati husika.

Mheshimiwa Spika, isipokuwa tu kwamba fedha hizi haziruhusiwi tena kununua sabuni na vitu kama hivyo. Fedha hizi ni kwa ajili ya matibabu na mgonjwa inabidi ajitegemee pale ambapo vitu zaidi ya matibabu vinahitajika.

Na. 69

#### **Tatizo la Mimba kwa Watoto wa Shule za Msingi Nchini**

**MHE. PROF. DAVID H. MWAKYUSA (K.n.y. MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali pamoja na vyombo vingine imeonekana kwa makini sana katika kushughulikia tatizo la ubakaji na kwamba marekebisho ya Sheria Na. 4 ya makosa ya Kujamiiiana *Sexual offences Special Provisions Act* ya mwaka 1998 yameelekea kuwa na matokeo mazuri.

- (a) Je, ni watoto wangapi wa shule za msingi wamekatishwa masomo yao kwa sababu ya mimba?
- (b) Je, ni Walimu na watu wengine wangapi wamefunguliwa mashitaka ya kuwabaka na kuwapa mimba wanafunzi wa shule za msingi?
- (c) Je, wazazi na watoto wa shule ambao wamebakwa na kupewa mimba na wao kunyamaza tu kwa nini wasifunguliwe mashitaka kwa kosa la kuficha uovu?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO (K.n.y. WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa William Shellukindo, Mbunge wa Bumbuli, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Spika, watoto wa shule za Msingi waliokatisha masomo kwa sababu ya mimba kuanzia mwaka 2001 - 2004 ni kama ifuatavyo:-
- (b)

<b>MWAKA</b>	<b>WASICHANA WALIOANDIKISHWA SHULE</b>	<b>WALIOKATISHWA MASOMO KWA MIMBA</b>	<b>ASILIMIA</b>
2001	2,407,244	2,666	0.10%
2002	2,929,320	2,380	0.08%
2003	3,197,352	2,227	0.07%
2004	3,456,822	2,550	0.07%

Tatizo la Mimba katika shule za Msingi litaendelea kupungua zaidi tutakapofikia lengo la rika lengwa la Elimu ya Msingi la miaka 7 - 13 kuwa shuleni asilimia 100. Mwaka jana walikuwepo shuleni asilimia 90.5 na mwaka huu inatarajiwa watavuka lengo la asilimia 95.

(b) Mheshimiwa Spika, tangu mwaka 1995 - 2004 kulikuwepo na mashauri 330 yanayohusu masuala ya mapenzi kati ya Walimu na wanafunzi. Walimu 42 walibainika kuwabaka wanafunzi na Walimu 79 kuwapa mimba wanafunzi. Walimu hao 330 ndio waliotuhumiwa kutenda kosa. Kuwa kuzingatia maadili ya kazi ya ualimu Wizara yangu kuititia kwa iliyokuwa Tume ya Utumishi wa Walimu iliachukulia hatua kali za kuwafukuza kazi na Utumishi Walimu hao. Hata hivyo Wizara yangu haina takwimu kuhusu idadi ya Walimu na watu wengine waliofikishwa mahakamnai na kufungwa, kulipa faini na ua fidia kwa sababu hatua za kushughulikia makosa ya jinai haziko chini ya Wizara yangu.

(c) Mheshimiwa Spika, baada kuona tatizo hili linaendelea kujitokeza katika shule zetu za Msingi na Sekondari, hivi karibuni imetungwa Kanuni Mpya iitwayo: "*The Education (imposition of penalties to persons who marry or impregnate a school girl) Rules 2003*" inayotoa adhabu kwa anayempa mimba, kuo, kuoza na kukatiza masomo Mtoto wa shule. Aidha Wizara yangu imeshatoa maelekezo kwa Maafisa Elimu wa Mikoa na Wilaya kwa njia ya Waraka wa Elimu Na. 6 wa mwaka 2004 kuchukua hatua za kisheria kwa yejote anayempa mimba, kuo na kuoza mwanafunzi na taarifa za matukio hayo ziwasilishwe Wizarani. Kwa hiyo, wazazi wa watoto wa shule ambao wamebakwa, kupewa mimba na wao kunyamaza kimya kwa mujibu wa Kanuni hii nao pia watachukuliwa hatua.

**MHE. PROF. DAVID H. MWAKYUSA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwanza namshukuru Naibu Waziri.

(1) Wakati Naibu Waziri anajibu swali Na. (b) ametuambia kwamba Wizara yake haina takwimu za Walimu na watu waliopelekwa Mahakamani kwa sababu hii ni shughuli ya Wizara nyingine. Wabunge tunapoulima maswali tunauliza Serikali nilitaka kujua Wizara yake ilipata shida gani kuuliza Wizara inayohusika ili sisi itupe majibu? (*Makofî*)

(2) Kwamba mimba inayozungumziwa katika swali la msingi ni ishara kwamba ngono iliyotendeka siyo salama. Na kwa maana hiyo, kuna uwezekano mkubwa kwamba hawa watoto wetu waliopata mimba wanaweza kuwa wameambukizwa Ukimwi

Je, Serikali ina utaratibu wowote kwamba iwasake hawa watoto iwape ushauri nasaha na kuwapima kama wameambukizwe ili kama watagundulika wapewe kipaumbele katika kupewa madawa ya kupunguza makali? Ahsante. (*Makofî*)

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO (k.n.y. WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Professa Mwakyusa, kama ifuatavyo:-

(1) Ni kweli Serikali ni moja lakini ukweli vile vile usiokatalika kwamba katika Serikali ya umoja ili utendaji uende vizuri, basi kuna mgawanyiko wa Wizara ili kila Wilaya ishughulike na jambo lake.

Kwa hiyo, kwa vile Proffessa alikuwa anahitaji kufahamu waliopelekwa Mahakamani tutalifikisha suala hili kwa Wizara ya Sheria na Katiba pamoja na Wizara ya Mambo ya Ndani ili kwa pamoja waweze kupata hiyo idadi ya waliofikishwa Mahakamani.

(2) Kuhusu Ukimwi. Watoto hawa pengine wameathirika kwa sababu kama kuna mimba ina maana ngono iliyotumika ilikuwa siyo salama. Uwezekano huo upo kabisa kwamba kama mtu amefikia hata kumzalisha mwanafunzi maana yake hapakuwa na vizuizi vya kujikinga/kumkinga yule mtoto kuambukizwa na Ukimwi. Sasa hili suala la watoto hawa wasakwe ili wapewe ushauri nasaha ni jukumu kwa kweli la kila mzazi kwa mtoto wake. Na mimi ningependa kutoa wito hapa, kwamba haya tunayozungumza hapa ni matokeo tu. Lakini la msingi kabisa ni tabia ya watu pamoja na sisi baadhi ya wazazi tunaoficha mambo haya maana tupo kutokuwaelimisha watoto juu ya hasara ya jambo hili.

Mheshimiwa Spika, inasitikitisha sana kuona kwamba mafahari ya ng'ombe na mabeberu ya mbuzi yanaleshimu Ndama. Majogoo ya kuku yanaleshimu Vifaranga. Lakini baadhi ya wanaume tunazidiwa akili hata na hawa wanyama. Kwa hiyo, la msingi hapa ni elimu zaidi ili kuzuia matukio haya. (*Kicheko*)

### **Tatizo la Upungufu wa Walimu Nchini**

**MHE. JEREMIAH J. MULYAMBATE** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali ya awamu ya tatu imetilia mkazo sana sula la Uboreshaji wa Elimu ya Msingi, Sekondari na Elimu ya Juu, lakini bado kuna upungufu nchini.

- (a) Je, Serikali ina matarajio ya muda gani itakuwa imefuta tatizo la upungufu wa walimu nchini?
- (b) Je, sasa elimu ya wastani kwa Watanzania ni ya kiwango gani?
- (c) Je, kwa mara ya mwisho Serikali ilifanya lini tathmini ili kuona kama elimu yetu Kitaifa au inashuka na kwa asilimia ngapi?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO  
(K.n.y. WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Jeremiah Mulyambate, Mbunge wa Miatu, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Spika, Serikali kuititia MMEM 2002 - 2006 na MMES 2004 - 2009 inaendelea kuandaa na kuajiri walimu wapya wanaohitimu mafunzo kutoka vyuo vya Ualimu ngazi ya Cheti, Stashahada, kwa lengo la kukabiliana na tatizo la upungufu wa walimu katika shule za msingi, Sekondari na Vyuo vya Ualimu. Inatarajiwa kuwa mwishoni mwa MMEM 2006 na MMES 2009 tatizo hili litakuwa limemalizika.
- (b) Mheshimiwa Spika, katika utafiti wa hivi karibuni Watanzania 57.9% wana angalau Elimu ya Msingi na 10% elimu ya Sekondari. Katika utekelezaji wa MMEM tumefikia Elimu ya Msingi 90.5% ya rika lengwa na mwaka huu tunategemea kufikia zaidi ya 95% ya rika hilo. Katika MMES lengo ni kufikia Elimu ya Sekondari 50% ya rika lengwa ifikapo mwaka 2009 kutoka 13% ya hivi sasa.
- (c) Mheshimiwa Spika, tathmini ya mwisho ilifanywa wakati wa kutayarisha mipango ya Maendeleo ya Elimu ya Msingi MMEM 2002 - 2006 na Sekondari MMES 2004 - 2009 ambayo inalenga kurekebisha mapungufu yaliyojitekeza katika utafiti uliofanywa wakati wa kuandaa program ya Maendeleo ya Sekta ya Elimu yaani *Education Sector Development (ESDP)* mwaka 1996. Tangu kuanza utekelezaji wa MMEM ubora wa Elimu kwa kipimo cha ufaulu mtihani wa D.VII umeongezeka kutoka 22% mwaka 2001 hadi 49% mwaka 2004. Aidha kutohana na hatua mbalimbali ufaulu wa madaraja ya kwanza mpaka ya tatu umeongezeka toka asilimia 25 mwaka 2001 hadi asilimia 38 mwaka 2004 kwa watahiniwa katika shule za Sekondari. Hata hivyo ubora

wa kufaulu Mitihani pekee yake siyo kipimo kamilifu cha ubora wa Elimu ndiyo maana katika Mipango hiyo hatua inachukuliwa kuboresha mitaala ili elimu yetu ielekee lengo lililo katika Dira ya Maendeleo ya mwaka 2025.

**MHE. JEREMIAH J. MULYAMBATE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa, suala la uboreshaji wa elimu unaendana pamoja na kuwa na Walimu wa kutosha hasa kama inavyotakiwa. Na kwa bahati sasa hivi tuna upungufu mkubwa sana wa Walimu katika elimu ya Msingi pamoja na Sekondari. Na kwa kuwa, suala hili bado hata wale ambao wamo sasa hivi wanafundisha Eimu ya Msingi na Sekondari katika mitaala hii mipya hawapati semina wala mafunzo yoyote yale. Kwa hiyo ina maana kwamba wanafundisha katika mitaala ile ya zamani.

Je, suala hili la kufundisha upya mitaala hii mipya ambayo imetokea hivi karibuni ni lini utanza ili kuwa na elimu inayoendana na mitaala hii mipya? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO (k.n.y. WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mulyambate, kama ifuatavyo:-

Nakubaliana na yeche na wanafunzi wa walimu tunao uhaba wa Walimu. Lakini uhaba huu unashughulikiwa ipasavyo. Kwa sababu katika miaka mitano ya Mpango huu wa MMEM, ilipangwa kwa ajili ya Walimu 45,849 ili uwiano wa moja kwa mwalimu moja kwa wanafunzi 45 ufikiwe ifikapo mwaka 2006. Na hadi mwaka 2004, tumeajiri walimu 34, 113 kati ya nafasi ambazo zilitengwa na Idara Kuu ya Utumishi 36,284. Nafasi 6,171 bado hazijajazwa. Lakini kwa mwaka huu wa 2005 tunatarajia kuajiri walimu wengine 7,286. Hata hivyo kutokana na ukweli kwamba kuna ongezeko kubwa la wanafunzi wa darasa la kwanza kutokana na wananchi kuitikia mwito wa MMEM.

Walimu wengine kutoku-report katika vituo vinavyopangwa kutokana na sababu zao wenyewe. Na hata kufa na kustaa fu bado tunajikuta mahitaji halisi sasa ya Walimu yamefikia 167,816 na wakati waliopo mashule ni 134,314. Kwa hiyo, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge lakini jitihada zinafanywa ili kuhakikisha kwamba suala hili linafikia mwisho wake.

Suala la Mitaala Mipy, kweli kilichotokea kutokana na Sera ya elimu ambayo tulipitisha hapa Bungeni mwaka 1995. Kilichofanywa ni kuondoa michepoo ambayo ilikuwa inamfanya mwanafunzi anamaliza na mchepoo wake wa kilimo lakini haifanani na nadharia yenyewe. Ukimchukua mtu wa mchepoo wa kilimo, akienda Chuo Kikuu mwenzake wa PCM anafanya vizuri zaidi kwa sababu alishakuwa na msingi mzuri wa kinadharia. Kwa hiyo, siyo tumeweka mitaala mipya lakini tumeondosha ile ambayo tunafikiria ilikuwa inampa mzigo mwanafunzi. Hata hivyo kila itakapotokea hoja ya Walimu kupewa semina jambo litafanywa mara moja. (*Kicheko/Makofi*)

**WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO (k.n.y. WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI):** Mheshimiwa Spika, napenda kuongezea

majibu mazuri ambayo ametoa Mheshimiwa Naibu Waziri, ni kwamba ni kweli mitaala mipyä imekamilika. Lakini maandalizi ya mitaala ile kuanza kutumika hivi sasa ndio inafanyika Vyoni. Wanaandaliwa Walimu kwanza ili kuhakikisha kwamba mitaala hii itakapoanza utekelezaji wake, unakwenda vizuri. Na ile michepuo ambayo imeondolewa katika mashule siyo kwamba imeondolewa tu kwa ghafla! Hapana. Tunatumia lile neno *facing out* kwa hiyo ile ambayo bado wanaendelea kumalizia masomo yao *form three, four* wanaendelea kumalizia ili kuanza kwa utaratibu mipyä. Ahsante.

Na. 71

### **Barabara na Reli Nchini**

**MHE. STEPHEN M. KAZI** aliuliza:-

Kwa kuwa Reli na Barabara ni njia za uchukuzi zenyé umuhimu sana na zina mchango mkubwa katika maendeleo ya jamii na kwa kuwa kwa wakazi wa mikoa ya Kanda za Ziwa na Kigoma reli ya kati ndiyo chombo muhimu cha uchukuzi hasa ikizingatiwa kuwa reli ikiwa katika hali nzuri inastahili usafirishaji wa mizigo zaidi ya barabara.

- (a) Je, Serikali ilitumia utaratibu gani kutofautisha Reli na Barabara na kuiweka barabara chini ya Wizara ya Ujenzi ambayo sasa imepangwa kuwa moja kati ya Wizara muhimu *priority* na kuiacha reli chini ya Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi wakati vyote vinahusiana na uchukuzi?
- (b) Kwa ni ni Serikali haifanyi matengenezo ya kutosha Reli ya Kati kwa kiwango cha kuiwezesha kutoa huduma ya usafiri wa treni kila siku kati ya Dar es Salaam hadi Mwanza na Kigoma kwenda na kurudi?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI (K.n.y. WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI):** Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Stephen Kazi, Mbunge wa Mwanza Mjini, napenda kutoa maelezo mafupi yafuatayo:-

Nakubaliana na Mheshimiwa Stephen Masaba Kazi kuwa reli ni njia ya uchukuzi yenye umuhimu sana na inatoa mchango mkubwa katika maendeleo ya jamii na kwa wakazi wa Kanda ya Ziwa na Kigoma ndicho chombo muhimu cha uchukuzi hasa kikiwa katika hali nzuri. Pia Wizara inaamini kuwa uimara na umadhubuti wa reli ungesaidia sana kuziweka na kuzidumisha barabara zetu. Kwa vile tegemeo ni kuwa reli inapaswa kubeba shehena nzito kuliko barabara ni matengenezo yake si ya mara kwa mara kama barabara. Baada ya maelezo hayo mafupi sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Stephen Masaba Kazi, kama ifuatavyo:-

- (a) Kabla ya mwaka 1995 sekta ya Mawasiliano na Uchukuzi na ile ya Ujenzi zilikuwa chini ya Wizara moja iliyojulikana kama Wizara ya Ujenzi na Mawasiliano. Baada ya Serikali ya Awamu ya Tatu kuingia madarakani mwaka 1995, Wizara hiyo

ilitenganishwa na kuwa Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi na Wizara ya Ujenzi. Kimsingi kutenganishwa kwa Wizara hizi mbili kulitokana na wingi wa majukumu ya iliyokuwa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kwa wakati ule.

Kutokana na majukumu hayo iliamuliwa ujenzi na utunzaji wa barabara ubaki chini ya Wizara ya ujenzi na utoaji wa huduma barabarani ikiwa ni pamoja na uendeshaji wa miundombinu mingine ya uchukuzi ihamie Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi. Huu ulikuwa ni uamuza wa kawaida uliofanywa na Rais kukidhi matakwa ya wakati huo.

Mheshimiwa Spika, suala la sekta fulani kupewa umuhimu kuliko nyingine halina maana kwamba sekta zilizoachwa hazina mchango wowote. Hii inatokana na maamuza ya ki-sera pamoja na kuzingatia ufinyu wa Bajeti.

Kilichotokea ni kwamba barabara kwa kipindi hicho zilitakiwa zijengwe kwa wingi katika maeneo mengi ya nchi ili kuwaondolea wananchi kero zinazotokana na ukosefu wa barabara. Hivyo katika awamu ya kwanza ya Mkakati wa Kuondoa Umaskini (MKU) nchini ulioanza mwaka 2000/2001, miundombinu ya barabara ilipewa kipaumbele zaidi kuliko mingine.

Hata hivyo dhana ya kubagua sekta zingine na kutoa upendeleo katika sekta fulani ilionyesha mapungufu. Kwa kuona mapungufu yaliyojitekeza katika Mkakati wa Kupunguza Umaskini ule wa kwanza kwa kifupi MKU, hivi sasa Serikali imeanzisha Mkakati mwingine wa pili unaoitwa Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kuondoa Umaskini kwa kifupi MKUKUTA.

Tofauti na Mkakati wa Awali yaani MKUKUTA ni mpana zaidi ya ule wa awali MKU na unalenga kukuza uchumi na kupunguza umaskini na utekelezaji wake unaohusisha sekta zote za Serikali, sekta binafsi na unashirikisha wananchi wote katika ngazi mbalimbali.

Hii ina maana katika mfumo wa MKUKUTA sekta zote sasa zinapewa kipaumbele bila ya ubaguzi wa sekta nyingine. Tunategemea kuwa sekta ya reli nayo hivi sasa itapewa umuhimu kama barabara pale hali ya kifedha itakaporuhusu.

(b) Mheshimiwa Spika, nia ya Wizara mawasiliano na Uchukuzi kwa kupitia Shirika lake la Reli Tanzania ni kuiweka reli hii katika hali nzuri kila inapowezekana na kukarabati injini na mabehewa na pia njia yenye. Bahati mbaya kazi hii huwa haifiki lengo linalokusudiwa kutokana na ufinyu wa Bajeti. Hata hivyo, kwa kushirikiana na wahisani mbalimbali Shirika la Reli Tanzania limeendelea kuboresha huduma zake. Kwa mfano, mwaka wa fedha wa 2005/2006 linatarajia kubadilisha mataruma ya reli yenye umbali wa kilometra 197 kwa msaada wa fedha wa Benki ya Dunia. Maeneo yatakayoguswa ni kati ya Kintinku/Makutopora, Itigi/Malongwe, Igalula/Tabora na Tabora/Mabana.

Pia upo mpango wa kubadilisha mataruma umbali wa kilometra 30 kati ya Mbamba na Kilosa, kituo cha kupakilia ng'ombe katika Stesheni ya Seke na Puma. Vile

vile upo mpango wa kufunga pampu za maji na umeme katika kituo cha Kilosa. Shirika la Reli Tanzania linalo uwezo wa kufanya mengi ila tu kama ikiwezeshwa kupata Bajeti ya kutosha.

**MHE. STEPHEN M. KAZI:** Mheshimiwa Spika, nilikuwa na mawili.

**SPIKA:** Ni vema na ni haki yako kuuliza maswali mawili endelea.

**MHE. STEPHEN M. KAZI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwa kuwa, utaratibu mpaka sasa hivi ulivyo ni kwamba mizigo inayokwenda Mwanza, Kigoma, Mara inapakiliwa Dodoma baada ya kuletwa kwa magari kutoka Dar es Salaam. Na hali hii inafanya gharama za *handling* kuwa mbili. Kwa sababu unapopakia malori kule mnakuja mnapakua hapa kupakia kwenye treni tena. Na kwa kuwa, tofauti ya sehemu hizi mbili kwa kutumia reli na barabara pia gharama zake ni tofauti. Na hii imeleta gharama za bidhaa Mwanza kupanda. (*Makofi*)

Je, sasa katika hali hii Serikali inasemaje wakati ikiandaa hili ili kwamba iweke ruzuku ili kutoa tofauti ya gharama hizi ambazo zinaongeza bidhaa za walaji Mwanza kupanda? (*Makofi*)

Je, ni lini sasa kwa uhakika Serikali itasema kwamba itairekebisha reli kwa kiwango cha kutosha na kwamba itanunua mabehewa ya abiria na mizigo ya kutosha? Ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI (k.n.y. WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali ya nyongeza mawili ya Mheshimiwa Kazi Mbunge wa Mwanza Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kama Mheshimiwa Mbunge alivyosema kwamba mizigo inaletwa hapa Dodoma halafu baadaye ndio inapakiwa kwenda Mwanza. Tatizo hili linatokana na matatizo ya reli yenyewe. Hii ni reli iliyojengwa karibu miaka mia iliyokwisha ni reli ambayo ni chakavu.

Kwa hiyo, kadri ambavyo tutaweza kuikarabati hii reli ikaweza kuhimili uzito wa uchumi wa sasa hivi, ndipo tutaweza kutatua tatizo hili. Lakini kama reli yenyewe iko katika hali jinsi ilivyo Mheshimiwa Mbunge vile vile kuna matatizo ya injini kama walivyosema ndio yanayosababisha haya matatizo.

Lakini kama nilivyojibu katika jibu la msingi kwamba Shirika la Reli linajitahidi sasa kuifanya marekebisho hii reli ambayo tumesema ni chakavu na nimetaja kwamba kwa mwaka ujao karibu kilomita 200 zitafanyiwa ukarabati hili likamilika.

Mpango huu ukikamilika ambao umeshaanza ndio utakaotatua tatizo ambalo Mheshimiwa Mbunge amesema na amesema sasa lini siwezi kutaja tarehe. Lakini nilivyojesta kwamba sasa katika Mkakati huu wa Awamu ya Pili MKUKUTA. Sasa

sekta zote zinapewa umuhimu na Sekta ya reli nayo itapewa umuhimu hii itaharakisha sasa kurekebisha reli yetu ili iweze kufanya kazi sawasawa kulingana na matarajio ya Watanzania.

Na. 72

### **Simu ya Kisasa Wilayani Chunya.**

**MHE. PAUL E. NTWINA** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imewapatia wananchi wa Wilaya ya Chunya simu za mtambo kwa kisasa (*automatic*) na kwa kuwa mji mdogo wa Mkwajuni na vijiji vya Makongolosi, Lupa, Kanga na Galula havina mawasiliano hayo.

- (a) Je, ni lini Serikali itavipatia vijiji hivyo simu za kawaida?
- (b) Je, Mashirika Binafsi kama vile *Celtel, Vodacom, Zantel, Mobitel* watafikisha lini huduma zao vijijini?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI (k.n.y. WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalil la Mheshimiwa Paul E. Ntwina, Mbunge wa Songwe, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa sasa haijihusishi moja kwa moja na utoaji wa simu kwa vijiji au miji kutokana na ukweli kwamba huduma hizi zimeachiwa sekta binafsi. Badala yake Serikali imekuwa ikijenga mazingira mazuri ya kuwezesha huduma kama hizi kutolewa na sekta binafsi moja au kwa kushirikiana na Serikali.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako tukufu kwamba kampuni ya simu za mkononi ya *Celtel* tayari imeshafikisha mawasiliano ya simu Wilayani Chunya kwa maana Makao Makuu ya Wilaya, pamoja na mji mdogo wa Mkwajuni. Pia huduma hizo zimefika hadi kijiji cha Makongolosi. Kampuni hiyo inaendelea kuboresha mawasiliano katika kijiji cha Loppa, maeneo mengine aliyotaja Mheshimiwa Mbunge yako kwenye mpango wa kampuni hiyo. Aidha, kampuni za simu za *vodacom* na *Mobitel* baada ya kufikisha huduma hizo makao makuu ya wilaya zina mipango wa kufikisha huduma hizo kwenye vijiji na maeneo ambayo Mheshimiwa Mbunge ameyataja na ningependa kwa kweli kwa dhati kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa ushirikiano mkubwa ambao ametoa kwa Wizara yetu, mpaka tumeweza kufikisha huduma katika maeneo haya aliyoyataja.

**MHE. PAUL E. NTWINA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru niulize swali dogo la nyongeza. Pamoja na kupeleka simu wilayani bado minara inaonekana haina nguvu. Je, Serikali inaweza ikasimamia minara ikaboreshwa zaidi ili isikie sehemu kubwa zaidi katika maeneo hayo?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI (k.n.y. WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI):** Mheshimiwa spika, madamu sasa minara imeshafika katika maeneo ya Mheshimiwa Mbunge, sasa suala tu ya kuirekebisha na kuongeza iwe na nguvu zaidi nafikiri ni suala ambalo litafanyiwa kazi haraka iwezekanavyo ili dhamira ya kuwapatia huduma ya simu, katika maeneo ambayo ametaja Mbunge iweze ikamilika. Kwa hiyo hilo litarekebishwa.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa kanuni muda wa maswali umekwisha. Sasa kuna matangazo ya vikao vya leo vya Kamati ambavyo vimepangwa na wenyeviti husika Kamati nne zimepangiwa vikao.

Kamati ya kwanza ni Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge, Mheshimiwa Eliachim Simpasa, Mwenyekiti anaomba wajumbe wa Kamati hiyo wakutane leo tarehe 19 Aprili, 2005 saa 5:00 Asubuhi, chumba Na. 428 ghorofa ya nne, Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge.

Kamati ya pili ni Kamati ya Mambo ya Nchi za Nje, Mheshimiwa Dr. William Shinja, Mwenyekiti anaomba wajumbe wa Kamati hiyo wakutane leo tarehe 19 Aprili, 2005 saa 5:00 Asubuhi, chumba Na. 227 ghorofa ya pili, Mambo ya Nje.

Kamati ya tatu ni Hesabu za Serikali za Mitaa (*LAAC*) Mwenyekiti wake Mheshimiwa Mgana Msindai, anaomba wajumbe wa *LAAC*, wa Kamati ya *LAAC* wakutane saa 5:00 Asubuhi hiyo hiyo kwenye chumba Na. 231 ghorofa ya pili.

Kamati ya nne na ya mwisho ni Kamati ya Miundo Mbinu. Mheshimiwa Prof. Mgombelo, Mwenyekiti anaomba wajumbe wa Kamati hiyo wakutane mara baada ya kipindi cha maswali yaani saa 4:30 asubuhi hii katika Ukumbi namba 219 ghorofa ya pili. Mwisho wa matangazo ya vikao sina tangazo zaidi, tunaendelea na *Order Paper*.

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

**Muswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria ya Shirika la Ukaruzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika wa Mwaka 2005 (*The Co-Operative Audit and Supervision (Amendment) Bill, 2005*).**

(*Kusomwa Mara ya Pili*)

**WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba nitoe shukrani zangu za dhati kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha Muswada huu hapa Bungeni. Aidha kama wenzangu waliotangulia naomba nichukue nafasi hii kutoa salamu zangu za rambi rambi kwa familia za marehemu Waheshimiwa Wabunge na kwako Mheshimiwa Spika kwa kuwapoteza Mheshimiwa Ahmed Hassan Diria, aliyekuwa Mbunge wa Rahaleo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Katiba na Utawala Bora wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, na Mheshimiwa Balozi Paul Bomani ambaye

alikuwa Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Mmoja wa Waasisi Mashauri, wa Ushirika Taanzani. Mungu aziweke roho za marehemu mahali pema peponi. Ameni

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Kurekebisha Sheria ya Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika yaani *The Co-operative Audit and Supervision Act No. 15* ya mwaka 1982 uitwao *The Co-operative Audit Supervision Amendment Act 2005* pamoja na marekebisho yake ambayo Waheshimiwa Wabunge wamegawiwa sasa usomwe kwa mara ya pili.

Mheshimiwa Spika, napenda nianze hotuba yangu kwa kutoa shukrani zangu za dhati kwa wale wote waliouwezesha Muswada huu wa kurekebisha Sheria ya Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika ujulikanao kama *The Co-operative Audit Supervision Amendment Act 2005*, kukamilika na kuwasilishwa mbele ya Bunge lako tukufu. Napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Uwekezaji na Biashara, Mheshimiwa William Shellukindo Mbunge wa Bumbuli na Waheshimiwa Wabunge wa Kamati, kwa uchambuzi wa kina wa Muswada huu na mapendekezo yao, ambayo yote yamezingatiwa katika kuboresha Muswada huu. Aidha napenda pia kuwashukuru wadau wote ambao walishiriki kikamilifu katika kujadili na kutoa maoni na mapendekezo juu ya vipengele vyote vya Muswada, ambavyo nayo yamezingatiwa.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge watakumbuka kwamba, mwaka 2002 Serikali ilipitisha sera mpya ya maendeleo ya Ushirika ambayo lengo lake kuu ni kutoa muongozo kwa ajili ya kuviwezesha Vyama vya Ushirika kuwa vyombo imara vya kiuchumi, vinavyojitegemea na vyenye kufanya kazi kwa ufanisi katika mfumo wa uchumi wa soko huru. Aidha ili kutekeleza sera hiyo Sheria ya Vyama vya Ushirika ya mwaka 2003 ilitungwa. Kutokana na mabadiliko hayo Sheria ilioanzisha Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika *COASCO*, ilipaswa nayo ifanyiwe marekebisho ili kuwezesha shirika kushiriki ipasavyo katika kutekeleza sera na sheria mpya ya Vyama vya Ushirika. Aidha kuanzia katikati ya miaka ya 90 yametokea mabadiliko katika sera za uchumi za taifa, ambayo hayana budi kuzingatiwa na Sheria ya *COASCO* ili kuwezesha utekelezaji wa majukumu yake ueandane na mahitaji ya wakati wa sasa.

Hivyo madhumuni makuu ya Muswada huu ni kufanya marekebisho katika baadhi ya vifungu vya Sheria, ilioanzisha Shirika la *COASCO* ili kukidhi mahitaji ya wakati uliopo na kuliwezesha shirika hilo kushiriki kikamilifu katika utekelezaji wa sera na Sheria mpya ya ushirika, hususan katika kufufua, kuimarisha na kuendeleza ushirika nchini, chini ya mfumo wa uchumi wa soko huru.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika *COASCO* lilianzishwa na Sheria Na. 15 ya mwaka 1982. Sheria hiyo iliahinisha majukumu ya *COASCO* ambayo ni kukagua na kusimamia hesabu za mwisho wa mwaka za vyama vya ushirika. Kutokana na marekebisho katika sera za uchumi ambayo imesababisha kuwa na sera na Sheria hii mpya ya maendeleo ya Ushirika majukumu hayo yamebainika kutokidhi mahitaji ya ushirika, chini ya mfumo wa uchumi uliopo.

Mheshimiwa Spika, Muswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria iliyoanzisha Shirika la *COASCO*, ukijadiliwa na kuitishwa na Bunge unatarajiwa kuwa na matokeo yafuatayo.

Kwanza kuondolea Shirika la *COASCO* ukiritimba wa kuwa mkaguzi pekee wa Vyama vya Ushirika. Kwani Sheria ya Vyama vya Ushirika ya mwaka 2003, kifungu cha 48 (3) inaruhusu Chama cha Ushirika kuteua mkaguzi mwingine yeoyote anayefaa kwa hidhini ya mrajisi wa vyama vya ushirika.

Pili kutenganisha majukumu ya utoaji huduma za ukaguzi na ushauri na kulipa uwezo shirika kufanya utafiti katika masuala ya husio Vyama vya Ushirika na kutoa ushauri kwa vyama hivyo na kwa Serikali, kifungu cha (4) kifungu kidogo cha (1) (d).

Tatu shirika la *COASCO* kuruhusiwa kutoa huduma za ukaguzi nje ya vyama vya ushirika ikiwa ni pamoja na vikundu vya mwelekeo wa ushirika yaani *Pre-Cooperative Groups* ambavyo vinatambuliwa na Sheria mpya ya ushirika ya mwaka 2003, kifungu cha (4) kifungu kidogo cha (1) (a).

Nne kurekebisha viwango vya adhabu na faini vinavyotozwa, kutokana na ukiukwaji wa Sheria ili vilingane na uzito wa kosa na thamani ya fedha ya wakati huu, vifungu cha (6) kifungu kidogo cha(4), kifungu cha (8)(3) na kifungu cha (11) na kifungu cha (15).

Tano kurekebisha muundo wa shirika ikiwa ni pamoja na uteuzi wa wajumbe wa bodi ya wakurugenzi. Ili uoane na majukumu ya shirika, Ibara ya (1) ya jendwali la kwanza.

Sita kubainisha majukumu ya shirika kutekeleza kanuni za maadili ya uongozi bora kwa vyama vya ushirika kama ambavyo yameainishwa katika Sheria ya Vyama vya Ushirika ya mwaka 2003, kifungu na (4) (8).

Mheshimiwa Spika, Muswada wa Sheria ya kurekibisha Sheria iliyoanzisha Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa vyama vya ushirika yaani *COASCO*, umegawanyika katika sehemu kuu mbili.

Sehemu ya kwanza inahusu masuala ya awali hususani inasisitiza kwamba Muswada unapaswa usomeke pamoja na Sheria iliyoanzisha Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika Na. 15 ya mwaka 1982.

Sehemu ya pili ya Muswada inapendekeza marekebisho yatakayofanywa katika sheria inayoanzisha Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika ya mwaka 1982 ambayo ni pamoja na yafuatayo.

Kwanza kuweka kifungu cha (4) kimpya kinachoainisha majukumu ya shirika. Kifungu hicho kinalenga katika kuanzisha na kutenganisha majukumu ya shirika na ya

ofisi ya mrajisi wa Vyama vya Ushirika. Aidha *COASCO* imepewa majukumu mapya ya kufanya utafiti katika masuala ya husuyo Vyama vya Ushirika na kutoa ushauri kwa vyama hivyo na kwa Serikali, na kuhakikisha Vyama vya Ushirika vinatekeleza kanuni za maadili ya viongozi wa vyama vya ushirika, kama yalivyofafanuliwa na Sheria mpya ya ushirika ya mwaka 2003 katika kifungu cha (125).

Pili vifungu mbalimbali vimelekebishwa ili kuviwezesha Vyama vya Ushirika kuwa huru katika kuteua wakaguzi wake wa mahesabu na kuwezesha *COASCO* kukagua Asasi nyingine zenyne mwelekeo wa ushirika ikiwa ni pamoja na *Pre-Co-operative Groups* kifungu cha (4) kifungu kidogo cha (1) na kifungu cha (6) kifungu kidogo cha (1).

Tatu vifungu vya sita kifungu kidogo cha (4), kifungu cha (8) kifungu kidogo (3), kifungu cha (11) na (15) vinahusu faini na adhabu kwa makosa mbalimbali. Pia vimerekebishwa ili kuianisha vifungu vya adhabu na faini na uzito wa makosa. Nne jendwali namba *one* limerekebishwa. Ili kuweka uteuzi wa wajumbe wa bodi ya shirika kuzingatia majukumu muhimu ya bodi na kuwa na uwakilishi unao wiana na majukumu ya shirika, unaozingatia utawala bora na uwiano mzuri wa kijinsia.

Mheshimiwa Spika, mwisho naomba kusisitiza kwamba marekebisho yaliyopendekezwa na Muswada huu, ni muhimu kwa umma na watendaji wa shirika, hususani katika kutekeleza azma ya Serikali ya kufufua, kuendeleza na kuimarisha ushirika nchini. Aidha kupanua uwigo wa kazi za shirika, kwa kuzingatia mfumo wa uchumi wa soko huru.

Baada ya maeleza hayo sasa naliomba Bunge lako tukufu lijadili Muswada wa Marekebisho ya Sheria iliyoanzisha Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika yaani *The Co-operative Audit Supervision Amendment Act, 2005* na kuitishwa kuwa Sheria.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

**MHE. ISMAIL J. R. IWVATTA (k.n.y. MWENYEKITI WA UWEKEZAJI WA BIASHARA):** Mheshimiwa Spika, maoni na mapendekezo ya Kamati ya Uwekezaji na Biashara kuhusu wa Muswada wa *Co-operative Audit and Supervision Cooperation Amendment Act 2005*.

Mheshimiwa Spika, Utangulizi naomba kutoa maoni kwa niaba ya Kamati ya Uwekezaji na Biashara kwa mujibu wa kanuni ya 70 kifungu kidogo cha (2) toleo la mwaka 2004. Uchambuzi wa Muswada; kabla ya kuanza kujadili Muswada huu Kamati iliwaalika wadau mbalimbali kuja kutoa maoni yao.

Mheshimiwa Spika, Mkutano na wadau; wadau waliofika mbele ya Kamati na kutoa maoni yao ni pamoja na Chuo Kikuu kishiriki cha Ushirika na Stadi za Biashara Moshi, *Mtoni Lutheran Church Savings and Credit Co-operative Society, Service and Co-operative Union, Tanzania Society* na *Tanzania Federation of Co-operatives*.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifaidika sana na maoni ya wadau na kwa hakika maoni ya Kamati kuhusu Muswada huu ni matokeo ya maoni mazuri ya wadau. Mkutano wa Kamati, baada ya mkutano na wadau Kamati ilikaa kikao chake cha kawaida na kuzingatia mambo yafuatayo.

Kwanza *COASCO* kufanya kazi zake kitaalamu zaidi.

Pili Sheria kuimarisha ushirika nchini.

Tatu *COASCO* kufanya kazi zake kiushindani na kuingia maeneo mengine ambayo haikujihusisha nayo kwa mujibu wa sheria iliyopo.

Nne uteuzi wa wajumbe kwenye bodi ya *COASCO*.

Maoni, kama nilivyoelezea hapo juu Kamati pia iliwashirikisha wadau ili kupata maoni yao hivyo maoni haya ya Kamati yametokana na michango ya Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati kwa kutilia maanani mawazo mazuri ya wadau.

Mheshimiwa Spika, Kamati inakubaliana na mapendekezo ya marekebisho kwenye Muswada na kwamba marekebisho haya yataleta ufanisi wa utendaji kazi kwa upande wa *COASCO*, ikiwa ni pamoja na kuongeza wigo wa kazi. Shirika sasa linaweza kufanya kazi kwenye taasisi nyingine. Pia Muswada unaipata nguvu zaidi ya kusimamia na kuratibu zaidi shughuli za ushirika kwa kutoa miongozo ya kuboresha utendaji kazi.

Mapendekezo, kwa kuzingatia yote hayo Kamati inapendekeza yafuatayo:

Kwanza *COASCO* iendelee na juhudzi za kupata watumishi waliobombea kwenye fani za uhasibu na ukaguzi. Aidha wapatiwe nyenzo ili waweze kutekeleza kazi zao kwa ufanisi zaidi. *COASCO* kama shirika ipatiwe nyenzo za kutosha ili iweze kufanya kazi zake kwa ufanisi zaidi. Kamati inapendekeza kuwa uteuzi wa wajumbe kwenye bodi ya *COASCO* izingatie zaidi taaluma, usoefu na jinsia bila kuathiri taaluma.

Mheshimiwa Spika, hitimisho. Napenda nikushukuru kwa kunipa nafasi hii niweze kutoa maoni kwa niaba ya Kamati.

Aidha naomba nimshukuru Mheshimiwa Balozi George Kahama Waziri wa Ushirika na Masoko, Mheshimiwa Hezekiah Chibulunje Naibu Waziri Ushirika na Masoko, Dr. C. Komba, Katibu Mkuu wa Wizara ya Ushirika na Masoko pamoja na watumishi wote walioshiriki kuandaa na kuboresha Muswada, pamoja na ushirikiano waliounyesha kwa Kamati wakati wote wa kuujadili.

Naomba pia niwashukuru na kuwapongeza wadau waliofika mbele ya Kamati na kutoa maoni yao kama walivyotajwa kwenye kifungu cha (2). Namshukuru Mwenyekiti Mheshimiwa William Shellukindo kwa kunipataia fursa hii kuwasilisha taarifa hii. Aidha nawashukuru wajumbe wenzangu katika Kamati ya Uwekezaji na Biashara kwa michango yao mizuri ambayo iliwezesha kutoa taarifa hii. Napenda kuwatambua wajumbe hao kama ifuatavyo.

Kwanza Mheshimiwa William Shellukindo Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Salome Mbatia Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Fatuma Said Ally Mchumo Mjumbe, Mheshimiwa Margareth Bwana Mjumbe, Mheshimiwa Dr. Aaron Chiduo Mjumbe, Mheshimiwa Omar Chubi Mjumbe, Mheshimiwa Steven Kazi Mjumbe, Mheshimiwa Aisha Philip Magina Mjumbe.

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Khamis Awesu Aboud Mjumbe, Mheshimiwa Freeman Mbowe Mjumbe, Mheshimiwa Herbert Mntangi Mjumbe, Mheshimiwa Ali Machano Mussa Mjumbe, Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro Mjumbe, Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya Mjumbe, Mheshimiwa Semindu Pawa Mjumbe, Mheshimiwa Mohamed Abdulaziz Mjumbe, Mheshimiwa Dr. James Wanyacha Mjumbe, Mheshimiwa Christopher Wegga Mjumbe, Mheshimiwa Sumri A. S. Mohamed Mjumbe, Mheshimiwa Ali Said Mjumbe, Mheshimiwa Nazir Mustafa Karamagi Mjumbe, Mheshimiwa Abu Towegale Kiwanga Mjumbe na Mimi Ismail Ivvatta. (*Makofî*)

Ningependa vile vile kumshukuru Katibu wa Bunge Ndugu Diamian S. L. Foka, kwa kuiwezesha Kamati kufanya kazi zake bila matatizo na Ndugu Aggrey N. Nzowa, Katibu wa Kamati ambaye aliihudumia Kamati vizuri wakati wote. Waheshimiwa Wabunge nawashukuru kwa kuniskiliza.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono. (*Makofî*)

**MHE. AISHA P. MAGINA - MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, yafuatayo ni maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Muswada wa Kurekebisha Sheria ya Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika yaani *Act to Amend The Co-operative Audit and Supervision of 1982*. Kwa mujibu wa kanuni ya Bunge kifungu cha (43) kifungu kidogo cha (5) (b) na kifungu (81) kifungu kidogo cha (1) toleo la mwaka 2004.

Aidha natoa pole kwa familia za hayati Balozi Paul Bomani na Hayati Balozi Hassan Diria kwa kuondokewa na wapendwa wao na Mwenyezi Mungu awapumzishe kwa amani.

Mheshimiwa Spika, baada ya kupitia marekebisho ya Sheria ya Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika, imegundulika kuwa tafsiri ya baadhi ya maneno kama vile *Appex, Federation, Pre-Co-operative Groups na Registered Co-operative Society* ilifanywa katika kifungu cha (2) cha Muswada huu inafanyiwa rejea

katika Sheria nyingine ya Vyama vya Ushirika ya mwaka 2003. Hii italeta mkanganyiko kwa watumiaji wa Sheria hii ambayo itawalazimu wawe na Sheria zote pindi watakapotakiwa kutumia Sheria hii ya *COASCO*.

Mheshimiwa Spika, kitendo cha kufanya rejea tafsiri ya maneno ya Sheria ya *COASCO* kwenye Sheria ya Vyama vya Ushirika inamaanisha kuwa Sheria hii ni kama Sheria ndogo au kanuni za Sheria ya Vyama vya Ushirika. Kambi ya Upinzani inashauri kuwa itakuwa vizuri kama Sheria yenyewe itajitosheleza kwa kila kitu na sio kufanya marejeo kwa Sheria nyingine kama Sheria hii inavyofanya.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha (4) kifungu kidogo cha (1) (b) na (a) kinapendekeza kazi moja ya Shirika hili ni kusimamia Mashirika mengine ambayo yatatoa huduma za ukaguzi kwa vyama vya *Pre-Co-operatives and Co-operative Society*.

Hata hivyo hakuna tafsiri ya maneno *Pre-Co-operative Societies* badala yake kuna tafsiri *Pre-Co-operative Groups* kwenye Sheria ya Vyama vya Ushirika kama ilivyofanyiwa rejea tafsiri kwenye Muswada huu. Maneno haya *Pre-Co-operative Societies na Pre-Co-operative Groups* yanaleta ukinzani.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani ina shauri kutolewa tafsiri ya maneno hayo kwenye Sheria ya Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika, na sio kwenye sheria ya Vyama vya Ushirika, ili kuondoa utata utakaoweza kujitokeza.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha (3) cha Muswada huu ambacho kinarekebisha kifungu cha (4) cha Sheria hii kinapendekeza kuwa kufuatana na maelekezo maalum ya Waziri anayesimamia Shirika la *COASCO* haitapokea maelekezo au maagizo kutoka mamlaka yoyote.

Kambi ya Upinzani inashauri maelekezo maalum yaliyopendekezwa kwenye kifungu yawekwe bayana, kitu ambacho kitaondoa uwezekano wa Waziri kutumia vibaya madaraka yake kwa kutoa maelekezo maalum kwa manufaa yake binafsi au kwa manufaa ya kundi fulani.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuainisha baadhi ya dosari zilizomo katika Muswada huu wa *COASCO*, naomba kuwasilisha.

**MHE. TALALA B. MBISE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa ya kuchangia kwenye hoja hii, kwanza kabisa naomba kutumia fursa hii nifikishe mawili makuu niliyotumwa na wananchi wa Arumeru Mashariki.

Kwanza ni shukrani za dhati kabisa kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na timu nzima ya Wizara ya Ushirika na Masoko kwa kuunga mkono jitihada za ufadhili wa soko la Tengeru kwa jitihada zao kwa sasa hivi. Shukrani pia zinazotoka kwenye soko la Tengeru kwa kila siku ya Jumatano na siku ya Jumamosi na kwa jinsi ambavyo mmeokoa maisha ya watu amba walikuwa wanapoteza maisha yao kwenye barabara kuu ya

Arusha kwenda Moshi. Hizo shukrani wameniomba nizifikishe kwa Wizara hii kwa kuwaokolea maisha yao na kuwaongezaa uwezakano wa kujiondolea umaskini.

Pili wanawaomba pia muwasaidie kupeleka shukrani zao kwa wafadhili waliowezesha hilo ambaa ni *Chapter ya Rotary International* ya Arusha, New Zealand na Canada. Pia wanashukuru Wizara kukubali *option* ya kutizama uwezekano wa kuboresha gulio la Kikatiti.

Pili ni maombi waliyoleta rasmi, maombi ambayo wanaleta ni ambayo nadhani haya hayatakuwa mageni kwa Wizara ni ambayo nimekuwa nikilia nayo hapa nadhani tangu niye kwenye Bunge hili mwaka 2000. Nayo ni kuhusu masuala mawili, kwanza ni madeni ambayo wanadai ushirika na madeni hayo ni aina mbili.

Mheshimiwa Spika, madeni ya aina ya kwanza ni hela ambayo walikuwa wanakatwa kwenye mauzo ya kahawa yakaingizwa kwenye kitabu cha amana. Yamekuwa yakikatwa kwa muda mrefu na hayo madeni wamekuwa wakidai kwa muda mrefu lakini kwa bahati mbaya hayajalipwa mpaka leo. Madeni ya aina ya pili ni madeni ya kahawa iliyotolewa ikauzwa lakini fedha haikulipwa, wakaendelea kudai walipwe hela yao lakini kwa bahati mbaya hiyo hela haikulipwa na mpaka leo wanaendelea kudai.

Wananchi hawa wanadai hiyo hela yao nadhani kwa watu wanaofahamu Arumeru Mashariki kwa kweli kule kahawa ndio siasa na hii hapa sitaendelea zaidi kufahamu kwamba nina maana gani. Wao wanadhani kwamba Serikali ndio inayohusika na mimi nakubaliana nao kwamba Serikali inahitaji kutoa kauli kuhusu haya madeni. Kila wakinituma na mimi nasema nimefikisha Bungeni wanangojea kauli ya Serikali hawaisikii na hawaoni.

Mheshimiwa Spika, wakati huu tunaomba Serikali iwafikishie kauli kwamba kuhusu hayo madeni yao kitabu cha amana na kahawa waliyouza na ambayo haikulipwa. Je, hiyo hela yao imepotea na ikumbukwe kwamba hii hela ilipotea wakati ambapo *COASCO* ilikuwepo na ilikuwa inafanya ukaguzi huu, tunashukuru kwamba sasa labda huenda mambo yakabadilika. Lakini tungependa yabadilike wakati ambapo wananchi mifuko yao itaonyesha na tungependa Wizara ifanye kazi, tuione hiyo kazi katika mifuko ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, chombo hiki cha ukaguzi na usimamizi wa Vyama vya Ushirika hakitakuwa na manufaa nasi kama wakulima wa kahawa au pamba au zao lingine lolote, kama mkulima hatapata kulipwa haki yake kwa mazao yake mara anapouza. Kwa kweli sisi wakulima ukituambia kwamba anakagua mazao yake, anakaguliwa anapouza na kwamba yule anayenunua anakaguliwa vizuri, mkulima yeze hiyo hatajali sana, hajui kwamba hayo yanafanyika wapi, anachojali ni kwamba analipwa hela yake.

Mheshimiwa Spika, ombi letu tutarudia tena na tena kwamba tunaomba tuhakikishiwe kwamba madeni yetu yatalipwa.

Sasa nirudi kwenye Muswada, kwenye Muswada huu naomba nirudi kwenye ukurasa ule wa 78 na 79. Kwenye ule ukurasa wa 78 ile Ibara ya 4 vile vifungu vidogo (a) mpaka (c), mimi hapo inanichanganya changanya kidogo. Ninajiuliza maswali pale ya kwamba hii *COASCO* ambayo inafanya Shirika na litafanya ukaguzi, naanza kujiuliza maswali kwenye Serikali kuu tulikuwa na *Tanzania Audit Corporation*. Serikali ilipojiondoa kwenye kutenda kazi moja kwa moja ikaondoa *Tanzania Audit Corporation* kwenye ngazi hii tuna *COASCO*, *COASCO* tunaiboresha na kulingana na kile kifungu (a) ni kwamba itaendelea kutenda.

Mheshimiwa Spika, lakini katika mazungumzo tunasema kwamba haitatenda badala yake itasimamia tu. Lakini tunakanganya pale kidogo (a) na (c) moja tunasema itafanya *Audit* na kingine tunasema kwamba itasimamia wale wanaofanya *Audit*. Hapo kwa kweli nadhani kuna haja ya kunyoosha na kuwa wazi kwamba hawa sio watendaji na tusingependelea kwamba tunaanza Shirika tena la Umma la kufanya kazi ambazo zinafanyika na *Private Sector*. Tuanze tena Shirika la Umma katika *sub sector* ya Ushirika iwe kazi yake ni kushindana na *Private Sector* katika kutoa *Audit Services*, mimi nisingependelea kuona kwamba ndivyo inavyofanyika.

Kuhusu zile kazi ambazo zinaainishwa pale *research* na *consultancy*, mimi nadhani ndio sababu ya *ku-strengthen cooperative college* na kuifanya Chuo Kikuu. Ni ili ifanye kazi hizo na nadhani pale ndipo pa kulenga na *ku-strengthen capability* zao ndio kazi yao kufanya *research* na kufanya *consultancy*. Kuwapa tena majukumu wao *COASCO* ya kufanya *research* tena kama *Private Sector Institution*.

Mimi nadhani inahitaji kufikiria zaidi, labda wao tuwape *rightly* kama vile tunavyoainisha kwenye kifungu (c): “*To formulate Audit and Accounting Policies for adoption by...*,” mimi nadhani wana maana *co-operative groups*. Hiyo ni *fair*, hiyo ni *rightful* kwa *COASCO* wao kazi yao iwe ni *ku-formulate Audit and Accounting Policies za Co-operative sub-sector, that is fair*. Lakini sio kwenda *ku-practice* ile *accounting* na *Auditing* na mambo ya kusema usimamizi kwa kweli mimi nadhani hiyo inahitaji kutizamwa zaidi.

Ukurasa ule wa 79 ile namba 7 pale juu ya pili kutoka mwisho kwamba *subject to special direction*, pale mimi kidogo inanisumbua kwamba eti wao watakuwa chini ya Waziri tena eti Waziri ni kwamba itakuwa ni *very special*. Mimi kidogo inanipa matatizo pale kwamba *COASCO* itakuwa ni so *unique*, kwamba usimamizi wao kutoka kwa Waziri itakuwa ni so *special* na hakuna mtu mwingine anayeweza kuwagusa halafu ukitizama hapo juu tena wanakuwa na *powers* tena zinakuwa *specialize* kabisa.

Mimi nadhani hiyo kidogo inanipa matatizo, mimi nadhani wanahitaji kuwa *under the overall supervision* ya Wizara na wao kupata *direction* na *guidance* ya Wizara and therefore chini ya Waziri, mimi sidhani kwamba hiyo inahitaji iwe *special unless* labda hiyo inakuwa *defined*.

Mheshimiwa Spika, langu la mwisho ni kuhusu kutizama hii *sub-sector* ya ushirika kwa jumla. Mimi pendekexo langu la jumla ni kwamba *sub-sector* ya ushirika

inahitaji maboresho kwa ujumla wake. Kwa sasa hivi *approach* ambayo tumekuwa nayo ni kutizama kimoja kimoja. Je, kuna uwezekano wa kuitizama hii *sub-sector* huku inatizamwa kama *movement* labda hiyo ni sawa. Lakini kuna uwezekano wa kutizama *Corporative*, kuitizama *the whole* na kuiboresha kama vile tunavyoboresha *Local Government, Public Service* tukaitizama hii ikitizamwa *as a whole* badala ya kwenda *piecemeal*. Kwa hiyo, mimi ningependekeza kwa kweli sasa hivi kuna haja ya kutizama ushirika *as a total package* ikaboresha na ikawa na *total reform programme* kwa ajili ya kuboresha ushirika.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru na ninaunga mkono hoja. (*Makofî*)

**MHE. JOHN E. SINGO:** Mheshimiwa Spika, naomba na mimi nikushukuru kwa kunipa nafasi ili nichangie hoja iliyoko mbele yetu. Awali ya yote nimpongeze Mheshimiwa Waziri na Naibu wake na Katibu Mkuu kwa kazi nzuri inayohitaji changamoto katika kuboresha Wizara hii ya Ushirika na Masoko. Lengo la Ushirika katika nchi yetu limefikia mahali pagumu sana kwa sababu imani za wananchi wetu sasa hivi ni hafifu sana kuhusu ushirika.

Kwa kweli wao wana changamoto kubwa sana ya kubadilisha imani za watu, kuwabadilisha watu imani ni kitu kigumu sana. Sasa leo tunaletewa sheria hii yenye lengo la kuifanyia marekebisho sehemu kidogo kidogo kwa kuangalia upande mmoja tu wa hawa wasimamizi wa Vyama vyetu vya Ushirika kwamba viweze kuwa salama kifedha, kiuchumi tunataka kubadilisha hii sheria ili iweze kuendana na uchumi wa sasa hivi ambao ni wa soko huru. Mimi nafikiri sheria hii imeletwa wakati muafaka, lakini wakati ambapo wananchi imani zao kuhusu Ushirika zimekwisha na kuwachosha.

Mheshimiwa Spika, sasa mimi ningependa kutoa tahadhari mbili au tatu kuhusu hali ilivyo sasa hivi ya ushirika na mabadiliko hayo tunayoyafanya. La kwanza ni kuhusu ukaguzi ulikuwa unafanyika, ulikuwa na upungufu mkubwa sana. Kwamba ukaguzi ulikuwa unafanyika nyuma ya muda, labda kama ilikuwa ni fedha za Ushirika zitakuwa zimeshamegwa, zimeshatumika na umeshapita muda mrefu labda mwaka au miaka miwili. Sasa ndio wakaguzi wanakuja, hawa ambao tunawatengenezea hii Sheria sasa pamoa na kuweka hii sheria inabidi haya mapungufu yaweze kuangaliwa na kuweza kuwekewa utaratibu yasiendelee kutokea.

La pili hatua za Kisheria (*Legal Measures*), zinachelewa kuchukuliwa na wakati mwingine Mahakama imekuwa ikipindisha haki ya wanaushirika na kumpa mtu mmoja ambaye amekosea Ushirika *either* kwa kuibia Ushirika. Sasa vile vile tungeangalia Mahakama zetu, watu wengi ambao wameibia Ushirika wamefikishwa Mahakamani, lakini inasikitisha kwamba wamekuwa na mianya mingi ya kuweza kuachiwa na kuondokana na kupatikana na hatia.

Je, Mahakama zetu zitaifanya haki Sheria hii tunayoitunga? Je, sheria hii tunapoiweka itaweza kulinda Ushirika? Je, Mahakama itaweza kusimamia vizuri maelekezo ambayo sasa hivi yanapitishwa kama sheria? Na hii ndio inayofanya wananchi wetu wanaoshiriki katika Ushirika haswa kule kwetu tuna *VUASU Co-operative Union*. Wananchi wakambiwa wajijunge na Ushirika wanakata tamaa sana, wanakata tamaa

wanapoonaa wale waliowaibia wanaendelea kupiga mkono barabarani na Mahakama zimewaachia huru. Sasa nachukulia mfano wa wakulima na Ushirika, Vyama vyaa Ushirika kama urafiki wa mbwa mwitu na komba.

Mheshimiwa Spika, mbwa mwitu na komba walikuwa marafiki wakubwa sana. Siku moja mbwa mwitu alitamani matunda yaliyokuwa juu ya mti, akamwambia komba amsaidie kumteremshia matunda kama vile ushirika pamoja na wakulima. Komba hakufanya hiyana akapanda juu ya mti, wakati anatafuta matunda amteremshie mbwa mwitu hapo chini kwa sababu hawezi kupanda kwenye mti akachomwa na miiba mara mbili mara tatu. Damu yake ikachuruzika pale chini komba akiendelea kutafuta matunda. Mbwa mwitu pale chini akaona damu ya komba ikidondoka pale tone moja moja akaona ile harufu ya damu yake inamanukato mazuri na utamu fulani akaanza kuilamba.

Komba kule juu ya mti akamwangalia mbwa mwitu pale chini analamba damu yake akamwambia sasa ndugu yangu sijakuteremshia matunda umeanza kuramba damu yangu huu urafiki utatufaa kweli? Kuanzia pale urafiki wa Komba na Mbwa mwitu ukaisha. Sasa ndio upofikia uhusiano wa ushirika na wakulima. Imani imepotea kabisa, watu wanapoweza kukomba amana za ushirika halafu wakaachiwa huru wakapita barabarani. Urafiki wa namna hiyo hata tungeutungia sheria namna gani hautatufikisha mbali. Tumesema tunataka kuufufua Ushirika ndio lengo haswa ndio madhumuni haswa ya hii sheria tunataka tufufue, tuimarishe na kuendeleza Ushirika kwa hii sheria. Lakini kwa mwenendo huu wa kuwaachia walioibia ushirika wanapita barabarani wananchi hawatakuwa na imani na ushirika.

La tatu ni kuhusu uongozi dhaifu, moja ya uongozi dhaifu ni kushindwa kukemea mabaya, ama kufanya upendeleo. Sasa ndani ya hiki chombo kuna hayo madhaifu ambayo mimi nafikiri kuyatungia sheria sioni sehemu yake ya kuiweka. Huwezi ukamtungia mtu sheria ya kutofanya upendeleo kama ana dhamira ya kufanya upendeleo na upendeleo unaleta mgogoro sehemu ya kazi. Watumishi wanashindwa kuamini uongozi.

Sasa kama tunataka Ushirika ufaulu lazima tuwe na uongozi madhubuti, uongozi unaoaminika, uongozi unaokubalika. Siyo kwa sababu ya sheria, lakini kwa sababu tunataka kujenga ushirika, je, tulifaalu vipi kujenga ushirika wakati uliopita? Tungerudi na *ku-compare notes* huko wakati uliopita na sasa kimetokea madhaifu gani? *Nepotism*, kiongozi anajiona yeye ni Mungu mtu huyo anayeongoza hilo Shirika akajiona yeye ni Mungu mtu, basi hawapi wale watumishi anaongoza imani. Hata kule anapokwenda kufanya ile kazi imani haipo wanapokwenda kufanya tu kwa sababu wako katika ajira, na hii ikishaanza kuleta migogoro basi Msimamizi wa hili Shirika la *COASCO* hatafaulu hata kama hii sheria tungeifanyia mabadiliko.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi ningeiomba Wizara la kwanza iweze kuangalia mapungufu yaliyosababisha tukaanguka katika Ushirika huko tulipopita na vipi tunaingia katika huu uchumi wa soko huru na vipi tufanye mabadiliko ya jumla badala ya kufanya mabadiliko ndondondo au kidogo kidogo. Leo tunataka tubadilishe hapa kesho

tunataka tubadilishe pale, tungeomba Wizara kama alivyosema msemaji aliyejita iangalie kufanya mabadiliko ya ujumla kwa ajili ya kujenga ushirika.

Wananchi walipenda sana ushirika miaka iliyopita ilikuwa ikiwapa faida, lakini sasa hivi wameogopa mno. Kule kwangu wameamua kuunda vikundi vyao vya watu wachache lakini hawapendi kujiunga na ushirika. Sasa tungeomba Mheshimiwa Waziri kwa uzoefu wake na ujuzi wake wa siku nyingi aweze kutusaidia kwenda kuangalia upya na kutuletea sheria ya ujumla na marekebisho ya ujumla ya kuweza kufanikisha Ushirika katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naunga hoja mkono na kuiombea Wizara mafanikio. Ahsante. (*Makofî*)

**MHE. EDSON M. HALINGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ili na mimi nionyeshe wasiwasni wangu juu ya mabadiliko ya sheria hii.

Mheshimiwa Spika, kwanza lengo letu lingekuwa kuokoa Vyama vya Ushirika visife na kujenga imani kwa wananchi. Lakini sheria hii haituonyeshi kuwa itafanya hivyo, wananchi wamezulumika sana kwa hali hii hawana imani na ushirika unaoendelea sasa. Kwa hali hiyo hatutapata nafasi ya kuweka ushirika huu tunaouzungumza katika nguvu tunayoitegemea. Sheria ya ushirika ilipaswa kuwa ijitegemee yenye ni kasehemu kama wanavyodonoa donoa hivi, iainishe na ielekeze na hasa katika suala la kusimamia mapato ya wakulima au wanachama wa ushirika uliopo. Hilo tu ndio inayoweza ikatupa nguvu, hii tabia ya kusema ukaguzi umefanyika waitwe wanachama ndio waje waamue yule mtu ashtakiwe au alipe na wakati katika ajira ya watu hawa inategemea sana katika hali ya watu wanavyooleweka na ukoo uliopo pale wenye nguvu ya kuwasimika wale wafanye kazi pale. Kwa hiyo, matokeo yake ni kwamba watu wanakata tamaa hawana nguvu, hawana nia wala hawana uwezo wa kufuatilia.

Pili, tunayo Idara ya Ushirika ambayo ndio ina wakaguzi wale kama ushirika upande wa Serikali Wilayani au popote pale. Sasa watu hawa wanakagua, hawakagui kwa njia ya kuokoa na kuwapa haki wakulima, wanakagua kwa nia ya kusema tu mambo yamepita. Mimi huko niliko kuna vyama vingine havijapata majibu ya ukaguzi uliofanyika hata miaka mitatu minne iliyopita mpaka leo. Sasa kama ndio hivyo unawapa nguvu zipi ushirika, na kama hivi ndivyo wale ndio wanaopaswa wapite kila wakati na kukagua vyama hivi vya msingi na vyama vingine vya ushirika mkubwa na nini.

Lakini sasa hawa hawana nafasi yoyote ya kuingilia wala kubana wale wanaozulumu vyama hivyo havina. Wanafika tu pale wanakagua wanasema vitabu sijui vinakaa mwaka mzima havijapitishwa je, *COASCO* itafanya nini wakati ile Idara haijakamilisha na hakuna mwaka mimi nikaona kwamba Idara ile itapitia vyama vyote vya msingi katika wilaya pale sijaona. Sasa hii *COASCO* itachukua wapi taarifa hizi za kukagua kila mwaka na taarifa itoke.

Hapa kwa kweli tusipozingatia nguvu ya ushirika itazidi kudidimia na haitakuwepo na kule kwangu watu wameamua kuwa na vikundi ambavyo kwa kweli ni

ushindi wa ushirika na inaonekana wanajipatia manufaa. Hawa wala hawahitaji *COASCO* wala ukaguzi wa Idara ya Ushirika, wao wanakusanya mazao yao wanayaiza wakishapata kule wanakaa wenyewe mazao wenye wanagawana ninaona wanakwenda vizuri. Sasa sijui, na kama mnasema wawe na uhuru wa kuchagua ni chama gani au ni Shirika gani likague sina hakika kama wale kwangu watakuwa tayari kuiomba *COASCO* ikakague. Hawatakuwa na haja ya ukagazi wowote maana mambo yao sasa wanajipatia kwa kadri wanavyohitaji, kwa hiyo, tunaiwu hii *COASCO* haitapata kazi na chama.

Pili, tumekwisha jenga tabia ya hawa watu wanaokagua wasifuatwe na kutimiza wajibu wao kwa haraka na hii imekatisha tamaa watu. Sasa wanakagua lakini kukagua huku wanakagua kumpa mamlaka gani? Kama ni sheria iwape mamlaka basi hawa wakaguzi wapeleke Mahakamani wanapopata mtu yejote ambaye ameibia chama kile au amehujumu mali ya chama kile. Hawa ndio wakatetee wawe ndio washtakaji, wasimamizi wa kesi hizo Mahakamani, lakini sasa mnakagua halafu mnasema uanachama wenyewe wakapeleke Mahakamani. Watu wenyewe wameingia pale kwa uelewano leo ukaseme eti waende Mahakamani, watu wanasema ya nini bwana tukahangaishane huko na kesi kwani ni ya leo hii.

Lazima sheria ingekaza kwamba wale watakoopeleka Mahakamani watozwe adhabu ya kutosha na pia watu hawa vile vile wasihisiwe maana wanachukua vitu vy a wazi wazi wanajenga majumba, wanunu magari, wanunu mashine. Sasa hakuna sheria inayosema wafilisiwe wala wabanwe vipi wanasema watu wenyewe waamue sasa sisi tumejitolea nguvu yetu inaliwa hivi hivi mseme tena ndio tusimamie tuamue.

Sasa hapa mimi nadhani sheria hii haina nguvu sana kutuwezesha kuimarisha vyama hivi halafu tunasema *COASCO* itasimamia ukaguzi wowote utakaofanywa katika Vyama vy a Ushirika. Lakini wale wenyewe chama wana haki ya kuchagua nani akague hivi ina maana gani hapa? *COASCO* wasimamie ukaguzi wa chama kingine na yale malipo na ushuru wanaotoza hapa watozwe kwa namna ipi.

Sasa hii nadhani tuepukane na masuala ya Ushirika kuwapatia watu nafasi ya kupata mapato ambayo si halali yao, wala hawakufanya kazi inayowapa nafasi wale wazalishaji kukubaliana na kuweza kupata hali ya maendeleo. Wao ndio watakoakagua ndio wapate haki na kudai ule ushuru wa kuendeleza Shirika lao wasiofanya hivyo hawana sababu ya kudai ushuru wowote.

Mheshimiwa Spika, halafu pia tunaposema wafanye utafiti, wafanye utafiti *COASCO* kwa namna vipi, wana taratibu zipi za kufanya utafiti? Mimi nina amini tulipopitasha Chuo Kikuu cha Ushirika cha Moshi ndicho kitakuwa msingi na uzalishaji wa si kila mtu ana mabadiliko mapya na ya kisasa ya kuleta maendeleo katika Ushirika wa nchi hii. Sasa tuweka wale wabovu walioitungusha na kutuzurumu huko nyuma, mnasema tuwategemee tutakwenda wapi?

Mheshimiwa Spika, mimi kwa kweli hili nadhani hapa Serikali vizuri ikaliangalia hilo ili waweze kuona kwamba wanaandaa kitu ambacho kitatusaidia. Halafu ile ni Ibara ya 7 ile anasema Waziri kama anaweza kuruhusu *under sub section for aweze kuruhusu*

ukaguzi ufanyike au utekelezwe kulingana na maamuzi ya Ushirika uliopo. Sasa Waziri hapa mimi nadhani tunamletea matatizo bure tu, Serikali italaumiwa bila sababu, kama ni Shirika hili tunalipa *COASCO* liwe ni hilo ndio lilaumiwe kwa kutokutekeleza shughuli zake. Tusiweke vitu vingine na tusije tukamchafua bure Waziri kwa sababu tu ya vile ambavyo havikutekelezwa kwa sababu ya ulegevu wa Sheria tunayoiweka wenyewe.

Mheshimiwa Spika, mimi kwa hili nadhani ni vizuri tungefikiria vizuri zaidi juu ya sheria hii. Sasa kama ni kuunganisha na ile ya zamani lakini nadhani hii italeta matatizo zaidi na tutapoteza nguvu ya *COASCO* na hata Bodi itashindwa hata kusimamia masuala haya.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Ahsante. (*Makofi*)

**MHE. JACOB D. SHIBILITI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kutoa mchango wangu katika Muswada huu ambao ni muhimu sana kwa Vyama vya Ushirika.

Mheshimiwa Spika, kabla ya yote, niungane na Wabunge wenzangu kwa sababu ni mara ya kwanza kusimama katika kikao hiki nitoe pole kwa familia ya Mheshimiwa Balozi Ahmed Hassan Diria na Balozi Paul Bomani. Niombe sana roho za Marehemu hao ziwekwe mahali pema peponi, *Amina*.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu wa Wizara ya Ushirika na Masoko kwa kazi ambayo kwa kweli inaonyesha matumaini makubwa kwa jinsi walivyosimamia Muswada huu na kuufikisha leo hapa, inaonyesha wamefanya kazi nzuri sana, nawapongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa vile ni shirika ni vema nikamtambua Mwenyekiti wa Bodi hiyo ya Shirika la *COASCO* na Mkurugenzi wake, wamejitalidi kuleta Muswada huu kwa wakati muafaka, nao nawapongeza pia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunapozungumzia ushirika tunakuwa tumewagusa wananchi wa kawaida walio wengi na tumekuwa tukipigiwa kelele hapa tubadilishe sheria, tusimamie mali za wananchi ni haki na chombo hiki mara kwa mara kinaonekana kwamba kipo na kipo kwa ajili ya kulinda maslahi ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, nielezee kwamba sheria iliyopitishwa itatusaidia sana kuboresha yote ambayo yanaonekana ni kero kwa wananchi. Waziri amesimamia vizuri na sheria tumeipitisha hapa na itakapokuwa imefuatwa mambo mengi yatarekebika.

Mheshimiwa Spika, lakini ni vema nikasema kwamba ushirika kweli una makosa lakini kuna taasisi nyingine pia za Serikali zenye makosa makubwa kuliko hata ushirika. Tukiangalia tu labda tugusie kwenye Serikali za Mitaa, ni mamilioni ya pesa tumeyaona hapa yametumika visivyo, ni pesa za wananchi. Wakurugenzi karibu 11 sasa hivi wamepelekwa Mahakamani, nao ni sehemu ya mali ya umma.

Kwa hiyo, tunapougusa ushirika, ushirika umeyumba kutokana na matatizo mengine ya kisera. Lakini kutokana na juhudzi zako Mheshimiwa Waziri tuna imani hali inavyozidi kuendelea unaboresha na tuna imani kabisa Rais ajaye kama ataona umuhimu wa kuendelea kuwa na Wizara hii basi Wizara hii itakuwa ni tegemeo la umma kabisa kabisa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, mpango uliouanzisha wa kuwa tunachukua *bill* mapema inaenda kusomwa inazunguka kwa wadau ni mpango muhimu sana. Muswada huu nimekuwa na masikitiko kidogo kwa sababu umecheleweshwa kidogo kuwafikia wadau. Umefika kwa wadau tarehe 30 Machi, kwa hiyo, michango ya wadau zaidi haikuweza kushirikishwa, ni muda mfupi sasa sijui kwa nini ulichelewa kuwafikia wadau na badala yake ni wachache sana waliohusika kwa ngazi tu ya Taifa kwa maana ya *TFC* pamoja na *SCULT*. Kwa hiyo, kwenye Vyama vya Msingi amba ni walengwa hawakuhusishwa zaidi. Lakini pamoja na hayo kuna mapendekezo mbalimbali ambayo wameona ni vema yafanyiwe marekebisho.

Mheshimiwa Spika, wenzangu wamezungumzia kile kifungu cha nne, sheria imetoa mwanya kwamba sasa shirika linakuwa huru linaweza likakagua taasisi nyingine lakini bado kumekuwa na sehemu ya kuatamia huku tena wakati ule uhuru tumeshautoa kwa vyombo vyote yeye *COASCO* tumemruhusu anaweza kukagua na mashirika mengine hatujamfunga lakini bado huku kwenye Vyama vya Ushirika anasema kwamba yejote mtakayempata lazima mimi nihakikishe kwamba amefanya kazi hiyo.

Sasa kwa nini uingilie tena? Naomba hapo Vyama vya Ushirika viwe huru kutafuta mkaguzi mwagine yejote yule ambaye amekubalika na mashirika mengine ya Kimataifa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hapa soko huria lione kane kwamba linatumika, awe na uhuru kutafuta huyu mlaji, huduma bora iko wapi na ikiwa katika kiwango cha Kimataifa. Sasa kama utamzuia utakuwa umemnyima uhuru kabisa, bado utaendelea kumfunga huyu mtu aonekane kwamba hawezi, hawezi kama unamlea. Kwa hiyo, hii wameona kwamba si vema ikaendelea kuwepo. Irekebishwe, Vyama vya Ushirika wapewe uhuru kutafuta yejote yule ambaye anaweza akakagua mradi anatambulika kisheria. Hilo wamelitaja na ninaomba sana lijaribu kuzingatiwa.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu haya ni marekebisho tu na ni sehemu ndogo, sehemu nyingine ambayo wamegusia ni Wakurugenzi wa Bodi, Mwenyekiti hawana matatizo naye, huyu *one member representing the Controller and Auditor General* hawana matatizo naye, *the Registrar of Cooperative Society* hawana taabu naye, *the secretary general of federation* hamna taabu, *the Principal of the Moshi Cooperative University*, inaonekana ni kama Serikali inataka kuzidi kwenye bodi, wadau wengi kwa nini wasihu shwe? Naomba hapo nipate maelezo hiki kipengele cha (e) kutoka Chuo cha Ushirika Moshi basi apatikane mdau kutoka kwenye ushirika. *The Commissioner of Budget* anaingia tena huko kwenda kufanya nini? Sisi tuko hapa kwa ajili ya kupitisha Bajeti, bado aingie tena kule ndani, tuongeze hapa angalau apatikane mwanamama mmoja kutoka kwa wana ushirika. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kwenye hiki kipengele kingine huku mwisho ambapo umetoa kwa wanaushirika wawili baada ya kuwasiliana na Waziri tunakubali lakini nimesema kule ndio apatikane mwanamama kwa wale wawili na hapa ningependekeza kwamba *Commissioner of Budget* apatikane na kama ni wadau wengi tukishindwa sana angalau ianishwe Mbunge basi aonekane kuingia kule huyu ni mwakilishi wa wananchi lakini sasa hivi kwa nini Mbunge haonekani mahali popote? Sina matatizo kabisa iwapo Mbunge yejote atawakilisha huku kwa sababu ni mwakilishi wa wananchi. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, sasa hivi kumekuwa na tabia ukitaka kuingia mahali hao wanasiasa, wanasiasa, bila siasa nchi haiendi. Kwa hiyo, wanasiasa wawe wanaigia kwenye mashirika haya. Tupo hapa kwa ajili ya kutengeneza sera za nchi, kuingia kwenye bodi fulani kunakuwa kuna mizengwe hawa wanasiasa, wanasiasa maana yake nini? Lazima wanasiasa waheshimike tuko hapa kwa ajili ya maslahi ya nchi hii. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, niendelee kumpongeza Waziri kwa usimamizi wake mzuri na jinsi shughuli zetu anavyozidi kuziweka kwenye mazingira mazuri.

Mwisho nigosie kuna suala moja ambalo limekuwa likizungumzwa zungumzwa linahusiana hasa na *COASCO*. Waandishi wa Habari wanapokuwepo hapa ndio wanasaidia kuuelewesha umma kuna nini kinaendelea. Popote pale wanapopata wanaandika kwa hiyo, lolote unaloliona likiwa kwenye gazeti wamelifanyia utafiti. *COASCO* nadhani imekuwa na matatizo, mara kwa mara wanaandika barua kwenda kwa Waziri, *COASCO*, *COASCO* kila siku inaandikwa. Labda kama ilikuwa ni tatizo la sheria hii basi ingekuwa vema tukaelezwa kwamba tatizo ilikuwa ni kwa sababu ya sheria, kelele sasa *COASCO* zitaisha, kuna nini hapo *COASCO*? Kama tatizo lipo kwa nini tusilirekebishe watu wakawa na imani na chombo chetu hiki ambacho ni tochi? Kila leo kwenye magazeti, Waziri ana kazi nyingi za kufanya kila leo analetewa msururu wa maandishi yanahitaji msaada wa Waziri kusaidia *COASCO* uongozi, uongozi.

Ningependa nipaye ufanuzi na umma uelewe kwamba tatizo lililopo *COASCO* ilikuwa ni hili na liko katika hatua hii ili angalau chombo hiki kiendelee kuaminika. Ni chombo muhimu, ni chombo kitakachosaidia wanaushirika kujua haki zao, wanaenda wapi, wanapaswa wawe wapi.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ni marekebisho tu yanayoipa nguvu sheria yetu tulioipitisha, nina imani kabisa wahusika wataweka vizuri na baadaye yataungana na sheria yetu ili wana ushirika waweze kuneemeka na sheria yao pamoja na shirika lao la *COASCO*.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo, naunga mkono hoja. (*Makofit*)

**MHE. KHALID S. SURU:** Mheshimiwa Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kutoa mchango wangu katika hoja hii ya Shirika la Ukaguzi la Vyama vya Ushirika nchini ya mwaka 2005.

Mheshimiwa Spika, kimsingi kabisa mimi sina tatizo na hoja yenyewe, kwa sehemu kubwa naiunga mkono lakini pia nitakuwa na hoja zangu au nitakuwa na mchango wangu ambao ninaamini kabisa utasaidia kuimarisha *COASCO* yenyewe pamoja na ushirika wenyewe, maana hivi vitu lazima viende pamoja.

Mheshimiwa Spika, nitazungumzia maeneo mawili kwa jinsi ninavyoona ushirika na *COASCO* yenyewe na hali halisi kule vijijini. Nitazungumzia habari ya ushirika, huu ushirika unamkomboa nani kwa sababu *COASCO* wako kwa sababu ya ushirika lakini pia vikwazo vyta maendeleo ya ushirika nchini maana lazima tukubali kwamba ushirika upo lakini una vikwazo, tukiondoa vile vikwazo tunaweza tukafanikiwa sana na malalamiko yatapungua.

Mheshimiwa Spika, ziko hoja kama tisa hapa zinazolezea ushirika hasa unamkomboa nani. Kwanza, ushirika unawakomboa wavuja jasho kule vijiji. Ushirika peke yake ukijengwa vizuri ndio utakaosaidia kuinua uchumi kwa wananchi wale wa chini na ndio maana hata sheria hii imeletwa hapa ili tuone namna ya kuwainua wananchi kule vijiji kupitia ushirika hakuna njia nyingine njia ya mtu mmoja mmoja tutachelewa sana kujenga uchumi na tutachelewa sana kuondoa umaskini wa kaya, wa jamii na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, lingine ni wafugaji na wachungaji vijijini. Kule vijijini wako wafugaji lakini wako wachungaji. Wale wachungaji nao wakiunganishwa wakafanya kazi zao kwa ushirika tutafanikiwa zaidi katika kujenga uchumi kupitia ufugaji wao na uchungaji wao. Kwa hiyo, ushirika ni suala la msingi kabisa na ndio maana sheria imeletwa hapa ili tuweze kubadilisha sheria iweze kwenda na wakati kwa ajili ya kuwasaidia hawa.

Mheshimiwa Spika, lakini sio hao tu hata wavuvi wa samaki, ili tuweze kufanikiwa lazima wakae katika ushirika na waweze kuvua zaidi na katika kuvua zaidi watauzza zaidi watapata uchumi zaidi.

Mheshimiwa Spika, lakini sio hilo tu hata wachimbaji wale wadogo wadogo wa madini, tukitegemea wachimbaji wakubwa peke yao ambao sisi hatuna tutachelewa sana katika kujenga uchumi wetu. Kwa hiyo, lazima ushirika uingie katika kuhamasisha na kuaweka pamoja wachimbaji wa madini katika vikundi vidogo vidogo.

Mheshimiwa Spika, lakini pia ushirika ni mkombozi wa uchumi wetu huu wa kisasa, uchumi tunaotaka sasa, ni muhimu sana kupitia katika ushirika.

Mheshimiwa Spika, halikadhalika ushirika huu unachochea kuunganisha nguvu ili kuharakisha maendeleo ya wananchi na hatimaye nchi yetu kwa jumla kiuchumi lakini pia ushirika unakabili suala la kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Spika, tisa, ushirika ni dhamana nzuri kwa vikundi kuweza kwenda kukopa na kadhalika. Kwa hiyo, ushirika wenyewe ndio dhamana nzuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, nilipenda hayo niyabainishe ili tuweze kuona umuhimu wa ushirika na sheria tunayoitunga, lakini pia nataka nibainishe vikwazo basi, viko vikwazo vingi sana ambavyo vinafanya ushirika wetu usiende mbele.

Mheshimiwa Spika, kikwazo cha kwanza au nambari *wahedi* ni umaskini wa fursa. Sasa umaskini wa fursa huo wa fursa vipi? Ubovu wa barabara vijijini ambazo zingewasaidia kusafirisha mazao kwenda katika ushirika, masoko na kadhalika. Kwa hiyo, hicho ni kikwazo cha msingi kabisa cha ushirika vijijini.

Lakini pia kikwazo kingine ni ukosefu wa mawasiliano, simu, posta na kadhalika. Huku mijini kumekuwa na mawasiliano ya kutosha simu zipo na kadhalika lakini kule vijijini kwa sababu simu hazijafika posta ni muhimu ili wakulima na hawa wa fugaji wetu hawa waweze kuwasiliana na wananchi na masoko mbalimbali.

Lakini pia kikwazo kingine ni kilimo cha aina ya ujima ambacho bado tunacho. Kwa hiyo, kupitia ushirika tunaweza kuondokana na kilimo hiki cha ujima ili kiweze kuzalisha mazao zaidi na tuweze kujenga uchumi zaidi.

Mheshimiwa Spika, lakini kikwazo kingine ni elimu yenye ya ushirika haijaenea vizuri. Elimu hii ipo kwenye makundi makundi tu lakini elimu ya ushirika haijaenea kwa wadau walio wengi.

Mheshimiwa Spika, lakini kikwazo kingine ni kukosa umeme, umeme ni muhimu sana katika maendeleo haya ya sasa.

Mheshimiwa Spika, kikwazo kingine ni maji kama nyenzo nyingine ya maendeleo katika jami yetu huko vijijini. Bado vijijini kuna matatizo ya maji na kadhalika kwa hiyo haya nayo yanachelewesha kukua kwa ushirika tunaoujenga. Matatizo haya yakiondolewa ushirika utakwenda kwa kasi sana.

Lingine ni nguvu kazi ya vijana wa kike na wale wa kiume bado hawajaunganishwa, nguvu yao haijaingia katika ushirika tunaoujenga, bado ushirika utakuta ni wazee na watu wazima hivi lakini vijana wa kike na kiume bado hawajawezeshwa kabisa wakachanga nguvu zao ili waweze kujenga shughuli zao kupitia ushirika. Kwa hiyo, ni kikwazo hicho lazima Serikali ijue ili iweze kuweka malengo yake kwa kuwalenga hao na ndio maana unakuta wengine wanakimbilia mijini na kadhalika lakini wakijengewa mazingira ya kuanganisha nguvu zao kupitia ushirika watatulia kule vijijini.

Lingine ni urasimu katika mikopo ya washirika. Washirika wanajiunga wakati fulani wanahitaji mikopo na nini kwa hiyo, urasimu unakuwa mkubwa, safari nyingi hatimaye wanafilisika hata wale washirika kwa sababu ya safari ya kufuatilia mikopo. Kwa hiyo, Serikali ione hilo kwamba ni moja ya kikwazo kinachokatisha tamaa washirika kule waliko.

Mheshimiwa Spika, lingine ni kwamba fursa za washirika zipo wazi kabisa, iko juhudhi, yako maarifa, iko ari na nia lakini tatizo ni kwamba hawajawezeshwa, hizo fursa zao hazijawezeshwa vizuri ili ziweze kufanya kazi vizuri za kujenga Taifa na kuondoa umaskini.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni kwamba Vyama vyta Ushirika ambavyo ni vichanga hufa kwa sababu ya ada kubwa ya ukaguzi. Ada ya ukaguzi ni kubwa, vyama hivi ni vidogo, kwa hiyo, hatimaye vinakufa. Serikali iangalie namna ya kuhuishwa ada ya ukaguzi iwe ya wastani na hasa iangalie vikundi vyta ushirika vinavyokuja vikoje, vina hali gani, hicho ni kikwazo cha kumi.

Kikwazo cha kumi na moja ni kwamba *COASCO* ipewe jukumu zaidi la kufundisha, kuelekeza na kufuatilia utekelezaji wa yale yaliyojitekeza katika ukaguzi badala ya Serikali maana sasa hivi kazi hii inafanywa na Serikali lakini ingefanywa na *COASCO* yenyewe tunaweza tukapiga hatua. Haya ndio mawazo yangu na ndio vikwazo ambavyo katika kufanya utafiti nimeviona.

Mheshimiwa Spika, kikwazo kingine cha kumi na mbili ni kwamba Mrajisi wa Vyama vyta Ushirika naye apewe mamlaka ya kisheria kusimamia Wakaguzi wa Vyama kwa sababu hali iliyoko sasa hivi Mrajisi wa Vyama hana mamlaka makubwa katika kufuatilia na kusimamia ukaguzi katika sheria hii.

Mheshimiwa Spika, kikwazo kingine ambacho ni cha mwisho, ni ushirika wa zamani. Kuna madeni ya ushirika wa zamani katika maeneo mbalimbali pamoja na Mkoa wa Dodoma ni moja ya vikwazo katika kujenga ushirika huu kwa sasa. Mfano mmoja *CRCU* ya Dodoma inadaiwa shilingi milioni .5.5 na Chama cha Msingi cha Ushirika kule Kwadelo, Kondo siku nyingi sana na chanzo chenyewe ni gari la *CRCU* liligonga ghala la Chama cha Ushirika. Kesi hiyo ilifika Mahakamani na hukumu ikatolewa Chama kile cha Msingi kilipwe shilingi milioni 5.5 lakini mpaka leo hakijalipwa. Kwa hiyo, katika Kata ile hata kama tunahamasisha habari ya ushirika wanasesma kwanza walipe deni letu.

Kwa hiyo, ni sehemu ya vikwazo, naomba sana Serikali ilipe maana nasikia wanajiweka tayari wamfikishe mfilisi na Serikali yenyewe Mahakamani. Kwa hiyo, naomba Serikali ikubali kuwalipa hela hizo mambo yaishe wasiende Mahakamani hawa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, hayo ndio sehemu kubwa ya vikwazo katika ushirika wetu ambao tunajenga tunaomba Serikali izingatie na iangalie namna ya kuviondoa. Ushirika ni kitu cha msingi sana na muhimu sana ndio utakaowainua wanyonge vijijini.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi, narudia tena kusema kwamba naunga mkono hoja, sheria ipite ili hoja hii ianze kufanya kazi, ahsante sana. (*Makofî*)

**MHE. SEMINDU K. PAWA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi nichangie Muswada uliopo mbele yetu inaohusu chombo cha udhibiti (*Audit*).

Mheshimiwa Spika, nimekuwa nauliza kwamba hivi chombo kama hiki cha udhibiti nacho hudhibitiwa? Nikasema ni sahihi kweli kwamba nacho hudhibitiwa kwa sababu mdhibiti hudhibitiwa.

Baada ya kuangalia mahesabu ya *COASCO* ya mwaka 2002, 2003 na 2004 nikaona kumbe aliyekagua shirika hili ni *Controller Auditor General* nikaja na usemi unaosema alaah kumbe kitu hakijilindi chenyewe hata nanasi lina miiba kuanzia shina mpaka tunda lakini lazima kuwe na mlinzi wa kuyalinda usitegemee miiba yake tu, huliwa. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, kinachoundwa hapa katika sheria hii ni chombo ambacho kipo tayari kinafanya mabadiliko kutokana na miundo na utaratibu uliofanyika hapo nyuma, kinafanya mageuzi ili kisibaki peke yake. Kwa sababu chombo hiki kimeundwa miaka mingi sana kikishughulikia ushirika peke yake. Ilikuwa changu, changu, chenu chenu. Kwa hiyo, chombo hiki hakiiti watu wengine kuja kuangalia Vyama vya Ushirika ambavyo ni vingi. Kwa taarifa ya Vyama vya Ushirika mpaka imezidiwa ni kwamba Vyama vya Ushirika vya Msingi viko 2,053, vya akiba 480 na kuna vyama vingine vya mchanganyiko viko 322. Kwa hiyo, jumla ya Vyama vya Ushirika ambavyo vinatakiwa vikaguliwe na shirika hili ambalo ni moja vilikuwa 2,852. Hata hivyo, natoa pongezi walifanya ukaguzi kwa mujibu wa Mkaguji Mkuu walipata mafanikio makubwa sana katika kufanya kazi hiyo pamoja na kwamba mabadiliko yalikuwa bado.

Mheshimiwa Spika, yako mabadiliko mengine kwa usimamizi wa Bodi iliyokuwepo na menejimenti ambayo ipo ni kwamba yako mabadiliko makubwa kwa mfano walipata faida katika mwaka 2001/2002 mpaka mwaka 2002/2003 kutoka kiwango cha shilingi milioni 355 mpaka shilingi milioni 433 haya ni mafanikio makubwa sana kwa chombo hiki. Hiyo sio taarifa yangu ni taarifa ya Mkaguji. (*Makofî*)

Lingine ni kwamba chombo hiki tunachokiunda leo ambacho kina mabadiliko ya mageuzi vile vile lazima kinafuata *financial regulations* hivyo kimetambuliwa na *BOT Regulation* kwa mujibu wa *financial regulations* iliyotolewa katika *circular 13* ambazo sitazitaja zote. Vile vile itaingia ndani ya ushindani na wengine.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaingia huko kwenye *tuition* nilitaka kuwaambia Wabunge wenzangu kwamba yako mabadiliko tumeyafanya kwa mfano katika *clause 2(c)* ya *definition, appropriate* tulikuta *pre-cooperative groups* kweli ilikuwa haina *definition* kule ndani nadhani atafanya marekebisho lakini itapatikana kwenye sheria mama ya ushirika. *Cross references* mara nyingi katika sheria naona inaruhusiwa haiwachanganyi kwa sababu wanaangalia sheria zinazohusiana na mambo ambata ya sheria inayokuwemo ndani ya mtiririko wa kutoa maamuzi.

Lingine kuhusu sehemu ya *definition, section 12*, namba (h) tulibadilisha kiwango kile, nashukuru kweli kwa sababu mara nyingi adhabu usiweke kiwango kinachomvutia mtendaji akafanya majoribu, adhabu isiwe majoribu iwe ni matokeo ili mtuhumiwa atoweke baada ya kufanya majoribu atajaribu na majoribu hujaribika. Hivyo basi kwa kutoa shilingi 200,000 kwenda shilingi 2,000,000 ni tishio kwa sababu mara nyingi ikiwa kidogo watu wanakwenda kujaribu na kufanya makosa makusudi na makosa makubwa ya kugushi kwa hiyo lazima kuweka shilingi 2,000,000.

Hapa tumeunga mkono kwenye Kamati na narudia tena iwekwe kwenye *Hansard* kwamba naunga mkono kwa sababu usiweke adhabu za kujaribu watu wakajaribu. Kuna watu watundu sana wanaendelea kwa kutaka kujaribu jaribu wajipatie mapesa kwa hiyo, hii itakuwa imekomoa kabisa. Ndio wanasema sheria kali, sheria haiwi kali, adhabu kali, adhabu imeandikwa tayari utasemaje kali? Adhabu zile zile tunasema atachukuliwa hatua kali, sheria kali au adhabu kali adhabu zimo tayari si kali *unless unaiweka adhabu nyingine ambayo inaiunda pale*. Kwa hiyo, sheria hii sasa ni kali imeandikwa pale pale. (*Kicheko*)

Halafu kwenye upande wa sheria yenyewe kwa kweli imejumuisha mambo mengi kuna *financial references*, kuna mambo ya ushirika, mambo ya mtazamo ya mwongozi, kwa hiyo ni *self contained*.

Kuna wakati niliwaambia kwamba sheria zote zingekuwa *self contained* watu wanaziogopa kuziangalia kwa undani. Usizisome tu au kutaka kuambiwa. Kwa mfano, mtu mmoja alikuwa anakwenda hotelini kwa sababu alikuwa anataka aelezwe eti, baada ya kumwambia naomba vyumba akaamwambiwa kuna vyumba vya aina tatu hapa. Aina gani? Akamwambia kuna *single, double* na *self contained*. Mtu ambaye mwenye falsafa na mtendaji mzuri kama Waziri huyu anayeleta hotuba hii na Wabunge sisi tunafuutilia unasema naomba nikaviona vyumba hivyo. Badala yake akamwambia naomba maelezo akapewa maelezo na yule mama msimamizi wa vile vyumba. Akamwambia *single* ni kitanda kimoja, *double* ni vitanda viwili na *self contained* kila kitu hapo hapo akawa anataka kujua kila kitu hapo hapo, vitu gani hivyo? Akaambiwa kuoga, kulala na choo. Akasema hilo zizi sitaki. Lile neno hapo hapo kwamba unaoga, unalala na choo hapo hapo, kumbe neno hapo hapo ni chumba kizuri amekataa. (*Kicheko*)

Muswada huu Waheshimiwa Wabunge ni *self contained* ambaao una kila kitu hapo hapo, neno hapo hapo maana yake ni kwamba tunaunda chombo cha udhibiti. Pili tunapanua wigo kwamba sasa kinakuwa na fursa na hatua za uwajibikaji zitaongezeka. Halafu tatu sasa itaingia kwenye ushindani.

Sasa naomba niwataje washindani wao sasa kama watakuwa na ubavu basi watajiju kule kule sisi tunapeleka taarifa hiyo. Kwa mujibu wa *International Report* ya *BOT*, ambayo nimeipata kwenye *internet*, Mheshimiwa Spika, sasa hivi natumia *internet*, kwamba kuna washindani wenu wengi ambaao *BOT regulation* imetoea taarifa kwamba mmepewa kibali tayari kwa mujibu wa taarifa ninayoisoma hapa nitamkabidhi Katibu Mkuu na Waziri mtaisoma hii.

Namba moja kwenye *KPMG* ambayo *Managing Director* wake anaitwa *Resident Paterner* ni Nicolus. Kuna mwingine ambaye mtapambana naye ni *Global Accountants Supervisor, Director* wake anaitwa Mngurusi. Kuna kampuni ya ukaguzi inayoitwa *Price Water House and Cooper Lab.* hawa ni watu ambao wameijengwa vizuri sana lakini watu wadogo hawajasambaa katika nchi lakini wana uwezo mkubwa, *Director* ni Mr. Msusa. Kuna *TAC-Associate, MD* wake ni Ndugu Sayore.

Mheshimiwa Spika, hawa watu wenye uwezo na uzoefu na ninyi vile vile mna uwezo na uzoefu kwa hiyo, ila kuwe na udhibiti mzuri katika kupeana kazi wasione tu *COASCO* wanaanza kupitiwa sasa hivi basi wakaanza kuwakanyaga kanya kwamba kufanya wale waliowazoea kwa hiyo natoa tangazo na tamko kwamba wale wote ambao wanatafuta ma-auditors sasa hivi leo tunapitisha sheria ya Muswada wa Sheria *COASCO*, sasa *COASCO* haitashughulikia Ushirika peke yake inatoa fursa katika kuingia ushindani na ni namba 11 kwa mujibu wa *BOT Regulations* kwa sababu wametekeleza majukumu yote ambayo yanaleezwa kwenye ukurasa 13 wa taarifa ya *BOT* wamefuata masharti yote yanayokubalika hii sheria tu inakuja kuweka hapa ili kuridhisha hayo.

Kuna *Bank of Tanzania Act 1995, Bank and Financial Institution 1991, Foreign Exchange Act 2002*, kuna *Banking and Financial Institution Regulation 1997*, kuna *Management Risk Asset* ya 1992 na kuna *regulations* saba zote zimefuatwa na vile vile na nyaraka nyingine na utaratibu wake wa uendeshaji.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo Muswada huu ni mzuri kwa sababu tunakwenda hatua kwa hatua, unaanza moja, mbili, tatu halafu nne. Sasa yale majumuisho tuliyokuwa tumeyafanya katika Bunge hili na katika kumbukumbu zangu tayari tumeshapitisha sheria ya Ushirika, yako matatizo ya kiutendaji ambayo Waheshimiwa Wabunge tunalalamikia kwa kweli watafutwe malaika au nusu malaika kusimamia hili ili kusudi waweze kupambana vizuri.

Kuna Muswada wa Sheria ya Pamba, Sheria ya Miwa, Sheria ya Kahawa, Sheria ya Pareto, Sheria ya Mazao mbalimbali ndipo pale ambapo sheria hizo zitadhibiti mazao hayo na vilevile Sheria za Ushirika zitadhibiti Ushirika. Hii itadhibiti mahesabu kwa sababu ni pamoja na mdhibiti hudhibitiwa kwa hiyo kanuni zote za mahesabu wameweka sawa.

Tumemponeza Mwenyekiti hapa Mheshimiwa Anne Makinda ambaye tulikuwa naye, tulimwita kwenye Kamati yetu alikuwa na majibu ya mkato kama ugali wa hoteli, lakini yenye usahihi. Tulikuwa tunamuuliza maswali lakini alitujibu vizuri sana kwamba chombo kitakuwaje akatupa *vision* tuliokuwa na msimamo tukawa tumepitwa na wakati wenye *vision* hawakuyumba lakini walikuwa na wakati kwa hiyo sisi sasa hivi Kamati yetu imeelimika vya kutosha na hatua kwa hatua tunafanikiwa. Ila tu kwa mfano chombo hiki sasa ni *Auditors* sasa hivi siyo *Fraud Inspectors* kwamba kuna baadhi ya ma-auditors na kwamba *Auditors* ambao *Internal Auditors* wana tabia wanapoambiwa kwenda ku-audit hesabu wanakimbilia kuangalia makasha ya fedha wanasema tupeleke kwenye kasha la fedha, hiyo siyo *auditing*, hiyo ni *inspection* unatafuta silaha za maangamizi kama walivyofanya kule Iraq wanaokimbia kuona mashelfu.

Mheshimiwa Spika, hii ni kuangalia mahesabu na kuangalia uwekaji mzuri wa mahesabu na wale *Internal Auditors* kazi yao ni kuangalia na kuweka sawa mahesabu yao hivyo muhimu kwa *External* kuja kuangalia ili mahesabu yaende sawa. Msigome kwa sababu msije mkafananishwa na wale Mapadri 110 waliambiwa wachore shetani, wakasema hatumjui, wakaambiwa choreni kila mtu afikirie, wakasema kawaida ya picha Mwalimu unachora sisi tunaiga, Mwalimu akasema hapana choreni kama mnavyofikiri, wakamwambia Mwalimu kalamu hatuna, wakapewa kalamu za rangi zote wakamwambia Mwalimu hatuna karasi, wakapewa karatasi ya leo, ya kuchora kesho na keshokutwa.

Mheshimiwa Spika, wakaambiwa choreni sasa, saa tatu, wakaona watumie muda wote, mmoja alikuwa sijui alikumbwa na nini akachukua kalamu akachora akaandika shetani akamrudishia Mwalimu, akaambiwa 100 toka haraka hili jibu lisiliki, akatoka njе akapigiwa makofi na watu wa njе akapata 100. Waliobakia wakachora vizuri baada ya saa tatu wakarudisha picha zikawa nzuri wakapata sifuri wote pamoja na muda mrefu waliotumia, wakaambiwa shetani sio huyu. Alichokosea Mwalimu ni kuwaonyesha picha ile mbaya akawaambia mfano wa kuigwa ni huu hapa, kwa hiyo, ilibidi asubuhi waje na kalamu nyeusi wote kwa sababu ni mfano wa kuigwa waliambiwa leo mnachora picha ya Malaika, wakaanza kuchora kama mwenzao kwa sababu waliambiwa mfano wa kuigwa wakachora picha nyeusi wote. Waliporudisha kwa Mwalimu wakapewa sifuri wote wakaambiwa leo malaika mlitakiwa mchore kama jana, kwa hiyo, akachukuliwa kama Mwalimu yule ni myumbishaji, jana tulichora picha nzuri tukaambiwa tuchore mbaya, leo tunachora mbaya tunaambiwa tuchore nzuri, kwa hiyo, kesho tugome akituambia tunaandika majina yetu wote halafu tunaandika jina na picha halafu tunarudisha vilevile bila kuchora.

Kwa hiyo, mgomo huo kwa kweli ni wana Ushirika wa Tanzania msigome, tokeeni matukio yaliyotokea, walipokuja Mwalimu wao akawaambia leo mnachora picha ya Mungu, wakaandika jina na picha, picha ya Mungu wakaandika majina yao halafu hawakuchora wakarudisha wamegoma. Kwenda kule Mwalimu kawapa 100 akawaambia Mungu hana mfano wa kuigwa wakapata 100 wote ambao hawakuchora.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana naunga mkono hoja hii. (*Makofi*)

**MHE. STEPHEN M. KAZI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie kwenye Muswada ulio mbele yetu.

Kwanza kabla sijachangia ningombwa niungane na Wabunge wenzangu kutoa salaam za rambirambi kwa matukio ya misiba yaliyotupata. Kwanza kwa familia ya Mheshimiwa Balozi Ahmed Hassan Diria, kwa kumpoteza huyu kiongozi na pili naomba nitoe salaam hizohizo kwa familia ya Marehemu Balozi Paul Bomani, nashukuru kwamba nilihudhuria mazishi yake na nina kumbukumbu nzuri ya hali ya huzuni ya familia ilivyokuwa siku hiyo, lakini kwa pamoja nawaombea kwa Mungu aziweke roho zao mahali pema peponi.

Mheshimiwa Spika, kwanza ningeomba niipongeze sana Wizara kwa ubunifu na kwa juhudzi zake za kujaribu kutuweka katika hali ya masahihisho na kuweka juhudzi kubwa za kuimashira ushirika katika nchi zetu. Nampongeza sana Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara kwa mawazo mazuri kama waliyoyafanya ya kutuletea mabadiliko na masahihisho katika Muswada wetu wa Ushirika wa mwaka 1982 kuhusiana na Idara ya Ukaguzi ili kwamba tuweke utaratibu mpya sasa kwa nia ya kuendeleza ushirika katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nikiangalia kwa karibu naona kwamba moja ya masahihisho makubwa, moja ya nguzo za kusimamia Ushirika ambayo ni kubwa ni ukaguzi, kama ukaguzi na mahesabu yanatunzwa, pesa zinatunzwa mahesabu ya pamba hewa yanakwisha basi nina imani kabisa Ushirika utarudi na utakwenda vizuri. Mpaka sasa hivi tukiangalia kumbukumbu bado iko wazi kwetu wote, matatizo ambayo yamejitokeza, tunavyoumwa tukiangalia Ushirika wetu ulivyoharibika haya yote yanatupatia picha ya kutafuta tufanyeje sasa ili tusahihishe mambo yote haya.

Sheria hii ya kuipatia nguzo na marekebisho mapya *COASCO*, kwa kweli mimi naanza kuona ni moja ya njia za kutufikisha mahali pema pa kuweza kuendesha Ushirika wetu vizuri katika nchi yetu hii.

Mimi labda tu ningejaribu kuisema kwamba pamoja na hali ilivyo sasa *COASCO* lazima ieletewe kwamba ina mzigoto mkubwa nchini bado kumbukumbu na picha ya Ushirika ipo pamoja na kufilisiwa na kufutwa na kufungwa vyama vyaa ushirika mbalimbali lakini mabaki yake yapo pale kuurudisha na kuuanzisha ni rahisi sana kama tutajaribu kujenga na kurudisha imani ya wananchi. Moja ya kazi kubwa ambazo *COASCO* sasa inapewa na tunajaribu kuitegemea kwa ukaribu ni kwamba ni lazima ijiandae sasa ijiweke katika hali ya kuridhisha kabisa kwamba inaweka sifa ya kuaminika inapofanya kazi zake katika Vyama vyaa Ushirika vilivyopo hai sasa. Iweze kuleta imani kwa wananchi ili kwamba matatizo tuliyokuwa tunayapata nyuma kule ya ishe.

Mheshimiwa Spika, ukikumbuka najaribu tu kuleta kumbukumbu kama historia kwamba katika zoezi na hali tulivyokuwa tunaendesha Ushirika katika nchi mpaka sasa hivi mambo ambayo yamegusa na kurudisha nyuma maendeleao ya Ushirika ni pamoja na ukaguzi mbaya. Ukaguzi ambao ulikuwa unashirikiana na watu wenye mawazo mabaya, ukaguzi ambao umetuleteleza kabisa kuharibu Ushirika katika nchi yetu, kilichopo sasa ninachojaribu kukiangalia ni juhudzi ya Wizara na juhudzi ya Waziri ni kwamba tubadilishe mindset ya wananchi wetu, tuelewe kwamba Ushirika ni Chombo cha Maendeleo, Ushirika ni Ukombozi katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kama tutauendesha Ushirika vizuri, suala la ushiriki wa wananchi kwa pamoja katika hoja nzima ya kuondoa umaskini utakuwa karibu na wote tutafaidika kama tutashiriki kwa utaratibu wa kuwa na utendaji mzuri katika maeneo mazuri ya Ushirika.

Mheshimiwa Spika, nikiangalia Mwanza kwa mfano bado hali ya Chama cha Ushirika Kikuu cha Nyanza ipo na kinafanya kazi ingawaje kwa matatizo, Shinyanga

*SHIRECU* ipo nayo kwa matatizo lakini nina imani kuna makundi sasa ambayo yanaingia kwa mtindo wa Vyama vya Ushirika vidogovidogo kwa shughuli mbalimbali za kibiashara na kimaendeleo vipo na hivi tu vinaweza vikafanya kazi na kuendelea vizuri kama ukaguzi *COASCO* itafanya kazi zake vizuri katika Taifa letu hili sasa na nina imani kama itafanya kazi vizuri na kujenga imani ya wananchi kujiwekea sifa ya kuaminika basi mimi nina imani kabisa kwamba hali ya Ushirika na Maendeleo ya Ushirika yataanza na tutakwenda vizuri tu na wananchi wako tayari kuona kwamba kama mali yao haikuvurugwa, mali yao haikuharibiwa watashiriki katika Ushirika hawatarudi nyuma hata kidogo.

Labda tu nijielekeze katika Muswada baada ya kusema hayo maneno ya jumla ili tu nijaribu kutoa maelekezo na pia kutoa mchango wangu wa karibu katika suala zima hili la Muswada huu wa *Amendment* au Marekebisho ya Sheria ya Ushirika ambao uko mbele yetu sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, tukiangalia Ibara ya nne kwa mfano tukienda nayo mpaka mwisho na pia na vifungu vingine ambavyo vinaendana na shughuli nzima ya Ushirika kuna maeneo ambayo yamenipa imani ambayo sasa kama yatafanyiwa kazi kwa karibu na Wizara na yatumie yatasaidia sana katika kuimarisha na kuliweka hili Shirika letu la Ukaguzi liwe na nguvu, imara na liweze kufanya kazi yake vizuri kwa wananchi.

Katika kifungu cha 4(1) ukiangalia sehemu ya (b) kwa mfano namna ya kusimamia, hii ni taratibu mpya ambayo imeongezwa katika Muswada pamoja na kukagua lakini Shirika limeombwa pia liweze kuwa na uwezo wa kusimamia kazi za ukaguzi huo.

Mheshimiwa Spika, lakini ukienda mbele katika sehemu ya 3 kifungu kidogo cha (3) hiki ambako inawekewa muda kwamba au *COASCO* inaambiwa na sheria kwamba kila Chama cha Ushirika kiweze kukaguliwa mara moja kila mwaka, sasa hii inawabidi kabisa katika Wizara, inawabidi kabisa ndani ya Shirika lenyewe la *COASCO* waweke utaratibu na *time table* ambayo iko imara kwamba lazima ukaguzi ufanyike kwenye shirika kila mwaka.Ukaguzi ufanyike kwenye kila Chama cha Ushirika kila mwaka, na unapokagua unatoa taarifa hukgui tu na kunyamaza na unapokagua inabidi pia uchukue na stock ya maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, tulikuwa na tatizo kubwa katika historia ya nyuma huko ukiangalia na ndiyo moja ya maeneo ambako Ushirika mwanzo ulivurugika ni suala la pamba hewa, katika *report* kwetu sisi ambao ni washiriki tunakaa tunajua kwamba ndani ya ghal a kuna kilo 1000 za pamba, tunakaa tunajua hivyo kwamba zimo ndani ya ghal a na wakaguzi wanakuja wanakagua, kwa sababu wanakuja bila *time table* wanaweza kuja baada ya miaka miwili au mitatu kukagua unakuta kwamba wanaandkia hivyo hivyo taarifa kwamba kuna kilo 1000 ndani ya ghal a wakati hasa wangechukua *stock* kumbe ziko kilo siyo 1000 ni 600 labda, sasa hii yote inakuwa ni ubadhilifu na uharibifu mkubwa na washiriki wananchi wameumia sana na jambo hili.

Mimi ningeomba Wizara, ningeomba *COASCO* yenewe iwe na mawazo sasa *mindset* yake ijibadilishe iweze kuwa na uaminifu, ijijengee uaminifu, ijijengee sifa ya kuaminika kwa wananchi, inapofanya na kutoa taarifa yake ya ukaguzi basi itoe taarifa sahihi ya hali yenewe halisi waingie kwenye maghala wachambue, wakague na wapime kama ni uzito wajaribu kutoa uzito ambaa unakubalika na walioukuta mle ndani kama kuna mapungufu, kuna ubadhilifu basi upatikane palepale na taarifa zikiwa zinakuja mara moja namna hiyo zitasaidia sana wananchi kusimamia Ushirika wao na imani ya wananchi itarudi na wataanza kushiriki kwa ukaribu katika masuala mazima ya kuendesha Ushirika wao.

Tukiendelea na hali yenewe hiyo ya ndani ya Muswada vifungu vingi vimewekwa sahihi na *Board* imepewa taratibu zake za kufanya kazi na ikaaje *Board* na pia nashukuru kwamba katika hili Waziri amekuwa na mipango ya kisasa hakutaka kurudi nyuma ameeleza kwa uhakika kabisa kwamba ndani ya *Board* ataangalia suala la jinsia kwa karibu kwa hiyo akinamama wasiogope, watashiriki watakuwa ndani ya *Board* nao watatoa maamuzi kwa sababu nao ni washirika wakubwa katika maeneo mbalimbali ambako wanatoka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo hili mimi nalisema na ninajaribu kuieleza Wizara kwa uwazi kabisa ningependa wakati Waziri akitoa maeleo haya ningemuomba ajaribu kunihakikishia kwamba atakuwa anapeleka waraka mara kwa mara wa *ku-update* hii asiiache sheria tukiimaliza leo basi tuiachie hapo, aifuatilie, apeleke, waraka na ajaribu kuifanya ikae *live* na ya kisasa zaidi iende na wakati isichelewe hata kidogo kwa sababu sasa tuna kazi kubwa hii ya kujenga Ushirika, kurudisha Ushirika kwa wananchi wetu na kuhakikisha kwamba Ushirika unaendelea Tanzania kwa sababu ndiyo njia mojawapo kubwa ya kumkomboa Mtanzania wa kiwango chochote kile na kuondoa umaskini kwa ukaribu bila kuhangaika na mambo mengine makubwa hayo.

Mheshimiwa Spika, kingine ambacho ningependa nikiseme hapa ni kwamba katika maagizo ambayo yanatolewa kufuatana na Muswada ulivyokaa ni kwamba Wizara isiishie hapo sasa kwa kweli naisifu sana kwa kuangalia Muswada na kuona kwamba sheria hii imerudi nyuma na kujaribu kuiweka *COASCO* katika hali yake ya sasa.

Mheshimiwa Spika, basi katika kifungu hiki ilichopewa cha 4(c) pamoja na utaratibu wa *consultancy* hiyo *research* hata kama isipofanya yenewe *research* inaweza ika *coo-opt* na kuwakaribisha wengine wa kufanya *research* kuna Chuo cha Ushirika kinaweza kikashiriki pia lakini *I think* maana ya *research* hapa na *consultancy* ina maana ya yenewe kuiweka endelevu isikae ikanyamaza *COASCO* ikatulia hapa tulipoishia leo, tujaribu kuendana na wakati kufuatana na hali halisi ya wananchi wetu wanavyokwenda na hali tuliyonayo ya kila siku ili kwamba mambo haya sasa yatatusaidia sana katika kuweka ushirika wetu na Shirika hili la Ukaguzi liwe imara, liwe na uwezo wa kutosha liweze kupambana na ushindani bila matatizo na kwamba pia lenyewe lionekane ni la kisasa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya nashukuru sana na ninazidi kumshukuru Waziri aendelee na utaratibu huu na mimi pia nasema kwamba naunga hoja

Muswada huu ili kwamba uweze kutusaidia sasa baada ya siku ya leo. Ahsante sana. (*Makofî*)

**MHE. ANNE S. MAKINDA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa kufuatana na kanuni zetu inabidi nieleze kwamba mimi ni Mwenyekiti wa *Board* ya *COASCO* na kanuni inasema kuwa yule Mbunge mwenye *interest* lazima atangaze *interest* zake. Mimi ni Mwenyekiti wa *Board* ya *COASCO*. (*Makofî*)

Baada ya kusema hivyo kwa sababu pia ni mara yangu ya kwanza kuzungumza katika Kikao hiki cha Bunge, naomba pia nitumie nafasi hii kutoa salaam zangu za rambirambi kwa familia ya Marehemu Balozi Ahmed Hassan Diria na familia ya Marehemu Balozi Paul Bomani, hawa wazee wetu kwa kweli walikuwa ni walimu wetu, walikuwa ni watu ambao wamepigania Uhuru lakini walikuwa ni watu kama yalivyooleza magazeti hawakuwa watu wanaojua majivuno wala jambo lingine lolote na walikuwa ni watu ambao sisi tuliweze kujifunza kutoka kwao. Mwenyezi Mungu aziweke Roho zao mahali pema peponi. *Amina*.

La pili naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa kazi zake nzuri katika dhana nzima ya kufufua Ushirika, Mheshimiwa Waziri Balozi George Kahama alikuwa Mwenyekiti wa Kamati iliyoundwa na Mheshimiwa Rais kujaribu kuona matatizo ya Ushirika na hatimaye kufufua Ushirika na kutokana na Kamati ile ndiyo Wizara hii iliundwa na jukumu kubwa la Wizara hii, moja, ni kujaribu kuona kwamba Ushirika unafufuka tena kwa hiyo ameshaleta sheria ya kujaribu kukarabati Sheria ya Ushirika ambayo sisi Bungeni hapa tumeipitisha. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, katika sheria ile ndiyo imeonyesha maeneo mapya ambapo ushirika unawezakuelekea sasa ukiacha matatizo yalikuwa siku za nyuma na katika sheria ile utakuta kwamba Ushirika si lazima uwe ule wa muundo tunaoufahamu sasa, Ushirika umepewa nguvu ya kupanuka katika maeneo mbalimbali, watu kufanya kazi zao katika njia ya Ushirika.

Mheshimiwa Spika, nchi ambayo asilimia kubwa ya watu wanajitegemea na wachache tu ndiyo wako, tunaweza kusema Sekta Rasmi ama Serikalini au kwenye Mashirika ya Umma, waliobaki hawana mali ni maskini na namna maskini anavyowenza kujikomboa ni kuungana pamoja na wenzake na kufanya kazi zilizo halali ili kujiondolea umaskini na kuweza kujulikana au kukubalika katika jamii ambayo inaweza kumfanyia maendeleo kwa mfano mikopo mbalimbali. Huwezi wewe ukaondoka peke yako unasema unataka mkopo, huwezi.

Mheshimiwa Spika, lakini mkijiunga pamoja katika namna ya Ushirika hata uite vikundi vyote ni namna ya Ushirika tu, sasa Waheshimiwa wanaosema kwamba watu sasa wanajiunga katika vikundi mimi nafikiri hiyo ni hatua nzuri. Hata kujungaunga katika vikundi ndiyo tunakwenda huko kwenye Ushirika maana mwisho utasema hiki kikundi nikitaka kwenda kukopo nitaenda kusema hiki kikundi kinaitwa nini, kwa hiyo unaenda kujandikisha kwa jina lolote lile lakini utajiandikisha na huo ndiyo ushirika wenywewe. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, natoa wito kwa kweli kwamba katika hali ya sasa ya utandawazi huwezi ukaondoka peke yako, umetoka kijiji chako huko unasema mimi naenda kukopa huna kitu chochote lakini kumbe ukijiunga katika hicho kikundi kiite kikundi kwa namna yoyote ile unaweza ukafikiriwa vizuri zaidi kuliko ukienda mtu kama mtu mwenyewe.

Katika mantiki zote hizo kumeundwa Ushirika ni imani unatoa imani yako wewe na wewe na mnaambizana tukutane pamoja tufanye shughuli zetu kusudi tuweze kujiendeleza, sasa utakuta katika imani ile mnaweza kupanuka na mkisha panuka sasa ndiyo linakuja tatizo, imani itabakia hivyo hivyo au kutatokea wengine watakuwa wajanja kuliko ninyi mloliojunga pamoja.

Kwa hiyo, suala zima la kuwa na vitabu vilivyoandikwa vizuri maana wanasema mali bila daftari hupotea bila habari, kwa hiyo tutaingiza dhana ya kuwa lazima kile kikundi kiwe na hesabu zake kwamba tumeweka hiki, tumetumia hiki, tumepeata faida hii tunagawana namna gani. Lazima vikundi vile viwe na utaratibu wa kuwa na hesabu zao haitakuwa vikundi mradi kama ilivyokuwa *UPATU* mnapeana mnakumbuka tu kwamba wewe mwezi uliopita ulichukua hiki na wewe mwezi huu sasa lete tupeane. Hapana mwisho lazima kila kikundi kiwe na utaratibu wa hesabu zao.

Kwa hiyo basi, tukiisha kuwa na hesabu haitoshi kuwa na hesabu, inatakiwa zile hesabu zikaguliwe na ziweze kusema kwamba naam, hizi hesabu zimekaguliwa, kama mnakwenda kuomba hela kwenye *bank* mkopo watakuuliza hesabu zako zimekaguliwa? Kwa hiyo, lazima kwanza uwe na hesabu halafu pia zikaguliwe ndivyo unavyokopeshwa.

Sasa mfumo wa nyuma wa Ushirika ule mkubwa tuliokuwa nao amba kama walivoyeleza vizuri wenzangu kwamba ilifika mahali ukawavuruga wananchi, wananchi wakaliwa mali zao na wachache waliokuwa wajanja ni kweli haya yametokea na yalionekana vizuri kwenye Tume kwamba ni kweli kulikuwa wizi mkubwa kwanza Ushirika wenyewe ulikuwa siyo hiari ilikuwa lazima tu ukifika mahali lazima kuwe kuna Ushirika tu, kwa hiyo, ile kutokuwa na uhiari ilikuwa ni rahisi sana kuweka hata watu wasiokuwa waaminifu ndani yake sasa tofauti hii na hiyo ndiyo sheria iliyokuwepo kwamba watu wajunge wenyewe kwa sababu wanayo sababu ya kuijunga pamoja na wanategemea kupata nini katika kuijunga pamoja kwa hiyo kuna *element* kubwa ya hiari na hii element ya hiari kila mtu atachunga mali yake iliyo kuwa ndani ya chombo cha Ushirika kwa hiyo katika mazingira ya sasa ndiyo maana hata sheria hii huwezi kufanya watu wawe hiari kuunda Ushirika halafu uwalazimishe kwamba lazima mtakaguliwa na *COASCO* tu ndiyo maana tena katika sheria ya mabadiliko kuna hiari kwamba *okey* ninyi mmependa kuijunga pamoja basi mnaweza kutafuta chombo kinachokubalika ama kinachoeleweka kwamba kiwakague.

Kwa hiyo, *COASCO* yenyewe siyo kwamba itasema kwa nini mmekaguliwa lakini wataangalia hiki chombo kinachowakagua maana yake nao ukaguzi sasa ni huru, Shirika la Ukaguzi wa Hesabu za Serikali ambaa niliwahi kuwa mfanyakazi wake miaka hiyo ya nyuma sasa nalo limebinafsishwa sasa na lenyewe linafanya ushindani wa kukagua Mashirika yanaomba kukaguluwa na *Audit Cooperation*, lakini zamani

Mashirika yote ya Umma yalikuwa lazima yakaguliwe na *Audit Cooperation* na Idara zote za Serikali ilikuwa lazima zikaguliwe na *Control* na *Audit General*, lakini sasa *Tanzania Audit Cooperation* imebakiza jina lakini haiwajibiki kukagua mashirika yote ya Umma yaliyobaki. Wao pia wanaweza kutafuta mtu yelete wa kuwakagua pamoja na *COASCO* wanaweza kukagua hayo mashirika. Pamoja na *COASCO* wanaweza kukagua hayo Mashirika kama watu watasema *COASCO* iwakague.

Hivyo hivyo *COASCO*, Vyama vya Ushirika havilazimiki kwamba lazima kwa sababu ni chama cha Ushirika lazima kikaguliwe na *COASCO* hailazimiki, wanaweza kumchukua mtu yelete ambaye anaweza kuwakagua lakini historia Wizara itajua je kwamba hili Shirika linalokagua kweli ni *genuine* maana kuna *auditors* ambao siyo *genuine* pia kama walivyo vyombo vingine siyo *genuine* kwa hiyo, inatakiwa hii inasimamia kwamba kuna hawa watu wanaokagua ni *genuine*. Kwa hiyo, ndiyo sababu ya kusema unadhibiti lakini *COASCO* haihitajiki siyo lazima Chama cha Ushirika kikaguliwe na *COASCO*.

Kwa misingi hiyo hiyo imeonekana kwamba kama sheria hii tunayotaka kuirekebisha ilikuwa inasema wenyewe ndiyo watakagua Vyama vya Ushirika sasa kama walivyosema vingine Vyama vya Ushirika asilimia kubwa vingine vimesinzia, vingine vimekuwa kwa hiyo ukisema *COASCO* iendelee kukagua Vyama vya Ushirika kama ilivyo sheria tunayotaka kurekebisha basi moja kwa moja *COASCO* wenyewe lazima ife, sababu watakuwa hawako wakuwakagua. Lakini uzuri ni kwamba sasa hivi kunajitokeza vikundi na watu wa aina mbalimbali wanaojunga katika Ushirika kwa hiyo hao watasema sisi tunataka *COASCO* itukague na *COASCO* sasa ili iweze kujitangaza na wenyewe kwamba ipo ndiyo inaunda kitengo cha pili cha utafiti kusudi *COASCO* kitafue tunakokwenda yaani dunia inakwendaje, watu wanafanya nini na huko sisi tunaweza kusaidia viyi kwa hiyo na wenyewe lazima wajitangaze wajiuze kwamba na sisi tunaweza kukagua, kukusaidia wewe uweke hesabu zako vizuri ama uangalie *business* yako uendelee na uende namna gani kwa hiyo, inajitangaza kupitia utafiti kutokana na mafunzo wanayopata kutoka kwenye kukagua Ushirika ama waliokwishapata kukagua Ushirika utumike katika kuweza kuboresha Ushirika huu sasa ufananaje katika mazingira ya sasa ndiyo maana ya kitengo kile kinachosemwa cha utafiti.

Hivyo hivyo katika kufanya kazi zake *COASCO* pia kuna Idara ya Ushirika katika Wizara, Idara ya Ushirika ni kama Mlezi wa Vyama vya Ushirika katika ngazi hiyo wao si wakaguzi, wao ni walezi wa Ushirika katika maeneo wanayohusika lakini Mkaguzi anayetambulika kisheria kwamba akikagua na akapeleka hesabu kwenye chombo chochote cha kutoa fedha ni Mkaguzi wa Nje, awe *COASCO* au hao wengine watakaona kwamba wanafaa. Lakini Idara ya Ushirika wanaangalia kama Ushirika unafuata, taratibu zinazohusika, unaundwa sawasawa na kuona kwamba unaweza kusema kwamba wanafanya pia kazi ya Ukaguzi wa ndani ili kuona kuwa shughuli nzima za Ushirika zinaendelea vizuri.

Kwa hiyo, mimi nasema kwamba *COASCO* hii iliyokuwepo iliundwa kwa sheria ya mwaka 1982 Namba 15 hii tunayoifanya marekebisho ilianza kufanya kazi mwaka 1985 ikiwa na jukumu moja la kukagua Vyama vya Ushirika vilivyokuwepo kwa hiyo

tulikwenda kwa urahisi tu Vyama vya Ushirika vilikuwepo na pesa zilikuwepo kwa hiyo *COASCO* ikaneemeka sana katika mfumo ule wa kukagua Ushirika kwa sababu na pesa zilikuwepo. Baada ya mabadiliko ya kwamba Vyama vya Ushirika vimeanza kufa Shirika lenyewe *COASCO* linadai vyama vya Ushirika zaidi ya bilioni 1.9 na hatujui kama hizo pesa zitapatikana kwa sababu Vyama vyenyewe havipo.

Mheshimiwa Spika, lakini kibaya zaidi ni kwamba ule utaalam wa shirika ulikuwa kiasi fulani haupo, kushindana na mashirika ya ukaguzi ya sasa kwa *COASCO* kwa miaka kama mitano iliyopita ilikuwa haiwezekani maana mpaka mwaka 2000 kulikuwa na wataalam, *professional auditors* wawili tu. Kwa hiyo, ilikuwa kama mwishoni kama tungeendelea hivyo hivyo ingekuwa nayo imefutika *ki-profession*. Kwa hiyo, sasa hivi tumeajiri wataalam wa ukaguzi karibu 20 ndio maana Mheshimiwa Semindu Pawa anasema hata Benki Kuu tumeweza kupata leseni ya kukagua mashirika ya fedha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika biashara ya ku-modernize *COASCO* ndio unaanza kupata wale waliokuwepo pale maana yake wengine hawawezi kusoma wengine ni kwamba sasa inabidi waachie njia, hawa lazima watalalamika, lakini ni lazima *COASCO* liwe shirika la kitaalam, liwe shirika la kisasa, kwa hiyo, tunamshukuru Mheshimiwa Waziri ametusaidia sana hivi tuna *computerized*. *COASCO* yetu ni *computerize* kuna *computer*, magari ya kutosha na sasa hivi ukaguzi wake utakwenda kisasa.

Sasa katika biashara hiyo waliokuwepo lazima wataleta kelele kama hizi unazoziona. Mimi naona sasa zimepungua sana nadhani baada ya muda mfupi zitaisha. Kwa sababu watasema *Manager* hafai afanye nini kwa sababu anakwambia wewe kasome, hutaki. Sasa mwenzengu kama mimi kusoma siweze sasa atafanya nini itabidi kuachia ngazi hilo ndio tatizo. Lakini nadhani *COASCO* litakuwa *one of the best* Shirika na litafanya kazi ya kukagua vijijini kwa sababu Mashirika haya mengine hayana uzoefu wa kukagua vijijini na wala hawaendi vijijini. Kwa sababu kwenda vijijini nako ni gharama. Kwa hiyo, atakayekwenda kwa urahisi vijijini ni *COASCO* kwa sababu ana uzoefu wa kwenda vijijini. Kwa hiyo, mimi naamini kabisa *COASCO* ndio mkombozi wa Ushirika na itashiriki katika kufufua Ushirika kama ilivyo dhana ya Serikali na nchi.

Mheshimiwa Spika, naomba niunge mkono hoja hii. (*Makofii*)

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. KHAMIS AWESU ABOUD:** Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote.

Kwanza, napendekeza bodi zinapoundwa ziangalie zaidi wakulima wanaohusika na mazao husika kama ni pamba wawemo watu wanaolima pamba wakiwemo na wawakilishi wa wananchi yaani Waheshimiwa Wabunge, wanawake na mtaalam wa Wizara, makundi hayo ni muhimu sana.

Pili, vikundi vyatya Ushirika vya aina mbalimbali wafanyiwe semina na mafunzo kuhusu umuhimu wa Ushirika wao badala ya kuwaachia wanaushirika kuendesha Ushirika wao kwa kubahatisha.

Tatu, jambo lingine ambalo limejitokeza ni ukosefu wa masoko ya kuuzia bidhaa za wanaushirika, mfano wakati wa mazao ya wanaushirika yanapopatikana wanabaki na mazao yao, hivyo hawajui wauze wapi ni vizuri Wizara iwe na utaratibu maalum wa kutafuta soko la kuuzia bidhaa zao.

Nne, Wataalam wa Ushirika kutoka ofisini ni lazima kwanza wajue vikundi vyote vyatya Ushirika ili wakaguliwe na kupewa maelezo ya mara kwa mara yatakayowafanya wanaushirika kupata moyo wa kuendesha Mashirika hayo.

**MHE. PAUL E. NTWINA:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kuchukua nafasi hii kwa kuchangia machache. Kwa sheria hii ya kuona *COASCO* wamepewa sasa nguvu kufuata misingi ya kusimamia kutekeleza maadili ya Ushirika.

Moja, kwa sheria yenyewe mimi sina matatizo ingawa bado kunatakiwa kuwepo na ushirikiano katika kuanzisha Ushirika ambao kwa sasa umekuwa katika hali ya kuzorota. Pengine sasa Wizara ingeweka nguvu kuimarisha Vyama vya Msingi ndipo tupate Ushirika ulio bora zaidi.

Pili, mali nyingi za Ushirika zilizopo ni chache pale Ushirika ulipokufa sasa hakuna wa kuvinusuru, aidha, Wizara au Mrajisi wa Vyama, kusimamia pengine sheria nzima ingeangaliwa upya.

Tatu, yapo madeni ambayo ingekuwa vizuri madeni yaendelee kuwepo kwa mfilisi naye aangalie jinsi ya kuyalipa. Bado wanaushirika wanaamini Ushirika utalipwa. Sasa ni wakati muafaka wa kufufua Vyama vya Ushirika viliyvo imara na bora. Mfano mzuri ni wa jinsi kuwepo kwa *SACCOS* au Vyama vingi vya kuweka na kukopa kumekuwa na ukimya sana na kufufua Vyama vya Ushirika lakini vinaweza kuboreshwa na kuwa na udhibiti na uongozi bora kwa kusimamiwa na *COASCO*.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. IRENEUS N. NGWATURA:** Mheshimiwa Spika, sheria hii ni ya zamani sana, ilitungwa takriban miaka 27 iliyopita. Ni sheria iliyopitishwa wakati wa Ushirika hodhi au Ushirika wa dola badala ya wanachama. Kwa hiyo, kuleta sheria viraka haitasaidia Ushirika uende na hali ya mabadiliko ya mfumo wa soko huria. Nashauri Serikali itazame upya mfumo mzima wa Ushirika, ikiwemo kufuta na kutunga upya sheria ya Ushirika pamoja na usimamiaji madhubuti.

Mheshimiwa Spika, wakati namwuliza Mheshimiwa Waziri swali namba 50 la tarehe 18 Aprili, 2005, kuhusu Hisa za Wakulima wa kahawa wa Mbinga, Mheshimiwa Naibu Waziri katika swali la nyongeza alijibu kuwa mfilisi anapaswa kutunza mali za chama kilichofilisiwa pamoja na fedha zinazotokana na mauzo ya mali

au gawio kutokana na Hisa, hususan gawio analopaswa kulipwa kutokana na kiwanda cha kukoboa kahawa ambacho kinatoa faida.

Ningependa Serikali ikakague mali zote za iliyokuwa *MBICU* pamoja na kupata ukweli kuhusu jinsi mali hiyo inavyohujumiwa. Ningependa nifahamu pia kama marekebisho ya sheria hii yanatoa kipengele cha kusimamia na kukagua mahesabu ya Kampuni au Vyama vya Ushirika vinavyokuwa chini ya mfilisi, vinginevyo panaweza kujitokeza Makampuni au Vyama vya Ushirika chini ya kivuli cha mfilisi kwa lengo la kujinufaisha kwa baadhi ya watu binafsi.

Mwisho, naunga mkono mabadiliko hayo ya sheria, kwa imani kwamba hatua hii ni ya muda mfupi wakati tunasubiri sheria itakayokuwa na mtiririko unaokidhi mahitaji ya Ushirika ndani ya mfumo wa ushindani wa soko huru.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua nafasi hii niweze kwanza kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Ushirika na Masoko, Naibu Waziri na Watendaji wake kwa usimamizi mzuri wa mpango wa kufufua Ushirika nchini. Katika mchango wangu juu ya mapendekezo ya marekebisho ya sheria husika ningependa kueleza yafuatayo:-

Kutokana na wengi kudhani kwamba *COASCO* ni chombo cha kufanya ukaguzi na kupeleka wahalifu Mahakamani ni vyema wananchi wakafahamu vizuri majukumu makuu ya *COASCO* kuwa ni kufanya ukaguzi wa hali ya vitabu vya Ushirika ili kuona kama uwekaji wa vitabu unafuata kanuni za uhasibu.

Katika kutekeleza jukumu hilo *COASCO* itaweza kugundua mapungufu juu ya utunzaji wa kumbukumbu kama upo, usahihi wa kumbukumbu zenyewe. Pia wataweza kubaini dosari za utoaji na upokeaji wa fedha za washirika na wateja wake, udanganyifu wa upokeaji mali za Ushirika na kuthibitisha hali halisi ya faida au hasara ndani ya Ushirika wenyewe. Kwa kuwa mwenye mali ni Ushirika wenyewe, ndio sababu taarifa za ukaguzi toka *COASCO* zitaelekezwa kwa viongozi wakuu wa Ushirika na hivyo maamuzi na jukumu la kuchukua hatua dhidi ya walioonekana na mapungufu linabaki mikononi mwa uongozi wa Ushirika wenyewe.

Mheshimiwa Spika, hata kama ndani ya sheria hii *COASCO* itapewa jukumu la ziada la kufikisha Mahakamani kesi dhidi ya wanaobainika kutumia vibaya mali za Ushirika bado mlalamikaji mkuu katika kesi za aina hiyo ni Ushirika wenyewe. Kutokana na taarifa za ukaguzi *COASCO* itakuwa shahidi mkuu wa kusaidia kuthibitisha Mahakamani jinsi mapungufu yalivyobainika na kuonyesha vielelezo.

Mheshimiwa Spika, kwa msingi huo ni vizuri wananchi wakapewa elimu juu ya majukumu ya chombo hiki cha ukaguzi na nia ya sasa ya Serikali kukiimarishe ili kiweze kuongeza ufanisi katika mazingira ya soko huria ambapo Vyama vya Ushirika vyenye uwezo vinaweza kutumia wakaguzi wa mahesabu huru au binafsi nje ya huduma za chombo hiki cha Ushirika.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, wote wale waliojiandikisha kuchangia Muswada huu wamepata nafasi waliokuwepo ndani ya ukumbi kwa hiyo kama taratibu zetu za kawaida zilivyo sasa tutampa Mheshimiwa Mto Hoja nafasi ya kipindi hiki cha mapumziko ili aandae majibu yake akishauriana na wataalamu wake halafu tukamwita tutakaporudi saa kumi na moja. Lakini niseme kwamba kutokana na maombi ya kuchangia Muswada unaofuata wa *Warehouse Receipt* yamekuwa mengi. Kwa hiyo, Muswada huu utakapokamilika, tutamwita Waziri asome awasilishe Muswada unaofuata ili tutumie muda wetu vizuri. Kwa sababu lengo letu ni kwamba Muswada huo wa pili nao ukamilike kesho halafu kesho kutwa tufanye maazimio ya Serikali.

Kwa hiyo, wale walioomba kuchangia Muswada unafuata ni vizuri wawepo kipindi cha mchana kwa sababu Mjadala utaanza. Baada ya maelezo haya, sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi saa kumi na moja jioni.

(*Saa 06:30 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni*)

(*Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia*)

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Juma J. Akukweti) Alikalia Kiti*

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kwanza nikushukuru sana kwa kunipatia fursa hii nami niweze kuchangia hoja hii ya marekebisho ya Sheria yetu ya Shirika la Ugaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (*COASCO*) ambao umetolewa leo asubuhi. Lakini pengine kwa sababu na mimi ni mara yangu ya kwanza kusimama hapa kwa kutoa hotuba niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu waliotangulia kusimama hapa na kusema, kutoa salaam za rambirambi kwa vifo vya viongozi wenzetu waliotangulia mbele ya haki Mheshimiwa Balozi Ahmed Hassan Diria, aliyekuwa Mbunge wa Rahaleo pamoja na Mheshimiwa Balozi Paul Bomani, aliyekuwa Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Muasisi wa Ushirika hapa nchini. Napenda kuziombea roho zao kwa Mwenyezi Mungu aziweke mahali pema peponi. *Amina.*

Mheshimiwa Naibu Spika, pengine napenda tu kusema kwamba nasimama hapa kuchangia Muswada huu kwa kusaidia kutoa maelezo ya hoja mbalimbali ambazo zilitolewa na Waheshimiwa Wabunge lakini nataka nitangulie kusema kwamba nauunga mkono Muswada huu. Basi niwaombe nanyi wenzangu Waheshimiwa Wabunge wote tuungane katika kuunga mkono ili marekebisho ya Sheria hii yaweze kuanza kufanya kazi na hatimaye kutimiza kile ambacho Serikali imekusudia kufanya katika kuimarisha ushirika nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wote ambao wamezungumza asubuhi hii wametujenga sana kwa kutupa moyo kwa michango yao mizuri ambayo kusema kweli naishukuru sana. Kwa mwelekeo huo sisi tuna matumaini kabisa kabisa kwamba yale yote ambayo wameyaeleza tutayafanya kazi kwa ujumla. Napenda

niwashukuru lakini Mheshimiwa mtoa hoja Mheshimiwa Waziri atakaposimama hapa atawatambua kwa heshima mmoja mmoja ili kutambua mchango wao, lakini napenda itoshe tu kwamba wametupa michango mizuri ambayo tutaendelea kuitumia na hatimaye katika utekelezaji wetu kwa kuisimamia hii sheria tuweze kushirikiana nao kwa pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pengine kipekee basi nimshukuru sana Mheshimiwa Talala Mbise, Mbunge wa Arumeru Mashariki, kwa kutushukuru sisi kama Wizara na Serikali kwa ujumla kwa kazi nzuri ambayo wameitambua kule Arumeru kwa soko lao hilo ambalo lilikuwa na matatizo siku nyingi na sisi tunashukuru kwamba wametambua, soko lile limetengenezwa, sasa limekuwa katika hali nzuri. Kwa hiyo, sisi tunarudisha ahsante hiyo ambayo ametupa na tunataka tuwaahidi kwamba tutaendelea kushirikiana nao katika kusaidiana katika yale yote ambayo yatakuwa yanahitaji usimamizi na utekelezaji wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, pengine sasa nijielekeze katika baadhi ya michango ambayo imetolewa na Waheshimiwa Wabunge kwa kufuata vipengele mbalimbali ambavyo vinahitaji tuvitolee majibu. Nianze na mzungumzaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Aisha Magina, ambaye katika mchango wake pamoja na kwamba hakuunga mkono moja kwa moja, lakini ilionyesha waziwazi kwamba alikuwa na matatizo ya vipengele fulani fulani ambavyo kwa mantiki yake kama vingefafanuliwa basi aliunga mkono Muswada huu. Hiyo ilikuwa inahusu maneno ya tafsiri yaliyopo kwenye sheria iliyokwishatungwa na Bunge kwamba sasa wanasema uende ukaangalie sheria nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, maneno ya tafsiri yaliyopo kwenye sheria iliyokwishatungwa na Bunge endapo yatatumika katika sheria nyingine inayotungwa baadaye, utaratibu wa marejeo ndio unaotumika na sababu ya utaratibu huo ni kurudia au kuepusha kuwepo kwa mgongano wa tafsiri ya maneno yanayofanana. Kwa hiyo, hapa ye ye alitoa mfano, kwa mfano wa neno *Aper* ambapo tumesema kwamba limefafanuliwa kwenye sheria ya Ushirika na maneno mengine ambayo tumeyaeleza kwamba yapo katika sheria nyingine. Sasa ye ye alikuwa anapendekeza kwamba tuyarudie tena katika kutoa maelezo katika ufanuzi. Lakini maelezo yake ni hayo kwamba, ndio utaratibu unaotumika na inaepusha migongano kama tutatoa tafsiri nyingi nyingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ilijojiteza ambayo ilizungumziwa na wachangiaji wawili amba ni Mheshimiwa Talala Mbise na Mheshimiwa Edson Halinga, ilikuwa inahusu uwezo wa Waziri kuwa na mamlaka ya mwisho katika usimamizi wa shughuli za sheria hii. Waheshimiwa Wabunge walikuwa wanaona kwamba pengine si vema Mheshimiwa Waziri kupewa mamlaka ya mwisho katika kusimamia utekelezaji. Hapa sisi tunasema kwamba Waziri ndiye mwenye dhamana ya shughuli zote za ushirika pamoja na vyombo vyote vinavyohusika na masuala ya ushirika ikiwa ni pamoja na Shirika la *COASCO* ambalo sasa hivi sheria yake tunaifanyia marekebisho na dhamana hiyo kapewa na Rais wakati wa kuunda Serikali. Licha ya kutoa miongozo ya kisera Waziri pia anawajibika kwa wananchi kipitia Bunge na kwa sababu hiyo lazima awe na madaraka makubwa kumwezesha kuagiza, kutoa miongozo na kusimamia shughuli zote za ushirika. Ndio kazi ya Serikali na maamuzi ya Waziri lazima yawe ya mwisho na endapo ataamua vibaya basi atawajibika katika Bunge. Katika hili tulitaka tueleze tu

kwamba, hata sheria nyingi zinaelekeza hivyo katika utaratibu huu tuliusema hapa ili kuepusha kuwa na milolongo ya mabishano yasiyokwisha. Vinginevyo tukiachia tu kwamba sasa kila mtu akawa anahoji kila hatua inayokwenda itafika mahali hamtatekeleza shughuli. Kwa hiyo, inakuwa ni vizuri basi ifike mahali uamuzi utakapokuwa umetolewa wa maelekezo basi wahusika wengine wote waendelee na utekelezaji huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kabla sijaondoka katika eneo hilo, Waheshimiwa hawa wawili Mheshimiwa Talala Mbise na Mheshimiwa Edson Halinga vile vile walikuwa wamejaribu kuelezea juu ya kwamba, pengine tunaleta marekebisho haya ya sheria vipande vipande na wakawa wanashauri kwamba ingekuwa ni vizuri sheria au kama tunaleta hapa jambo tuliletatikatika ujumla wake. Lakini mimi nataka niseme kwamba katika hili si kipande hata kidogo isipokuwa ni utekelezaji wa yale maboresho ya ujumla. Kama Waheshimiwa Wabunge watakavyokumbuka tumeanzia mbali kidogo kama alivyooleza Mheshimiwa Mama Anne Makinda asubuhi kwamba kulikuwa na Kamati ile ya Mheshimiwa Rais ambayo ilipewa majukumu ya kuangalia matatizo ya ushirika nchini. Kamati ile ilitoka na mapendekezo na mapendekezo yale yaliyotoka ndio yaliwezesha Serikali kuunda Wizara, lakini baada ya Wizara kuanza kazi vitu kadhaa vimeshajitokeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza tulianza na kuandaa sera ambayo yalikuwa ndio maelekezo ya ujumla ya kwamba sasa ushirika uendeshwe kwa utaratibu upi, lakini katika sera tukawekea mfumo wa sheria ambayo ilipitishwa hapa Bungeni ya ujumla wake vile vile ya maelekezo.

Lakini vile vile kutokana na sheria hiyo tumeandaa kwa ujumla wake *cooperative reforms* yaani mageuzi katika ushirika. Sasa kutokana na hayo ndio unakuta kwamba baadhi ya vitu ambavyo vinatakiwa sasa vifuate sera na sheria na hizo *reforms* ni lazima navyo vifanane fanane na ndio maana sasa tunakuja na mapendekezo ya kurekebisha sheria ili ifanane na mlolongo huo wa kufanya maboresho ya jumla. Kwa hiyo, si vipande vipande kama ambavyo walikuwa wamedai Waheshimiwa Wabunge bali ni utekelezaji wa maboresho ya jumla kama ambavyo nimekwishaeleza hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ipo hoja pia ambayo Waheshimiwa Wabunge Mheshimiwa Talala Mbise tena, Mheshimiwa Jacob Shibili, Mheshimiwa Anne Makinda na Mheshimiwa Stephen Kazi, wameieleza kuhusiana na COASCO kujihusisha na shughuli za utafiti yaani research na ushauri na uelekezi. Ushauri hapa ilikuwa kwamba pengine ingekuwa ni vizuri shughuli hii ya ushauri, utafiti ikaachiwa chombo ambacho tumeshakipa hadhi kubwa sasa hivi Chuo chetu cha Ushirika ambacho sasa hivi kimekuwa Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika na Stadi za Biashara. Lakini ninachosema tu ni kwamba, kazi hii ya ushauri na uelekezi ambayo tunialekeza katika shirika hili ni ile ambayo inahusiana na jukumu linalohusu utafiti na ushauri katika kuboresha ufanisi wa kazi hizo za uhasibu, lakini zile nyingine za ujumla wake zitaendelea kufanywa na Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vile vile kwa sababu vyombo hivi viwili vyote vinafanya kazi vikilenga sekta moja vitafanya kazi kwa ushirikiano. Kwa vyovyote vile

haiwezekani kwamba utafiti ukafanywa mathalan na *COASCO* ikapata matokeo ambayo hatima yake pengine yatahitaji yatolewe sasa mafunzo. Kwa hiyo, tunasema kwamba msisitizo wa utafiti kwa upande wa *COASCO* unajielekeza zaidi kwenye suala la ukaguzi wa Vyama vya Ushirika. Kwa maana hiyo Chuo Kikuu cha Ushirika kitaendelea na jukumu lake la utafiti na ushauri elekezi kwa ujumla kwa Vyama vya Ushirika.

Aidha, *COASCO* kwa kushiriki katika utafiti na ushauri itaweza kuboresha ufanisi wake wa kazi kuhimili ushindani na kwenda na wakati. Kwa hiyo, katika hii nadhani lengo letu lilikuwa ndio hilo na nadhani kazi hii ikifanywa kwa ufanisi mzuri Vyama vyetu vya Ushirika na Ushirika kwa ujumla unaweza ukaboreka.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine iliyojitekeza hapa ilikuwa ni kucheleweshwa kwa ukaguzi wa Vyama vya Ushirika. Wachangiaji katika hili walikuwa ni Mheshimiwa John Singo na Mheshimiwa Mama Anne Makinda alieleza kusema kweli sababu zaidi ambazo zilikuwa zimejitekeza na mimi nataka tu niongezee kwamba, zipo sababu nyingi zinazochangia kucheleweshwa kwa ukaguzi ikiwa ni pamoja na mambo yaliyo nje ya uwezo wa *COASCO* kama vile kutotunza vitabu na kumbukumbu ipasavyo, waandishi wa vitabu kubadilishwa mara kwa mara.

Kwa hiyo, haya yote yanababisha ukaguzi kuchelewa, lakini juhudzi za kutoa elimu kwa watendaji wa Vyama vya Ushirika na Mrajisi akishirikiana na Chuo Kikuu Kishiriki cha Moshi na *COASCO* zinaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuna sababu zilizo ndani ya Shirika kama uchache wa wakaguzi na nyenzo. Shirika kwa kushirikiana na Wizara limeendelea kuboresha utendaji wa kazi katika shirika na kama ilivyoelezwa asubuhi, sasa hivi viwango vya wataalam wetu katika shirika hili vimebadilika sana, walikuwa hawana wataalam wa ngazi ya juu ile inayotakiwa kwa mujibu wa Sheria ya Wahasibu na Wakaguzi. Sasa hivi idadi hiyo imepanda kutoka watumishi wawili waliokuwepo hadi kufikia zaidi ya kumi na wanaendelea kuongezeka.

Kwa hiyo, kwa zile sababu ambazo zipo ndani ya uwezo wa shirika na ndani ya uwezo wa Serikali hizo zitaendelea kushughulikiwa lakini kwa yale ambayo yako nje ya uwezo kama haya ya kwamba labda Watumishi katika Vyama vya Ushirika wanahamishwa hamishwa bila utaratibu na wakati mwingine vitabu haviandikwi sawasawa, ndio hapo hoja sasa ya uelekezi inapojitekeza kwamba kama vitabu haviandikwi kwa utaratibu mzuri, baada ya kugundua matatizo kama hayo basi hoja ya ushauri na uelekezi inapata nafasi yake ili kuweza kuboresha kazi hiyo ya ukaguzi iweze kwenda vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ambayo imejitekeza ilikuwa ni juu ya taarifa zinazotolewa na hili kalizungumzia nadhani Mheshimiwa Edson Halinga ya kwamba utaratibu wa ukaguzi wa Vyama vya Ushirika unapofanyika wanaopewa taarifa ni wanachama kupitia Mkutano Mkuu na baadaye wakaguzi hawa wanakuwa hawana hata mamlaka ya kushtaki. Kwa hiyo, ye ye alikuwa anapendekeza kwamba kwanini wakaguzi wasipewe mamlaka ya kushtaki.

Mheshimiwa Naibu Spika na Bunge lako Tukufu kama mtakavyokumbuka kwa sheria ile kuu ambayo imepitishwa na Bunge hili Tukufu ile Sheria ya Ushirika, kuna kipengele ambacho kimetoa nafasi kwa wale tunaowaita *Special Prosecutors* yaani Waendesha Mashtaka mahsusni ambao watakuwa wanasmamia Vyama vya Ushirika. Kwa hali hiyo pendekezo lake nadhani kwa kweli lilikuwa linalenga huko kwamba ili kusiwe na ucheleweshaji wa kuchukua hatua endapo kutakuwa kumetokea na ubadhirifu basi wakaguzi waweze kutoa taarifa na hawa *Special Prosecutors* waweze kushughulikia hizi kesi ili kuweza kuharakisha kesi hizi kule Mahakamani kupeukana na mapungufu yaliyopo sasa hivi. Lakini si hivyo tu sheria ile vile vile ina kipengele ambacho kinamruhusu Mrajisi kutoa *surcharge* kwa watu ambao wanafanya ubadhirifu ndani ya Vyama vya Ushirika, kama mtu amebainika kwamba amefanya ubadhirifu ndani ya Chama cha Ushirika Mrajisi ana mamlaka ya kuamuru watu hawa wafuatiliwe na kuweza kufidia hasara waliyoipata.

Kwa hiyo, kusema ukweli haya yote yamezingatiwa katika Sheria pamoja na kwamba hayakujitokeza katika sheria hii lakini kwa sheria ile ambayo ndio ya maboresho ya jumla yamezingatiwa. Kwa hali hiyo tusingeweza tena kuiandika huku kwa sababu makusudio ya sheria hii ni kujaribu tu kurekebisha vile vipengele ambavyo vitatuwezesha kufanya kazi kwa uhakika zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ipo hoja pia ya kukaguliwa kwa chama kilichokuwa chini ya ufilisi na hoja hii waliitoa Mheshimiwa Ireneus Ngwatura na Mheshimiwa Paul Ntwina, ambao walitaka maelezo kwamba je, itakuwaje kwa chama ambacho kipo chini ya mufilisi, utaratibu wa kukagua utakuwaje? Maelezo ambayo tunayotaka kutoa hapa ni kwamba sheria ya Ushirika ya mwaka 2003, kifungu 103, kifungu kidogo cha (i) na (f) cha sheria ya Vyama vya Ushirika inaruhusu Vyama vya namna hiyo kukaguliwa kufuatia maelekezo ya Mrajisi. Kwa maana hiyo, ukaguzi huu unaweza kufanywa na COASCO au shirika lingine lolote ambalo litakuwa limechaguliwa. Kwa hiyo, chama kikishakuwa chini ya mfilisi sheria inatoa nafasi kuendelea kukaguliwa pia na kuweza kutolewa taarifa kama itakavyoonekana inafaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ilijitokeza hapa hoja ya muundo wa Bodi. Hii ilitolewa na Mheshimiwa Jacob Shibili na Mheshimiwa Khamis Awesu Aboud. Kipekee Mheshimiwa Jacob Shibili, alikuwa anapendekeza kwamba ule muundo wa Bodi na akapendekeza kwamba baadhi ya wajumbe wengine pengine walikuwa hawahitajiki na alikwenda moja kwa moja kusema kwa mfano Mkuu wa Chuo Kikuu Kishiriki cha Moshi kwa nini anakuwa mjambe, pale anafanya nini?

Nimekwishaeleza kwamba vyombo hivi vyote vinalenga katika kusimamia sekta ya ushirika na kwa hiyo vinategemeana na kama tulivoona kwamba katika shirika hili kunakuwa na kazi ile ya utafiti ya ushauri elekezi na hizi ndio kazi zinazofanywa vile vile na Chuo cha Ushirika. Kwa hiyo, kwa taaluma ile tunadhani kwamba itakuwa ni vizuri kuwe na ushirikiano na ushirikiano huo unaweza kufanywa kwa njia bora zaidi kama tutamshirikisha Mkuu wa Chuo hiki kuwa mmoja wa wajumbe katika Bodi ya Wakurugenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile alitaja kazi ya Kamishna wa Bajeti, itakumbukwa kwamba *COASCO* ni Shirika la Serikali ambalo linamilikiwa na Serikali na kwa hiyo hata fedha zake zinatolewa kutoka kwenye bajeti ya Serikali. Kama mnavyofahamu Waheshimiwa Wabunge kwamba mtoa fedha au mtu mwenye maslahi ya Shirika hilo ni chombo kinachotoa fedha. Kwa hiyo, ndio maana tunamweka Kamishna wa Bajeti kuwa ndani ya Bodi hii na kusema kweli tunataka tutambue mchango mzuri sana wa Kamishna wa Bajeti katika kuendeleza shughuli za Shirika letu na hasa hasa katika kutoa michango ambayo imesaidia sana sana hata katika kuendeleza Shirika la *COASCO* katika utoaji wa fedha za kuliendesha. Kama mlivyosikia leo asubuhi Mheshimiwa Anne Makinda ameleeza jinsi ambavyo Serikali imesaidia kutoa nyenzo za kufanya kazi na vile vile kuboresha hata maslahi na kuwafundisha watumishi hawa. Zote hizi zinatoka kwenye Bajeti ya Serikali na kwa hali hiyo Kamishna wa Bajeti anakuwa ni mtu muhimu sana kuwepo katika Bodi ile.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vili Mheshimiwa Jacob Shibili alipendekeza kwamba hivi kwa nini isingetajwa tu hata moja kwa moja kwamba na Wabunge nao wawemo, tunaogopa nini? Nadhani hili si jambo baya, isipokuwa tu tunataka tuseme kwamba mamlaka ya uteuzi nadhani inayo hekima yake na inayatazama sana hayo pamoja na kwamba haitajwi moja kwa moja kwamba na Mbunge awepo na nani awepo, lakini wakati wa uteuzi hayo yote yanazingatiwa kwa kuangalia taaluma kwa sababu chombo kama hiki ni cha taaluma. Kwa hiyo, kama watapatikana Wabunge amba wana taaluma amba wanaweza kusaidia katika kuliendeleza shirika basi wanakuwemo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe tu mfano, Bodi ya sasa Mwenyekiti wake ni Mheshimiwa Anne Makinda ambaye ana taaluma ya uhasibu yaani mzoefu na huyu ni Mbunge japokuwa haikutajwa kwenye sheria kwamba Bodi iwe na Mwenyekiti Mbunge au *Board Member* mmoja awe Mbunge, lakini kwa hekima ya mamlaka ya uteuzi hilo limefanyika. Niseme hata katika Bodi iliyopita, Bodi iliyopita pia Mwenyekiti wake alikuwa Mbunge ambaye vile vili naye alikuwa na taaluma ya uhasibu na ukaguzi. Kwa hiyo, hata hivi nadhani tusipende kusema tu kwamba mpaka itajwe moja kwa moja. Mimi ningependa nishauri tu kwamba tuiachie mamlaka ya uteuzi ambayo inaweza kufanya kazi hiyo kwa kuzingatia taaluma za shirika linalohusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ipo hoja ilijitokeza ya wabadhirifu wa Ushirika kuachiwa huru na Mahakama na ikatolewa mfano hapa kule *VUASU*. Hii ilisemwa na Mheshimiwa John Singo na Mheshimiwa Khalid Suru ameleeza hapa kwa upande wa *CRCU* pia na Mheshimiwa Herbert Mntangi. Nimekwishaeleza kwamba katika maboresho haya tunayoyafanya au katika hizi *cooperative reforms* nia na madhumuni yake kusema kweli ni kupambana na haya. Kwa maana ya kwamba kwenye Sheria kwa mfano ile ya Ushirika yapo sasa hivi maadili ya uongozi na utendaji ndani ya Vyama vya Ushirika, nia na madhumuni yake ni kuhakikisha kwamba vitendo vya wizi na ubadhifuru vinadhibitiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kama nilivyokuwa nimesema kwamba suala la kwamba kesi hizi pengine zinapokwenda Mahakamani hazieleweki vizuri na hatimaye zinaachiwa na Mahakimu ndio tumesema kwamba sasa hivi kuna *Special Prosecutors*

ambao wana taaluma hiyo ya ushirika. Nadhani watakuwa na upeo mzuri sana wa kwenda kuelezea yaliyotokea na kwa namna hiyo unawarudishia imani wananchi ambao wanatakiwa kuanzisha ushirika.

Kwa hiyo, tungependa tuwashauri Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa John Singo kwa kule *VUASU* kwamba, masuala haya sasa kwa ujumla wake kusema kweli yanasisimamiwa vizuri kwa mujibu wa sheria mpya na yataendelea kufuatiliwa na kama nilivyokuwa nimesema kwamba inapobainika mahali kwamba wahusika wa ubadhirifu huo wamepatikana hatua za kisheria zinachukuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pengine niseme hili la *CRCU* ya Dodoma kwa sababu na mimi ni mdau, alilolisemea Mheshimiwa Khalid Suru asubuhi, amezungumza habari ya *CRCU*, kwanza *CRCU* ilishafilisika na hakuna kitu kinachoitwa *CRCU* sasa hivi, ilishafunga vitu vyake. Lakini kwa hili alilolitolea mfano la kwamba *CRCU* ilikuwa inadaiwa na Chama cha Msingi cha Kwadelo kule Kondo ni kweli na hili suala mimi nilikuwa nimekwishaletewa na mmoja wa wajumbe wa kutoka Kwadelo, alikuwa ni mjambe wa Halmashauri Kuu ya *CRCU* wakati huo Mzee Huruvi. Walishakuja hapa tukatoa maelezo tu kwamba, *CRCU* ilikwishafilisika na katika kufilisika kwake mali zilizouzwa hazikuweza hata kukidhi madeni mengine yaliyokuwa bado yanadaiwa na *CRCU*. Kwa hiyo, isingekuwa rahisi kutafuta fedha kwenda kukilipa chama hiki cha Kwadelo ambacho kilikuwa ni mmoja wa wanachama wake. Kwa hiyo, utaratibu wa kulipa madeni unafahamika kwamba unafuata yale mashirika ya Kiserikali na mengineyo na baadaye kuweza kufuatiliwa na wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Wizara itaendelea kuelimisha Vyama vya Ushirika ili pale ambapo kuna ushahidi wa kutosha basi wanachama wasimamie suala hilo kikamilifu ikiwa ni pamoja na kukata rufaa ili watuhumiwa wachukuliwe hatua za kisheria. Kuimarka kwa *COASCO* kupitia Sheria hii kutaliwezesha Shirika kufanya kazi kwa ufanisi na kubaini makosa mapema ili wahusika wachukuliwe hatua mapema. Aidha, Sheria ya Ushirika ya mwaka 2003, inatoa nafasi kwa Wizara kuwa na wapelelezi kama nilivyokuwa nimesema yaani *Special Prosecutors* na kuweza kufuatilia hizi kesi za Vyama vya Ushirika na hatimaye kubaini wale wote ambao watakuwa wamehusika na mambo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivytangulia kusema hapa kwamba hoja zote zilizokuwa zinatolewa hapa kusema ukweli zilikuwa ni za kusaidia ili tuweze kusimamia utekelezaji wa sheria hii vizuri. Nami nina imani kabisa kwamba marekebisho haya yakishapitishwa na Bunge lako Tukufu yatasaidia sana sana utendaji wa Shirika letu la *COASCO* na kwa hakika itasaidia sana kazi za ukaguzi ambazo zilikuwa zimelala kwa miaka mingi. Asubuhi imeelezwa kwamba huko nyuma *COASCO* ilikuwa imekagua Vyama vya Ushirika vingi na ilikuwa bado inavidai, lakini nadhani kwa marekebisho haya kwa sababu sasa *COASCO* itakuwa ina nafasi ya kukagua na taasisi zingine ambazo zina uwezo wa kuweza kulipa, itajiimarisha zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka tu niseme kwamba kwa sababu *COASCO* ndio yenyeye uzoefu wa kukagua Vyama vya Ushirika na vikundi vingine vingine, kwa hiyo hata vile vikundi ambavyo vimetajwa asubuhi na Mheshimiwa Halinga kwamba sasa

vikundi hivi vinaanzishwa havina habari tena na ushirika, havina habari tena hata na Shirika la *COASCO*.

Mimi nataka nishauri kwamba kwa vyovyyote vile uite kikundi au Chama cha Ushirika lakini nia na madhumuni kusema kweli ni kuunganisha uwezo kwa sababu uwezo wa mtu mmoja mmoja hauwezi kutufikisha mahali popote. Kwa hiyo, kama utaungana kwenye kikundi nia yake ni kukusanya uwezo badala ya kupeleka gunia lako moja peke yako mpaka ukalikute soko, basi mnaungana kwenye kikundi, ushirika au chochote kile utakachokiita, lakini nia na madhumuni kusema kweli ni kukusanya uwezo wa pamoja ili kuweza kufikia azma inayokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo vikundi mbalimbali na Vyama nya Ushirika vyote vitahitaji ukaguzi kwa vyovyyote vile ili hesabu zao ziweze kukaguliwa na hatimaye kutoa taarifa kwa wahusika na hayo ya wizi yote ambayo yalikuwa yameelezwa asubuhi yaweze kubainika mapema. Kwa hiyo, huwezi kusema tu kwamba, maadam nimeshaanzisha kikundi basi na hata ukaguzi kwaheri. Kusema kweli itakuwa sio sahihi kwa sababu itakuwa haikupi pitcha nzuri ambayo itakuwezesha kuwa na mwongozo mzuri wa kujua kwamba unachokifanya ni kizuri au la.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nikushukuru tena kwa mara nyingine kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia hoja hii na naomba nirudie tena kusema naunga mkono hoja hii. (*Makofi*)

**WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba na mimi nichukue fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwako kwa kunipa nafasi kwa mara nyingine kusudi nihitimishe hoja yangu niliyoitao hapa Bungeni leo asubuhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri Hezekiah Chibulunje, Mbunge wa Jimbo la Chilonwa, kwa kunisaidia kujibu hoja nyingi zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge wakati wa kuchangia hoja yangu leo asubuhi. Namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda vile vile kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia katika mjadala wa Muswada huu ama kwa maandishi au kwa kuongeza hapa Bungeni. Napenda niwatambue kwa kuwataja majina yao kama ifuatavyo:-

Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa kuzungumza ni kama ifuatavyo, Mheshimiwa Ismail Iwavatta, ambaye aliongea kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara na kuwasilisha maoni ya Kamati ya Uwekezaji na Biashara, Mheshimiwa Aisha Magina, Msemaji wa Kambi ya Upinzani na vile vile Waziri Kivuli kwa Wizara yangu, Mheshimiwa Dr. Talala Mbise, Mheshimiwa John Singo, Mheshimiwa Edson Halinga, Mheshimiwa Jacob Shibili, Mheshimiwa Khalidi Suru, Mheshimiwa Semindu Pawa, Mheshimiwa Stephen Kazi, Mheshimiwa Anne Makinda na

Mheshimiwa Hezekiah Chibulunje, Naibu Waziri wa Wizara ya Ushirika na Masoko. (*Makofî*)

Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Ireneus Ngwatura, Mheshimiwa Paul Ntwina, Mheshimiwa Herbert Mntangi na Mheshimiwa Khamis Awesu Aboud. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema katika utangulizi, Mheshimiwa Naibu Waziri ametoa maelezo na ufanuzi kwa baadhi ya michango ya Waheshimiwa Wabunge waliota katika mjadala wa hoja hii tangu asubuhi. Mimi ningependa kuchangia katika maeneo machache ambayo Waheshimiwa Wabunge wameyazungumzia lakini yanayohusiana na mambo ya jumla na ya kisera.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia kwa maandishi na kwa kauli katika Muswada huu. Wabunge hao ni hawa wafuatao:- Mheshimiwa Anne Makinda na Mheshimiwa Semindu Pawa kwa michango yao ambayo imesaidia kufafanua hoja kadhaa za Waheshimiwa Wabunge. Maoni na mapendekezo ya Waheshimiwa Wabunge ambayo hayahu moja kwa moja katika Muswada huu lakini yanahusu uboreshaji wa maendeleo ya Vyama vya Ushirika yamepokelewa na ninapenda kuwahakikisha Waheshimiwa Wabunge kwamba Wizara yangu itayafanya kazi ipasavyo. (*Makofî*)

Hoja ya Mheshimiwa Dr. Talala Mbise wa Arumeru Mashariki inayohusu suala la madeni ya wakulima wa Kahawa wa Arumeru Mashariki, hili pamoja na madeni ya Vyama vingine yanashughulikiwa na Wizara pamoja na madeni mengine ya Vyama vya Ushirika. Kauli ya Serikali kuhusu tatizo hili itatolewa baada ya mashauriano ndani ya Serikali Kuu kukamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hoja nyingine ilitolewa kuhusu *COASCO* kuwa na jukumu la kusimamia ukaguzi wakati yenye we inafanya ukaguzi. Waliochangia katika hoja hii walikuwa ni Mheshimiwa Aisha Magina, Mheshimiwa Edson Halinga, Mheshimiwa Dr. Talala Mbise, Mheshimiwa Jacob Shibili, Mheshimiwa Semindu Pawa na Mheshimiwa Anne Makinda. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama alivyotangulia kueleza Mheshimiwa Naibu Waziri, ipo haja ya kuwa na Msimamizi wa Ukaguzi wa Vyama vya Ushirika na Mkaguzi huyo ni *COASCO* kama tulivyoeleza. *COASCO* ina dhamana ya ukaguzi wa Vyama vya Ushirika na ni chombo cha kudhibiti ukaguzi wa Vyama vya Ushirika. Pia, *COASCO* inawajibika kuhakikisha kuwa matumizi ya taarifa za ukaguzi wa Vyama vya Ushirika zinawasilishwa kwa wanachama wake. Hili tumelisisitiza kwa wote wanaohusika, si viongozi wa *COASCO* peke yake, lakini na kwa Viongozi wa Vyama vya Ushirika vyote nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ilitolewa hoja nyingine ya nne ambayo inasema, kufanywe mabadiliko ya jumla kwenye Shirika la *COASCO* ili kuondoa mapungufu kwenye Ushirika. Waliochangia hoja hiyo walikuwa ni Mheshimiwa John Singo,

Mheshimiwa Anne Makinda na Mheshimiwa Edson Halinga. Tungependa kutoa maelezo yafuatao katika hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya *COASCO* haiwezi kuzungumzia mambo yote ya Ushirika kama alivyoeleza Mheshimiwa Naibu Waziri, kwani kuna sheria mama ya Vyama vya Ushirika ambayo Bunge hili Tukufu liliipitisha mwaka 2003 ambayo inazungumzia mapungufu ya Ushirika kwa jumla na kama alivyoeleza pia tuna mpango kabambe ambao tunauita *Cooperative Reform and Modernization Programme* ambao unachukua muda wa miaka minne ambao utaweza kurekebisha mambo mengi ambayo yamejitokeza katika kuendesha Vyama vya Ushirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mpango huu, pengine ningependa Waheshimiwa Wabunge wafahamu kwamba tumesaidiwa na Mashirika mengine na nchi nyingine rafiki. Ni kwamba katika muda wa miaka minne ijayo tutapata msaada wa kuweza kuwafundisha watu wa kwenda katika Vijiji kuwaeleza wananchi juu ya Ushirika na faida zake wapatao 250 ambao watasaidia sana katika kueneza Ushirika katika sehemu zote za uvuvi, za wakulima, za fedha na kadhalika. Sheria ya zamani ya Ushirika ya mwaka 1991 ilifanyiwa mapitio na Sheria ya mwaka 2003 kama alivyo sema. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mara nyingine tena nawashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao na ninawaomba wapitishe Muswada huu kutuongezea nguvu za kuimarisha Ushirika nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo machache. Naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

(*Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Pili*)

## KAMATI YA BUNGE ZIMA

**Muswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria ya Shirika la  
Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika wa  
mwaka 2005 (*The Cooperatives Audit and Supervision  
Amendment Bill, 2005*)**

Jina la Muswada

(*Jina la Muswada lililotajwa hapo juu lilipitishwa na  
Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebishi yake*)

Ibara ya 1

(*Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima bila mabadiliko yoyote*)

Ibara ya 2

Ibara ya 3

Ibara ya 4

Ibara ya 5

Ibara ya 6

(*Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima pamoja na marekebisho yake*)

Ibara ya 7

Ibara ya 8

Ibara ya 9

Ibara ya 10

Ibara ya 11

(*Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima bila mabadiliko yoyote*)

Ibara ya 12

(*Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima pamoja na marekebisho yake*)

Ibara ya 13

Ibar ya 14

Ibara ya 15

(*Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima bila mabadiliko yoyote*)

Ibara ya 16

(*Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima pamoja na marekebisho yake*)

(*Bunge lilirudia*)

***Muswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria ya Shirika la Ulaguzi na***

***Usimamizi wa Vyama vya Ushirika wa Mwaka 2005***

***(The Cooperatives Audit and Supervision Amendment Bill, 2005)***

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imepitia Muswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria ya Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vyta Ushirika wa mwaka 2005 uitwao, *the Cooperative Audit and Supervision Amendment Act, 2005* pamoja na marekebisho yake kifungu kwa kifungu na kuukubali. Hivyo basi, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa *the Cooperative Audit and Supervision Amendment Act, 2005* sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya  
Tatu na Kupitishwa)*

***Muswada wa Sheria ya Kutumia Stakabadhi za Mazao  
yaliiyowekwa kwenye Maghala wa mwaka 2005  
(The Warehouse Receipts Bill, 2005)***

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Stakabadhi za Mazao kwenye Maghala uitwao *the Warehouse Receipts Act, 2005* pamoja na marekebisho yake ambayo Waheshimiwa Wabunge wamegawiwa sasa usomwe kwa mara ya pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa wale wote waliowezesha Muswada huu wa Sheria ya Mfumo wa Stakabadhi za Mazao kwenye Maghala ukamilike na kuwasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu.

Napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Uwekezaji na Biashara, Mheshimiwa William Shellukindo na Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati hiyo kwa uchambuzi wa kina wa Muswada huu na mapendekezo yao. Napenda pia kuwashukuru wadau ambao walishiriki kikamilifu katika kuujadili Muswada huu. Maoni na mapendekezo yao yamesaidia sana kuuboresha Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee napenda niwashukuru Waheshimiwa Wabunge waliohudhuria Semina mbalimbali zilizojadili umuhimu wa Mfumo wa Stakabadhi za Mazao kwenye Maghala na kuchangia mawazo ambayo ni mojawapo ya chimbuko la Muswada huu.

Vilevile, nichukue fursa hii kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote walioshiriki katika Semina Maalum iliyofanyika katika ukumbi huu tarehe 15 Aprili, 2005. Ushauri na maoni yao yamesaidia kuongeza uelewa kuhusu umuhimu na faida za Mfumo wa Stakabadhi za Mazao kwenye Maghala. Napenda niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba ushauri na maoni yao yatazingatiwa katika kutekeleza sheria itakayotungwa kutokana na Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, madhumuni ya Muswada huu ni kutunga sheria ya kusimamia Mfumo wa Kutumia Stakabadhi za Mazao kwenye Maghala ikiwa ni njia madhubuti ya kuhakikisha ongezeko la uzalishaji wa bidhaa zenyenye ubora na uwezo wa kutumiwa kwa bidhaa zao hizo, kuongeza mtaji wa kifedha kwa wazalishaji wa bidhaa. Muswada huu ukipitishwa, sheria inayopendekezwa itawezesha wakulima na wafanyabiashara wadogo wadogo kuweza kupata mikopo katika mabenki kwa kutumia Stakabadhi za Mazao yaliyowekwa kwenye Maghala kama dhamana. Rasilimali zisizotambulika kibenki kwa sasa kama mazao ya kilimo zitahalalishwa kisheria ili zitambulike na kutumiwa kama dhamana ya kupata mikopo katika mabenki.

Mheshimiwa Naibu Spika, chimbuko hasa la Mfumo wa Stakabadhi za Mazao kwenye Maghala hapa nchini lilitokana na udhaifu wa uchumi wa soko huru katika Sekta ya Kilimo ulioanzishwa miaka ya 90 na kusababisha kuyumba kwa mfumo uliokuwepo kwa kutoa mikopo kwa wakulima wadogo hususan mikopo ya kununulia mazao na pembejeo kupitia Vyama vya Ushirika. Aidha, kutokana na Vyama vya Ushirika kukabili ana na ushindani wa wafanyabiashara wakubwa usiokuwa wa haki, uongozi mbaya ndani ya Vyama vya Ushirika uliokuwepo na ukosefu wa dhamana, Vyama vingi vya Ushirika vilishindwa kutoa huduma kwa wanachama na wakulima kwa ujumla kwa kukosa mikopo.

Vilevile, Vyama vya Ushirika vilivyoweza kupata mikopo kutoka Benki za Biashara kwa ajili ya kununulia mazao ya wakulima walipewa mikopo hiyo kwa masharti magumu ikiwa ni pamoja na riba kubwa, gharama za kukubali mkopo yaani *commitment fees* na kulazimika kuwa na dhamana za mali zisizohamishika. Yote haya yamekuwa yakiongeza gharama ambazo hukatwa kutoka kwenye mapato ya wakulima. Kutokana na hali hiyo, wakulima wengi wamekuwa hawana mfumo wa uhakika wa kupata mikopo ya kuwawezesha kukidhi mahitaji yao mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua zilizochukuliwa na Serikali kukabili tatizo hili ni kama ifuatavyo:- Kuanzia mwaka 2000 Serikali ilianza kuchukua hatua za kuweka mifumo mbalimbali ya kuwawezesha wakulima wadogo kupata mikopo hususan ya kununulia mazao yao. Mifumo hiyo ni pamoja na Mfuko wa Dhamana ya Mikopo kwa ajili ya kuuza bidhaa nje ya nchi, yaani *the Export Credit Guarantee Scheme* na Mfuko wa Kudhamini Biashara ndogo na za kati, yaani *Small and Medium Enterprises Guarantee Fund*.

Lakini kweli kwamba Mifuko hii inayosaidia sana wakulima kupata mikopo ni ya gharama, kwa sababu matumizi yake huhitaji dhamana ya mali isiyohamishika na inahitaji wadhamini mali, yaani *collateral managers* ambao hutoza gharama kubwa kwa huduma zao. Kutokana na hali hiyo, Serikali imeendelea kutafuta mifumo endelevu ya kuwawezesha wakulima kupata mikopo kwa gharama nafuu ukiwemo Mfuko wa Stakabadhi za Maghala, yaani *the Warehouse Receipts System*. Kwa mantiki hii, Mfumo wa Stakabadhi za Maghala hautaondoa fursa nyingine zilizopo za kuwawezesha wakulima kupata mikopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kurudia hili. Mfumo wa Stakabadhi za Maghala hautaondoa fursa nyingine zilizopo za kuwawezesha wakulima kupata mikopo. Mfumo huu una lengo la kusaidia jitihada ambazo zinaendelea kutekelezwa kwa kutoa fursa nyingine kwa wale ambao fursa zilizopo hazitoshi kukidhi matakwa yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfumo wa Stakabadhi za Maghala ni utaratibu ambao unawawezesha wakulima wadogo kuitia Vyama vya Ushirika au vikundi vyao kutumia mazao yao kwenye maghala kama dhamana ya kupata ya mikopo. Mfumo huu hutumia stakabadhi za ghala zinazotolewa na mwendesha ghala ambazo zinakuwa na hadhi na thamani kama zilivyo nyaraka nyingine za fedha, yaani *negotiable instruments*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfumo wa Stakabadhi za Mazao kwenye Maghala kama dhamana ya mikopo, unatumika sehemu nyingi duniani. Katika Bara la Afrika umetumika kwa mafanikio katika nchi za Afrika Magharibi hususan katika nchi za Ghana na Mali. Aidha, unatumika Afrika Kusini, Zimbabwe na Zambia na katika Afrika Mashariki nchi ya Uganda ilianza kutumia utaratibu huu kuanzia mwaka 2003.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa Tanzania mfumo huu umetumika kwa majaribio kwa kuitia mradi wa kuendeleza na kuboresha biashara na masoko ya mazao ya pamba na kahawa unaohifadhiwa, *Common Fund for Commodities (CFC)*. Mradi huo uliozinduliwa rasmi tarehe 20 Septemba, 2000 unatekelezwa katika Mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Mbeya, Ruvuma, Kigoma, Kagera kwa zao la kahawa na Mikoa ya Shinyanga, Mara, Mwanza, Kagera, Morogoro, Pwani na Manyara kwa zao la pamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa zao la kahawa mafanikio makubwa yameonekana katika Mikoa ya Kilimanjaro anapotoka Mheshimiwa Thomas Ngawaiya. Mbeya na Ruvuma na kwa upande wa zao la pamba mafanikio yameonekana Mkoani Manyara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mikoa hii yenye mafanikio, Vyama Vikuu vya Ushirika vya Msingi, vikundi vya wakulima na hata Kampuni ndogo ndogo binafsi za Watanzania zilipata mikopo kwa ajili ya kukusanya mazao ya wakulima, kuyasindika na hatimaye kuyauza yakiwa na ubora wa hali ya juu zaidi. Vyama vya Ushirika na vikundi hivyo vimeweza kuwalipa wakulima fedha nyingi zaidi kuliko wale waliouza nje ya utaratibu huu. (*Makofi*)

Aidha, Vyama vya Ushirika vilivyotumia mfumo huu vimeweza kuwalipa wanachama na wakulima wao malipo ya pili na hata ya tatu. Mifano halisi ni Vyama vya Msingi 31 katika Mkoa wa Kilimanjaro, Vyama saba katika Mkoa wa Ruvuma, Chama kimoja katika Mkoa wa Manyara, Vyama Vikuu vya Ushirika vya *KCU, KNCU, MBOCU, MICU, VUACU* na *ISAYULA* pamoja na vikundi vya wakulima vya Jinusuru na Jikomboe vilivyoko Wilayani Mbozi, Mkoani Mbeya anakotoka Mheshimiwa Edson Halinga. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema, mfumo huu umetumika kwa majaribio kwa mazao ya pamba na kahawa. Lakini mfumo wenyewe unaweza kutumika kwa mazao yote ya biashara na hata ya chakula hususan nafaka. Kwa sababu hiyo, Serikali inaazimia kueneza matumizi ya Mfuko huu kwa mazao mengine na pia katika Mikoa mingine ambayo haikuwa kwenye mradi huu. Kwa sababu hiyo, Muswada unaowasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu unalenga mazao yote.

Aidha, mara baada ya Sheria ya Stakabadhi za Mazao kwenye Maghala kutungwa, mazao mengine yanayoweza kuhifadhiwa kwa muda mrefu yataweza kutumia utaratibu huu. Utaratibu huu pia utaweza kutumika kwa baadaye kwa mazao kama mbogamboga na matunda endapo maghala yataboreshwaa na kuweza kuhifadhi bidhaa za namna hiyo kwa muda mrefu kama inavyofanyika Afrika Kusini hadi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfumo wa Stakabadhi za Mazao kwenye Maghala umeonyesha kuwa na manufaa na faida nydingi. Muhimu kati yake ni hizi zifuatazo:-

Kwanza, unawezesha matumizi ya mbinu za masoko ya kisasa yaani *Modern Marketing Techniques*; kwa mfano, kuwawezesha wakulima kujikinga na mabadiliko ya ghafla ya bei na kuuza mazao yao bila ya kulazimika kuyapeleka sokoni. Katika kipindi hiki cha utandawazi, Tanzania haiwezi kukwepa kutumia mbinu hizo za kisasa.

Pili, unapunguza upotevu wa mazao baada ya kuvunwa na hivyo kuongeza uhakika wa chakula na kipato kutokana na hifadhi bora. Hivi sasa kati ya asilimia 30 hadi 40 za mazao ya chakula zinapotea baada ya kuvuna kutokana na hifadhi hafifu.

Tatu, kupunguza athari za kuporomoka kwa bei. Utekelezaji wa mfumo utawezesha wakulima kuweka mbinu endelevu za kuhimili mporomoko wa bei kama Bima na kinga ya bei.

Nne, kuwawezesha wakulima kuhifadhi mazao yao kwa usalama na kwa muda mrefu na hivyo kuyauza wakati ambapo bei ni nzuri au wanapohitaji kuyauza. Mkulima anahifadhi mazao yake na akiyauza bei inapokuwa nzuri hupata faida kubwa kuliko wanaoyauza mara tu baada ya kuvuna bila kuzingatia mwenendo wa bei. Hii inawezekana, licha ya gharama za Bima, uhifadhi, usindikaji na usafirishaji zinazotozwa; kwa mfano, utafiti uliofanywa mwaka 2004 na Kampuni ya EC Mkoa wa Mbeya kwa mazao ya mpunga na mahindi unaonyesha kuwa kilo moja ya mpunga huuzwa wakati wa mavuno kwa Sh. 60/= sawa na gharama za uzalishaji. Gharama za uendeshaji wa ghala

ni Sh.1.25, gharama ya Bima ni Sh.1.50 na riba ya mkopo wa Benki kwa miezi minne hadi mitano ni Sh.5/= kwa kilo.

Kwa hiyo, jumla ya gharama zote zilifika Sh.67.75 kwa kilo moja. Bei ya kuuzia kwa kutumia mfumo huu ilikuwa Sh.1.25/= kwa kilo. Hii ina maana kwamba mkulima aliyetumia mfumo wa stakabadhi za maghala alipata faida ya Sh.57.25/= kwa kilo wakati aliyeuza mara moja baada ya kuvuna hakupata faida yoyote.

Aidha, utafiti kama huo ulifanyika kwa zao la mahindi na kubaini kuwa mkulima aliyetumia mfumo wa stakabadhi za mazao aliuza kwa Sh.30/= kwa kilo wakati yule aliyeuza baada ya kuvuna alipata Sh.12/= kwa kilo. Ukiiondoa gharama za uzalishaji ambazo ni Sh.15/= kwa kilo mkulima alipata faida ya Sh.15/= kwa kilo alipotumia mfumo huu wakati yule aliyeuza mara baada ya kuvuna alipata hasara Sh.3/= kwa kilo.

Tano, kuwawezesha wakulima wanaohitaji mikopo ya Benki kuwa na dhamana zinazokubalika na mabenki na hivyo kuwafanya wakopesheke. Faida za mfumo huu zimejionyesha wazi katika Vyama vya Ushirika na vikundi vya wakulima katika maeneo mbalimbali yanayolima kahawa na pamba kama nilivyokwishaeleza hapo awali.

Sita, kusaidia kuongeza ubora na matumizi ya viwango yaani *standards* kwa mazao yanayouzwa katika masoko ya ndani kikanda na Kimataifa kwa vile yanahifadhiwa katika maghala yaliyoidhinishwa na yanayosimamiwa na Sheria.

Saba, kuwepo kwa sheria kutasaidia kuongeza imani kwa Taasisi za fedha, kutoa mikopo kwa kutumia Stakabadhi za Mazao kwenye Maghala kama dhamana. Kwa hiyo, Benki nyingi zitashiriki kutoa mikopo kwa wakulima. Hali hii itaongeza ushindani wa kutoa huduma bora zenye ufanisi na zenye riba nafuu. Aidha, Benki ya *CRDB, Kilimanjaro Cooperative Bank* na *EXIM Bank* zinatoa mikopo hiyo, kwa sasa zinakiri kuwa kutokana na ugumu uliopo wa kuuza mali zisizohamishika. Mfumo huu unafaa zaidi kuliko kutumia dhamana ya mali zisizohamishika pekee.

Benki hizo zimeanza kutumia mfumo wa Stakabadhi za Maghala bila kuhitaji udhamini wa kutoka kwa wasimamizi wa dhamana yaani *Collateral Managers* bali wanatumia udhamini unaotolewa na waendesha maghala. Mbinu hii imepunguza gharama za kusimamia mikopo na woga wa hasara, yaani *perceive risk* kwa mikopo inayotolewa na Benki hizo. Hali hii imefanya riba zinazotozwa chini ya mfumo huu kupungua hadi asilimia 12 ikilinganishwa na zile zinazotozwa nje ya mfumo huu ambazo ni asilimia 19 au zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafanikio ya mfumo wa Stakabadhi za Maghala yanatategemea kwa kiasi kikubwa kuwepo kwa maghala na waendeshaji makini. Aidha, mazao yatakayohifadhiwa yanapaswa kuwa yenye wingi wa kutosha na wenye viwango vya madaraja ya ubora. Hivyo, wingi wa mazao bora ndivyo vitakavyochochea kuwepo kwa maghala katika sehemu fulani. Kwa kuhamasisha wakulima kujiunga kwenye Vyama vya Ushirika na vikundi wingi wa mazao utapatikana. Aidha, ili kuwepo kwa maghala yenye ubora katika ngazi zote, Serikali tayari imefanya tathmini ya maghala

yaliyopo na ubora wake. Maghala yanahitaji ukarabati na maeneo mengine yanahitaji maghala mapya.

Aidha, Serikali kupitia programu ya uboreshaji mifumo ya masoko ya mazao ya kilimo imeanza kuwezesha Halmashauri za Wilaya kukarabati na kujenga maghala katika maeneo ambayo programu inatekelezwa. Serikali itaendelea kuhamasisha sekta binafsi vikiwemo Vyama vya Ushirika kujenga maghala ili yaweze kukidhi mahitaji chini ya Mfumo wa Stakabadhi za Maghala.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile mfumo huu ni mpya na wadau wengi bado hawajaelewa vizuri, Serikali kwa kushirikiana na wadau wengine itaendelea kutoa mafunzo kwa wadau wote wakiwemo wakulima, Vyama vya Ushirika, vikundi, vyombo vya fedha, wamiliki na waendesha maghala kuhusu utekelezaji na manufaa ya mfumo huu. Hadi sasa mafunzo yameshatolewa kwa wakulima katika maeneo ya majaribio yanayozalisha mazao ya kahawa na pamba na maeneo ambayo ujenzi na ukarabati wa maghala unafanyika. Mafunzo haya yanafanywa kwa ushirikiano wa karibu na watendaji wa Wilaya husika na mabenki ya *CRDB, Kilimanjaro Cooperative Bank* na *EXIM Bank*.

Kwa upande wa Serikali, mafunzo hayo yanaendeshwa kwa kutumia bajeti ya kawaida ya Wizara pamoja na fedha za maendeleo kupitia mradi wa kuendeleza na kuboresha biashara na masoko ya mazao ya pamba na kahawa; mradi wa kuendeleza mifumo ya masoko ya mazao ya kilimo; mpango wa huduma za fedha Vijijini na programu ya kuendeleza Sekta ya Kilimo. Lengo la mafunzo haya ni kuhakikisha kuwa wakulima wengi wanauelewa na kutumia mfumo huu kwa faida yao. Mafunzo yanatilia pia mkazo wa kuongeza uzalishaji ili mazao yanayowasilishwa ghalani yawe mengi na yenye ubora unaoridhisha.

Aidha, mafunzo yatalenga kuwaelimisha kuhusu mbinu za kuepuka hasara zinazoweza kutokea hususan mabadiliko ya bei na namna ya kunufaika na fursa zinazojitezea katika soko. Benki zitahamasishwa kushiriki kwa wingi zaidi na sekta binafsi vikiwemo Vyama vya Ushirika ili kuboresha maghala yaliyopo na kujenga mapya kadri ya mahitaji na kujenga viwanda vya usindikaji mazao, kwa lengo la kuyaongezea thamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili mfumo huu wa Stakabadhi za Mazao kwenye Maghala uweze kutumika kikamilifu na kuendelea kuwa na manufaa na faida kwa wananchi wote, ni muhimu pawepo na sheria ya kusimamia mfumo wenyewe. Sheria itabainisha pamoja na mambo mengine, wajibu na haki ya kila mdaa na itafafanua kuhusu namna stakabadhi zenyewe zitakavyotakiwa kuwa ili kukwepa kugushiwa kirahisi na kuzuia vitendo vya uhalifu kwa ujumla.

Matumizi ya mfumo huu ni njia endelevu na madhubuti ya kuhakikisha ongezeko la uzalishaji wa mazao na bidhaa za kilimo zenyewe viwango vya ubora unaokubalika Kitaifa na Kimataifa. Kwa sababu hiyo, kutungwa kwa sheria hii ni moja ya mikakati ya kuunga mkono jitihada za kuleta maendeleo ya haraka na kuondoa umaskini nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu umegawanyika katika sehemu tisa kama ifuatavyo:-

- 1) Ufafanuzi.
  - 2) Inapendekeza kuanzishwa kwa Bodi ambayo itakuwa chombo cha usimamizi wa mfumo huu hapa nchini.
  - 3) Inafafanua mapato ya Bodi na inapendekeza taratibu za usimamizi wa fedha katika Bodi.
  - 4) Inaweka masharti kuhusu utaratibu wa upatikanaji wa leseni ya kuendesha mfumo huu.
  - 5) Inaeleza hadhi, utaratibu wa kutoa Stakabadhi na jinsi itakavyotumika katika mfumo huu.
  - 6) Inaainisha haki na wajibu wa mwendesha ghala yeny leseni ya kufanya shughuli na kutumia Stakabadhi ya mazao yaliyomo katika maghala.
  - 7) Inaweka masharti kuhusu utaratibu utakaotumika katika kuhamasisha haki ya umiliki katika kuhamisha haki ya umiliki wa Stakabadhi ya mazao.
  - 8) Inaainisha makosa mbalimbali na adhabu zitakazotolewa kama makosa kwa makosa hayo. Lengo la adhabu hizi ni kuondoa au kuepusha wizi na udanganyifu katika mfumo huo.
  - 9) Inaweka utaratibu unaompatia mamlaka Waziri mwenye dhamana ya masoko ya mazao ya kilimo kutunga au kutengeneza Kanuni ili kuwezesha Muswada huu wa sheria uweze kutekelezwa.
- Aidha, jedwali linapendekeza namna ya kuwapata Wajumbe wa Bodi idadi yao na taratibu za Mikutano ya Bodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema hapo awali, Muswada huu kwa ujumla unapendekeza sheria ambayo ni muhimu katika utaratibu wa kisasa wa biashara ya mazao ya kilimo na bidhaa nchini unaolenga katika kuwasaidia wakulima wadogo kupata mikopo katika Benki na hivyo kuongeza uzalishaji wa mazao na bidhaa zake zenyen ubora na kupata huduma bora za kifedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya, sasa naliomba Bunge lako Tukufu lijadili Muswada huu uitwao *The Warehouse Receipts, 2005* na kupitishwa kuwa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofî*)

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

**MHE. MBARUK K. MWANDORO (K.n.y. MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO - MWENYEKITI WA KAMATI YA UWEKEZAJI NA BIASHARA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 70 (b) Toleo la 2004, Kamati ya Uwekezaji na Biashara imemaliza kazi ya kuchambua na kujadili Muswada wa *The Warehouse Receipts Act, 2005* na sasa iko tayari kutoa maoni yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni haya ni matokeo ya mchakato mrefu wa kuandaa Muswada huu. Kwa upande wa Kamati, Mheshimiwa Waziri Balozi Clement George Kahama, aliandaa Semina ya siku moja kwa Wajumbe ili kueleza nia na madhumuni ya Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Semina hiyo tulieleweshwa kwa kina jinsi mfumo huo utakavyofanya kazi na manufaa yake kwa wakulima wetu pamoja na kwa uchumi wa Taifa letu. Aidha, tulieleweshwa mafanikio yaliyopatikana katika maeneo ambayo utaratibu huu ulifanyiwa majaribio katika Mikoa ya Mbeya, Ruvuma na Kilimanjaro.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya Semina Kamati ilikutana na wadau ili kupata maoni yao juu ya Muswada huu. Napenda kuwatambua wadau wafuatao ambao walifika mbele ya Kamati na kutoa maoni yao au maoni ya Taasisi zao. Taasisi hizo ni Bodi ya Pamba, Bodi ya Kahawa, Bodi ya Pareto, *Audit Control and Expertise Limited*. Aidha, michango iliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwenye Semina iliyoandalisha na Wizara hii hapa tarehe 15 Aprili, 2005 pia imechangia kwa kiasi kikubwa kwenye maoni ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya Semina pamoja na Mkutano wa wadau, Kamati ilikaa kwenye Kikao chake cha kawaida. Katika Kikao hicho, Kamati ilizingatia maeneo yafuatayo:-

- 1) Wakulima na wafanyabiashara wadogo kupata mkopo;
- 2) Ubora wa mazao;
- 3) Kuwepo kwa maghala bora;
- 4) Gharama kutokana na mchakato huo;
- 5) Huduma za Ugani kwa wakulima;
- 6) Elimu kwa wananchi;
- 7) Kuongeza gharama za mazao;
- 8) Kuimarisha ushirika na vikundi vyta wakulima;

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kujadili Muswada huu, Kamati imeridhika kwa kuletwa kwake kwani itakuwa ukombozi mkubwa kwa wakulima na wafanyabiashara wadogo wadogo. Aidha, mfumo huu si mbadala kwa taratibu nyingine

ambazo zinalenga katika kumsaidia mkulima wetu kama vile *Export Trade Guarantee Scheme* na nyinginezo bali kwa lengo la kumwona mkulima anafaidika zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muda mrefu wakulima wamekuwa wanashindwa kupata mikopo ya kuendeleza shughuli zao za kilimo na mipango ya maendeleo kwa kukosa dhamana ya mikopo hiyo na pia kutojua utaratibu wa kupata mikopo yenye. Hali hii imedumaza maendeleo yao kwa kutumia stakabadhi ya mahali. Mkulima atapata faida zifuatazo:-

- 1) Ataweza kutumia stakabadhi kupata mikopo kutoka Benki kwa kutumia mazao kama dhamana.
- 2) Ataweza kuibadilisha stakabadhi hiyo kuwa fedha taslimu ili kumaliza matatizo yanayomkabili.
- 3) Mkulima huyo ataweza akahifadhi mazao hayo hadi bei zitakapokuwa nzuri kwenye soko.

Mheshimiwa Naibu Spika, wote tunakubaliana hapa kuwa kwa miaka ya hivi karibuni tumeshuhudia jinsi ubora wa mazao yetu ulivyoshuka na sehemu nyingine tumeshuhudia pamba ikichanganywa na mchanga au maji ili iweze kuvuta uzito zaidi kwenye gulio au Kahawa ambayo haijakaushwa au kuchambuliwa vizuri. Mazao hayo yakipelekwa kwenye Soko la Dunia yanapata bei haffifu. Tunaamini kuwa sheria hii ikitekelezwa kikamilifu, basi wakulima wetu watapata bei nzuri ya mazao yao kutokana na ubora wa mazao yenye.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaamini kuwa Muswada huu utahamasisha na kuimarisha vikundi vya wakulima na ushirika ili wapate mazao mengi na bora zaidi na hivyo kupata bei nzuri na mapato makubwa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukuhakikishia kuwa kutokana na Semina tulioipata, michango ya wadau wakiwemo Waheshimiwa Wabunge kwenye Semina, Kamati imeweza kuwa na msimamo na uelewa wa kutosha kuhusu Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunamshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kufanya kazi baadhi ya maoni ya wadau na Kamati na hivyo kufanya marekebisho kwenye Muswada huu na pia kutuelimisha kuhusu pale ambapo hapakueleweka vizuri na hatimaye tukakubaliana. Tunampongeza sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na malengo mazuri ya Muswada huu, mafanikio yake hayataonekana kama wakulima hawataelimishwa kuhusu faida zake. Hivyo, tunaiomba Wizara, Waheshimiwa Wabunge na wengine waielimishe jamii ili iweze kuelewa ipasavyo na kunufaika na utekelezaji wa sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iimarishe huduma za ugani ili wakulima waweze kuzalisha mazao mengi na bora kwa gharama nafuu ili kupata faida kubwa.

Tatu, Muswada huu unakuja na utamaduni mpya wa huduma za kulipiwa kwa mfano Bima ya Mazao, gharama ya kuhifadhi mazao, gharama za usafiri, riba na kadhalika. Kamati inaiomba Serikali kwamba iandae mazingira ambayo yatahakikisha kwamba gharama hizi hazitamuathiri mkulima kwa kiasi kikubwa na kumsababishia hasara.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, tunaishauri Wizara iimarishe ushirika kwa kuwapeleka Maafisa Ushirika katika ngazi ya Wilaya na Vijiji ambao watahamasisha shughuli za vikundi na ushirika ikiwa ni pamoja na kutoa elimu ya ushirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijamaliza mchango wangu huu, naomba nichukue nafasi hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia hotuba ya Waziri wa Ushirika na Masoko. Naomba pia nimshukuru Mheshimiwa Waziri Balozi Clement George Kahama, Mheshimiwa Hezekiah Chibulunje, Naibu Waziri, Dr. C. Komba, Katibu Mkuu Wizara ya Ushirika na Masoko na wafanyakazi wote walioshiriki katika kuandaa Muswada huu kwa njia moja au nytingine na kwa ushirikiano wao waliounyesha wakati wote wa kuchambua Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwashukuru na kuwapongeza wadau niliowataja hapo juu kwa kutoa maoni yao mbele ya Kamati. Aidha, namshukuru Mwenyekiti, Mheshimiwa William Shellukindo, kwa kunipa fursa hii ya kuwasilisha maoni haya kwa niaba ya Kamati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru Wajumbe wenzangu wafuatao katika Kamati ya Uwekezaji na Biashara kwa michango yao hata tukaweza kutoa maoni hayo leo. Wajumbe hao ni:-

Mheshimiwa William Shellukindo, Mheshimiwa Salome Mbatia, Mheshimiwa Fatma Said Ali, Mheshimiwa Margareth Bwana, Mheshimiwa Dr. Aaron Chiduo, Mheshimiwa Omar Chubi, Mheshimiwa Ismail Ivvatta, Mheshimiwa Stephen Kazi, Mheshimiwa Aisha Magina, Mheshimiwa Khamis Aboud, Mheshimiwa Freeman Mboge, Mheshimiwa Herbert Mtangi, Mheshimiwa Ali Mussa, Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya na Mheshimiwa Semindu Pawa. (*Makofi*)

Wengine ni Mheshimiwa Mohamed Abdulaziz, Mheshimiwa Dr. James Wanyancha, Mheshimiwa Christopher Wegga, Mheshimiwa Sumri Mohamed, Mheshimiwa Mohamed Ali Said, Mheshimiwa Nazir M. Karamagi, Mheshimiwa Abu T. Kiwanga, Mheshimiwa Balozi Clement George Kahama, Mheshimiwa Hezekiah Chibulunje, pamoja na Mheshimiwa Mbaruk Kassim Mwandoro. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda vile vile kumshukuru Katibu wa Bunge Ndugu Damian Foka, kwa kuiwezesha Kamati kufanya kazi zake bila matatizo na Ndugu Aggrey Nzowa kwa kuihudumia Kamati hii wakati wote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru kwa kunisikiliza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja iliyopo mbele yetu. Ahsanteni sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Kabla sijamwita Msemaji wa Upinzani pengine ningewataja wachangiaji watatu wa mwanzo. Wa kwanza Mheshimiwa Abdillahi Namkulala, Mheshimiwa Ireneus Ngwatura na Mheshimiwa Dr. Milton Mahanga. Hawa watakuwa wa kwanza. Sasa namwita Msemaji wa Kambi ya Upinzani.

**MHE. AISHA P. MAGINA - MSEMADI WA UPINZANI KWA WIZARA YA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge kifungu cha Kanuni ya 43(5)(b) na 81(1) Toleo la 2004, naomba kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Muswada tajwa hapo juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama inavyoelewaka kuwa kilimo ndio muhimili na injini ya uchumi wa Tanzania ambapo zaidi ya asilimia 80 ya Watanzania wanapata riziki zao kwa kutegemea kilimo, wigo na ukuaji wa uchumi na kupunguza umaskini utategemea ni jinsi gani kilimo kitakavyopewa kipaumbele. Hivyo, mfumo wa Risiti za Mazao kwenye Maghala ni njia nyingine yaku-*liberalize* sekta hii na kushirikisha sekta binafsi katika uzalishaji na uuzaji wa mazao ya kilimo, kitu kitakachoongeza tija kwa wakulima na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango huu wa matumizi ya stakabadhi za mazao kwenye maghala kuwa kama dhamana ya kupata mikopo toka kwenye Taasisi zinazokopesha ni ishara nzuri kwa ukombozi wa kilimo katika nchi yetu. Tunaukaribisha utaratibu huu uweze kutumika katika mazao yote ya kilimo na siyo kwa mazao yale ya biashara tu kama ilivyobainishwa katika *Pilot Study* ya mfumo mzima hadi mapendeleko ya kutungiwa sheria. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na ukubwa wa nchi yetu ambayo kila Mkao kunalimwa zao la biashara na kila Mkao uwezo wake kiuchumi unatofautiana, utaratibu mzima wa uhakiki wa maghala kwa ajili ya mfumo kuweza kuanza unaweza kuwa mgumu na utakaotumia gharama kubwa. Hii inatokana na ukweli kuwa maghala yaliyokuwa yanamilikiwa na Vyama vya Ushirika tayari yamebinafsishwa au yanakodishwa, hivyo gharama za ujenzi wa maghala na yatakayokidhi matakwa ya mfumo huu bila Serikali kuweka mkono wake, basi malengo ya kutungwa kwa sheria hii yanaweza kuishia njiani. Vinginevyo wafanyabiashara wale wale wanaofanya biashara ya mazao watakuwa wamepata njia nyingine rahisi ya kujinufaisha kwa kutumia mfumo huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye maandishi ya sheria inaonyesha kuwa utaratibu mzima wa utoaji wa leseni za uendeshaji wa maghala ni rahisi na wa wazi. Kambi ya Upinzani inaomba ni bora iwe hivyo, lakini ukiritimba unaweza kufanya

mfumo huu ushindwe kueleweka na kusababisha kukosa kabisa watu watakuokuwa wanatunza maghala ambao ndio injini ya mfumo mzima wa stakabadhi za mazao zitakazotumika kama dhamana.

Mheshimiwa Naibu Spika, uanzishwaji wa maghala kwa wafanyabiashara binafsi mpaka kuja kukubalika na kupewa kibali kunahusisha utaratibu mrefu wa vibali mbalimbali toka kwa wataalam mbalimbali. Kwa mtazamo wetu, wahusika wanapokuwa wengi zaidi, maana yake utendaji kazi huwa ni wa pole pole kitu kitakachowanyima haki wale wenyewe uwezo mdogo, lakini wako makini katika kufanikisha na kuendeleza mfumo mzima wa stakabadhi za mazao kwenye maghala.

Kama inavyoeleweka, gharama za uzalishaji mazao ya kilimo ziko juu kuliko bei halisi ya kuuzia. Utaratibu huu wa stakabadhi za mazao kwenye maghala unamtaka mkulima au wakulima kuongeza gharama nyingine za usafirishaji wa mazao hadi kwenye maghala. Hivyo, Kambi ya Upinzani inaomba Mheshimiwa Waziri atupe ufanuzi ni nani ana dhamana ya kutoa bei na kuthamanisha mazao hayo ya wakulima na wanatumia vigezo gani, kwani bei halisi na halali ni lazima ufikirie miundombinu ya barabara toka kule yanapozalishwa hadi kwenye maghala.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu kinachohusu mamlaka na uwezo wa Bodi, ibara ya 6(1)(e) kuwa Bodi inaweza kuapisha na kutoa hati ya wito (*summons*) kwa mtu kuja kutoa ushahidi, Kambi ya Upinzani inadhani utoaji viapo, *summons* na taratibu nyingine za kisheria ni kwa mamlaka za kisheria na kulindwa na sheria na sio chombo au mtu yejote anaweza kufanya hivyo na uwezo huo hautolewi kiholela kwa mtu au chombo chochote. Tunashauri kifungu hiki kiangaliwe vizuri ili kuondoa migongano inayoweza kujitokeza na vyombo vilivyopewa mamlaka hayo kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfumo huu kama tulivoarifiwa kuwa umefanyiwa majaribio kwa mazao mawili ambayo ni kahawa na pamba na katika Mikoa ya Ruvuma, Kilimanjaro na Manyara. Kutohana na utofauti wa mila na desturi za makabila ya Tanzania kuchukulia vigezo vya Mkoa wa Manyara na kuvipeleka Shinyanga au Mwanza ni makosa makubwa japokuwa wote ni wakulima wa pamba. Kambi ya Upinzani inashauri sheria hii kwa kuwa ni kwa wakulima wote, isionyeshe upendeleo kwa baadhi ya mazao. Mfano, ni vipi wakulima wa chai na tumbaku sheria imewafikiria na majaribio ya mfumo huu yameonyesha mafanikio gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mamlaka za kutoa uthibitisho wa ubora wa bidhaa hizo au soko lenyewe linawenza kulinganisha ubora huo kulingana na wazalishaji tofauti wa bidhaa hiyo. Ubora wa bidhaa ndio unatoa bei nzuri au ubaya kwa uzalishaji. Kambi ya Upinzani inaomba Mheshimiwa Waziri aweke wazi ni vipi mkulima atapangiwa bei kulingana na ubora wa mazao yake, kwani mtunza ghala sio mtaalam wa kutoa ubora (*Quality Assurance Officer*). Hapa tunaisa Serikali iwe makini yasijie yakajitokeza mambo kama yalivyokuwa yanafanyika kwa wakulima wa tumbaku ambapo wakulima walipangiwa bei za ajabu kwa kigezo kuwa tumbaku yao ni ya ubora wa chini na kuwanufaisha wale wanaouiwa tumbaku hiyo kwa mnunuzi wa mwisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfumo huu wa Stakabadhi za Mazao kwenye Maghala ni mgeni katika nchi nyingi zinazoendelea japokuwa ni maarufu katika nchi nyingi zilizoendelea, na huko ulifanikiwa vizuri kwa kuwa kuna wakulima wakubwa tu. Sasa hapa nchi yetu hapajakuwa na wakulima wakubwa, kilimo bado ni cha jembe la mkono na mashamba ya kilimo bado ni vieneo vidogo vidogo. Kambi ya Upinzani inadhani mfumo huu ungefani kiwa hapa kwetu japokuwa hatuna wakulima wakubwa kwa njia ya Ushirika. Lakini kutokana na makovu waliyoyapata wananchi toka kwa baadhi ya Vyama vya Ushirika katika Mikoa mbalimbali, ni dhahiri dhana hiyo ya Ushirika itakwama japokuwa wahusika wanadai kuwa ni ushirika mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vigumu kusukuma gari wakati mmekaa ndani ya gari hilo hata kama mko wengi, hivyo hata muundo wa ushirika ubadilishwe vipi, jina Ushirika ndani ya fikra za wananchi na wakulima bado ni tatizo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inashauri, mfumo uliokuwa na maeneo mengi nchini India kwa vikundi vidogo vidogo vya wakulima 5 - 20 amba wanaishi katika mazingira na maeneo yanayofanana kwa kuratibiwa na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (*NGOs*), kuvilinda hivyo vikundi vidogo vidogo katika masuala yote yahusuyo taratibu na sheria za mfumo mzima wa Risiti za Maghala. Kwa utaratibu huu, ukubwa wa Watendaji wanaotegemea kodi za wale wale wakulima itapungua na itahamasisha wataalam katika nyanja za kilimo kufanya kazi kwa karibu na wakulima na hivyo dhana nzima ya Risiti za Maghala kwenda sambamba na kupunguza umaskini kwa Watanzania wengi waishio Vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria hii inatungwa kwa makusudi ili kuinua na kuiendezea sekta nzima ya kilimo kwa kuweka mazao kuwa dhamana katika Taasisi zinazotoa mikopo, Taasisi zenye zinafanya biashara. Kambi ya Upinzani inaona ingekuwa ni bora sheria ikatamka wazi kuwa viwango vya riba viwe kati ya asilimia moja na tatu. Hii itatoa msukumo zaidi kwa wakulima. (*Makofii*)

Vile vile, Kambi ya Upinzani inaipongeza nia njema ya Serikali kwa wakulima, kwa kuwa dhana ni nzuri baina ya pande zote, yaani wanaozalisha na wale wanaotoa mikopo, sheria haimkatazi mkulima kupata mkopo toka kwa mtu au chombo chochote. Cha muhimu, mwenye stakabadhi ya mazao kwenye ghala amekubali kwa ridhaa yake, dhana ya biashara huria. Tunaishauri Serikali kuweka kipengele cha kudhibiti biashara huria isiwe holela.

Mheshimiwa Naibu Spika, iliwahi kutokea kwa wakulima Mkoani Ruvuma, baada ya kuuza mazao yao kwa mkopo, mnunuzi alilazimika kuwaambia wayachukue mazao yao baada ya kukaa nayo kwa karibu msimu mzima. Wakati wakulima wanataka kuvuna mnunuzi anasema njooni mchukue mazao yenu ya msimu uliopita kwa sababu yamekosa mnunuzi, vinginevyo wakubali kuuza kwa hasara. Kambi ya Upinzani inashauri kuwepo na kipindi maalum ambacho asasi za fedha zitakuwa tayari zimekwishauza mazao na wakulima wawe wamepata salio la pesa zao, vinginevyo maghala yatashindwa kukidhi matakwa ya uanzishwaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali imekubaliana na matumizi ya Mfumo huu lakini imefanya majaribio kwenye mazao ya kahawa na pamba tu, basi kwa mazao ya nafaka Kambi ya Upinzani inashauri kitengo cha *Strategic Grain Reserve (SGR)* kilicho chini ya Wizara ya Kilimo kianze moja kwa moja kutumia mfumo huu ili Serikali iondokane na aibu ya mara kwa mara ya kukabiliwa na upungufu wa chakula wakati wakulima huzalisha mazao ya kutosha na walangazi huuza mazao hayo nje ya nchi kutokana na udhibiti mdogo. Kwa njia hii, ziada inaweza kuuza mazao hayo kwa Mashirika ya Umoja wa Mataifa kama vile *UNHCR*, *WFP* na wakulima wanawenza kupata bei nzuri tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfumo huu kwa kiasi kikubwa unategemea asasi za fedha. Katika kipindi chote cha majaribio ya mfumo huu Benki kubwa iliyohusika ni *CRDB*, nyingine hazina mtandao wa kuweza kufika hadi Vijijini japokuwa hata *CRDB* mtandao wake unaishia kwenye Makao Makuu ya Wilaya. Kambi ya Upinzani inashauri kuziimarisha Benki za Wananchi kwa kuwa ziko karibu nao zaidi, kwa kulinganisha na Benki za Mijini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoa ushauri na maoni ya Kambi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. (*Makofii*)

**MHE. ABDILAH O. NAMKULALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kwanza ya kuchangia hoja iliyoko mbele yetu. Lakini kwa ruhusa yako kabla sijaanza kuchangia nikuombe nitoe utangulizi kwamba jana Serikali ilinijibu kwamba Walimu Mtware Vijijini wamelipwa na nimepata simu sasa hivi kwamba kesho wanaandamana kumbe hawakulipwa. Sasa nilikuwa naomba watu wa Redio Tanzania wawaambie wale Walimu wasiandamane kwa sababu mimi niko humu na Serikali iko hapa itashughulikiwa habari zao. Waambieni wasiandamane waniachie mimi kwa sababu nimeshaanza kuwasiliana na Mheshimiwa Waziri hapa amesema atalishughulikia. Waambieni sasa hivi wasiandamane kwanza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nianze kuchangia hoja iliyoko mbele yetu kwamba, hoja hii ni nzuri na nia yake, ni nzuri sana. Lakini kama walivyosema wengine kwamba wamefanya mazoezi katika mazao mengine, wangefanya na la korosho tukaona itakuwaje. Maana yake tatizo la korosho mnunuzi ni moja tu, Muhindi. Sasa wewe uhifadhi uuze muda huo huo uuze mwakani, uuze kesho utarukaruka utafika kwa yule yule Muhindi. Kwa hivyo akipanga kukidhibiti hata ukiweka uuze kesho atakudhibiti tu, tofauti na mazao mengine. Mtindo huu sisi tulijaribu. *MAMCU* ilikusanya mazao ya wakulima ikaweka ghalani wakitafuta soko zuri. Walipokusanya kwetu wakulima, risiti walizotupa zilikuwa watatupa fedha Sh.250/= kwa kilo. Lakini baada ya miezi kadhaa walipokuja kutulipa wakatulipa Sh.190/=, Sh. 60/= unyookaji, sijui kuchagua, sijui kufanyaje, kwa hivyo habari hizi sisi tulijaribu tukakwama.

Kwa hivyo tatizo la mkulima wa korosho sio wakati huo wa mavuno, maana yake kukusanya mazao maana yake tayari mavuno. Sasa tatizo letu sisi wa korosho sio wakati wa mavuno, hatuhitaji mkopo wakati wa mavuno. Sisi tunahitaji mkopo wakati wa palizi na kupulizia dawa kwenye mikorosho. Naomba mfanye taratibu tupate mikopo wakati

wa palizi na kupulizia dawa korosho, ule mkopo tukanunua *sulphur* haswa ndio tatizo letu sisi.

Tatizo lingine sisi watu wa korosho ni bei ya *sulphur* kuwa juu sana. Hivi kungekuwa na taratibu za aina yoyote labda ruzuku, *sulphur* kwa mfuko Sh.2,000/= au Sh.3,000/= na ikapatikana kwa wakati, naam!!! Hapo ndio sawa sawa. Tatizo letu sisi ni bei ya korosho kuwa chini. Hivi labda *Price Stabilization Fund* mngeianzisha ili zao la korosho likawa kila moja Sh.2,000/= hadi Sh.3,000/= bila ya kuyumba kila mwaka, naam!!! Lakini tuzalishe korosho sisi kwa shida wakati wa kuuza ndio mchukue korosho zetu mtuambie fedha mtatupa, lini? Mpaka mkienda kuuza baaa!!! Maana kijana akirudi sokoni lazima anaulizwa na wazee *jengo lose limekwacha*. Korosho ziko wapi? *Japa twete*. Korosho wameshachukua.

Kwa hivyo mzee anategemea fedha, *ji hela*. Yaani hela *jikapali baa!!* Korosho wamechukua, hela hawakukupa mpaka mwakani, sijui mpaka lini, hiyo haiwezekani kwetu sisi. Sisi tukupe korosho na kutupa fedha. Huo mtindo wa kukusanya, halafu ukauze sijui ukafanyeje upeleke wapi sijui halafu sisi utuachie karatasi. Tafuteni utaratibu mzuri kwenye zao la korosho. Huu nadhani hautufai. Sisi tukikupa korosho tupe fedha zetu.

*Sulphur* mfanye taratibu ipatikane kwa wakati na bei nafuu mfuko Sh.2,000/= au Sh.3,000/=, mikopo hiyo wekeni taratibu tupate wakati wa kupulizia na kupalilia maana ndipo tutakapohitaji mikopo na bei iwe nzuri Sh.3,000 au Sh.4,000/= kwa kilo, hapo mmemaliza kazi kwenye korosho. Vinginevyo nadhani Muswada huu sio wetu, labda sio kwa zao la korosho, maana kwa kweli hautatufaa. Kwa hivyo mkifanya marekebisho, nitaunga mkono. Hii hoja. Lakini ikiwa hivi itabidi nikawaaulize wale Wamakonde kwamba jamani si mmesikia, nikaunge mkono maana wasije wakaniadhibu. Ahsanteni sana. (*Makofî*)

**MHE. IRENEUS N. NGWATURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia Muswada huu ulio mbele yetu. Lakini kwanza kabisa kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kuchangia katika Bunge lako Tukufu, naomba na mimi niungane na wenzangu kutoa rambirambi zangu kwa familia za Marehemu Balozi Ahmed Hassan Diria, Mbunge mwenzetu na Balozi Paul Boman, ambaye kwa kweli ni mmoja kati ya watu mashuhuri sana katika kuendeleza ushirika katika nchi hii. Naomba Mwenyezi Mungu aziweke roho zao mahali pema Peponi. Amen.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, naomba nichukue nafasi hii nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na Watendaji wote walioshiriki katika kuandaa Muswada huu. Hongereni sana. (*Makofî*)

Tatu, vile vile napenda nichukue nafasi hii, niwapongeze wakulima wangu wa kahawa wa Mbinga kwa kukubali kujiunga katika utaratibu huo na mpaka ukawa ni mmoja kati ya mifano ya kuwezesha Muswada huu uweze kuletwa hapa Bungeni. Ni

matumaini yangu kwamba wale wengine ambao walisitasita watajiunga ili waweze kunufaika na utaratibu huu mpya ambao leo hii tunauundia sheria.

Baada ya hapo ningependa nianze na kuunga mkono Muswada huu moja kwa moja. Lakini pamoja na hayo kama Waheshimiwa Wabunge walivyosema hapa kwamba, kwa kweli Muswada huu ni Muswada mpya ambao unatakiwa uchukuliwe kwa uangalifu kwa sababu mazao ya aina mbili tu yasitufanye tuone kwamba huu Muswada utaweza ukafanya kazi katika sehemu zote. Kwa hiyo, hii ni tahadhari. (*Makofi*)

Lakini, lingine la jumla ukiangalia sana Muswada huu hauko wazi. Kama wakulima watakuwa na mkataba na mfumo wenyewe au na utaratibu huu katika kuboresha masoko na uzalishaji kwa mazao ya kilimo hauko wazi, unakuwa unaelea wenyewe, wala haugusii maeneo mengine kama sheria za Bodi mbalimbali. Kwa hiyo, mimi nalionna hilo ni tatizo kwa sababu unaweza ukachukuliwa juu juu tu. (*Makofi*)

La tatu la jumla, sheria hii haionyeshi mahusiano jinsi mfumo wenyewe utakavyoendeshwa katika maeneo mbalimbali kwa kuzingatia mazingira ya kijiografia pamoja na mazao kama ulivyosema huko awali kwamba usije ukachukuliwa kwa ujumla, vinginevyo utashindwa kuleta yale matunda ambayo yametarajiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa katika kupitia Muswada huu ukiangalia ibara ya tisa inaonyesha njia za mapato ya Bodi. Moja ni Bunge mimi sina tatizo; lakini la pili, linaeleza leseni ambazo kwa kweli atakayetozwa hatimaye ni mkulima. Ukaguzi na usimamizi atatozwa mkulima yule yule. Udhibiti wa vitabu vya *receipts* ya hayo maghala atatozwa mkulima. Sasa mimi naogopa kwamba matokeo yake mkulima ndiyo atabebeshwa mzigo mkubwa sana. Kwa hiyo, ni dhahiri hapa kinachojionyesha ni kama vile tunataka kutengeneza ajira hapa katikati kwa watu wengine siyo wakulima.

Kwa hiyo, mimi nashauri tuangalie labda Serikali kama kweli ina nia ya kuboresha kilimo, basi ibebe huo mzigo badala ya kuupeleka mzigo huu kwa wakulima moja kwa moja. Vinginevyo sheria hii itakuwa ni mzigo badala ya kusaidia uboreshaji wa mazao ya kilimo ya biashara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda sehemu ya nne, pale kuna masharti ya kuendesha maghala chini ya utaratibu. Mimi nitatoa mfano wa kahawa. Tuna maghala ambayo yako Vijijini yanayoshughulikia kuweka kahawa Vijijini. Toka hapa kahawa inapelekwa kwenye kiwanda cha kukoboa kahawa ambako nako kuna maghala. Ukipakobo kahawa inatoka hapa inapelekwa kwenye maghala mengine yako Makambako, yanangojea manunuzi na huu utaratibu umekuwa hapo tangu siku za nyuma na tumekuwa tukiulalamikia kwamba kwa kweli ndiyo unasababisha gharama kubwa sana.

Sasa mimi sielewi hapa watatusaidia vipi. Kuna sababu yoyote kuhusiana na mfumo huu kuwa na maghala katika ngazi hizo tatu? Hii sheria inasemaje? Kama lengo letu ni kuboresha, kwa nini tusifutilie mbali ikiwa kwamba tunakuwa na ghalaa pale

ambako kutakuwa na nafasi ya kusindika mazao, kwa mfano kukoboa na toka hapo wanunuzi waende hapo badala ya kumpa tena mzigo mkulima? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ningeomba niangalie ibara ya 17 (1) inasema kwamba, Bodi inaweza ikazuia mtu au taasisi isipate leseni ya kuendeshea shughuli hizi. Sasa picha ninayopata hapa ni kwamba, ikiwa wakulima hawatafurahishwa na urasimu huu, ni dhahiri kabisa sheria hii itashindwa kufanya kazi. Kama kutakuwa na urasimu wa aina yoyote ambaa utawafanya wakulima wasiwe na kivutio cha kufuata mfumo huo ni dhahiri kabisa kwamba sheria hii itabaki kwenye vikapu.

Sasa naishauri Serikali iangalie kwamba mfumo wenyewe unakuwa ni kivutio kwa wakulima kupenda kupeleka kahawa yao kwenye maghala hayo. Kama itakuwa ni gharama ujue kabisa kwamba hawatapeleka, vinginevyo wasiwasu hapa ni kwamba inaweza ikafikia ikawa ni lazima, kitu ambacho kitakuwa kinashindana na dhana ya soko huria. Ukienda ibara ya 18, kuna masharti ya kutoa leseni. Mimi nina wasiwasu kama haya masharti yanaweza yakawa ni kichocheo kwa sababu kama atakayemiliki maghala haya anataka kupata wateja wengi walete kahawa kwenye maghala hayo, basi lazima gharama zake ziwe nafuuu, zikiwepo gharama kubwa, ujue basi itakuwa ni tatizo, watu watasita kupeleka mazao yao kwenye maghala hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine kama sehemu ya hitimisho, ukiangalia Muswada wenyewe hasa kwenye ibara ya 61 (1) inazungumzia suala la bidhaa zinazoharibika au bidhaa hatari. Kule Mbanga kuna maghala mengi tu ambayo yalikuwa yanamilikiwa na *MBICU* ambayo iko chini ya Mfilisi. Maghala haya yana uwezo wa kuhifadhi kwa wakati mmoja zaidi ya tani 50,000 za kahawa. Sasa hivi yako katika hali mbali sana. Asasi inayosimamia ni Mfilisi. Kinachotushangaza kidogo na ningeomba Serikali ilitazame hilo, tumeputa manung'uniko kutoka kwa wakulima kwamba Mfilisi sasa hivi ameruhusu ujenzi wa Kituo cha Mafuta kwenye viwanja hivyo vya maghala haya. Sasa sielewi Mfilisi anapokabidhiwa mali ya mfilisiwa, anaruhusiwa kufanya mabadiliko yoyote!! Nalo hili lingeangaliwa kwa sababu sasa linajenga mazingira ambayo hayaeleweki sana.

Kwa kumaliza, naomba nihitimishe tu kwa kusema kwamba utaratibu huu ili ufanikiwe, lazima pawepo na elimu ya kutosha kwa wakulima. Vile vile, lazima mahusiano ya bei kwa mkulima pamoja na suala la pembejeo na soko viwe na mtiririko ambaa utaeleweka kwa wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo naomba kusema tena naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia. (*Makofi*)

**MHE. STANLEY H. KOLIMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa naomba nikupongeze na kukushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Nilikuwa naomba nijiunge na wenzangu katika kutoa rambirambi zangu kwa wenzetu waliotutangulia mbele ya haki. Mwenyezi Mungu aziweke roho zao mahali pema Peponi. Amen.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naomba niipongeze Wizara ya Ushirika na Masoko kwa kuleta Muswada huu mzuri wa kihistoria. Nasema Muswada huu ni wa

kihistoria kwa sababu nchi hii tunajenga sasa hivi uchumi wa soko, hatujengi uchumi wa kupanga kama zamani. Kwa hiyo, katika hali hiyo lazima ujenge Taasisi maalum zinazohusika katika kujenga uchumi wa kisasa ambaa unaambatana na soko. Kwa hiyo, hii ni moja ya mkakati wa kuhakikisha kwamba wakulima wanakuwa na Taasisi ambazo zinaweza kuwasaidia katika kujenga uchumi. (*Makofî*)

Kwa hiyo, naomba niwakumbushe kidogo kwamba miaka ya nyuma wakati Ushirika unaanza kulegalega, palikuwa na utaratibu wa Benki kukopesha wakulima na Vyama Vikuu, lakini nao walikuwa wanakusanya mazao, Benki inakuja inatathimini pale kama mazao kweli yapo kwenye godauni na hii iliwezekana kwa Benki kutoa mikopo kwa wakulima. Kwa hiyo, hii sioni kama ni ajabu isipokuwa hapa sasa inaimarishwa na kuweka sheria maalum, tuliwahi kufanya huko nyuma. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi naunga mkono sana sheria hii kwa sababu sheria hii inatoa dirisha lingine la kupita. Yako madirisha mengi tu. Ukiona Serikali imeweza kuweka utaratibu ule wa *Export Guarantee Scheme*, upo utaratibu wa mifuko ya pembejeo, uko utaratibu wa *SACCOS*, uko utaratibu wa *SELF* na utaratibu mbalimbali katika nchi hii. Lakini sasa hii ni moja ya mpango au mfumo wa kuweka dirisha lingine zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi sioni kama una matatizo, ukiukataa utaratibu huu unakataa ukweli kwamba wakulima wadogo ambaa hawana dhamana kabisa wabaki maskini. Maana utaratibu mwingine wowote uliokuwepo lazima utoe kitu cha kuweka rehani, *collateral* na kadhalika. Lakini hii mtu anaweza kujivuna, anaweza kujiweka kifua mbele kwa sababu ana mazao yake na hayo mazao yake anaweza kuyatumia kupata mkopo. Kwa hiyo, mimi sioni tatizo liko wapi, nausifu utaratibu huu. (*Makofî*)

Halafu licha ya hiyo mfumo huu unaweza kumaliza matatizo ambayo tunayo. Kwa mfano ukichukua kwenye Wilaya ya Ludewa, unakuta mazao mengi wakulima wanalima mahindi kwa wingi sana na wanauza mara baada ya kuvuna. Kwa hiyo, utakuta baada ya miezi mitatu au minne ambapo wangeweka kwa muda mfupi au kwa muda wa miezi miwili au mitatu wangeweza kupata bei nzuri. Lakini hawawezi kufanya hivyo kwa sababu hawana uwezo wa kuhifadhi. Kwa hiyo, siku zote wao watakuwa wanalima na kuuza kwa bei ya chini sana. Lakini kwa utaratibu huu wanaweza kuweka kwenye godauni au kwenye kwenye ghala ili kuweza kungojea bei nzuri inapokuja.

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna mpango au utaratibu ama mfumo ambaa hauna kasoro. Lakini moja ya hii inaweza kusaidia kuwapa wakulima bei nzuri. Lakini siyo kuwapa bei nzuri tu, vile vile kuwasaidia mpaka kufika kwenye soko kwa sababu watakuwa na uwezo, wanawezeshwa kwa utaratibu huo. Kwa hiyo, mimi naomba nikubaliane na kuunga mkono huo utaratibu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vile vile utaratibu huu una matatizo yake ya kiutawala, usimamizi na udhibiti. Nimeona katika muundo wa kwetu hapa kutakuwa na matatizo katika Taasisi zenyewe kwanza za mikopo. Utakuta kwamba karibu taasisi

nyingi za mikopo hazipo Vijijini. Kwa hiyo, hata kama watu wana nia nzuri, lakini huko Vijijini *Financial Institution* ambayo inaweza kuwapa hiyo mikopo haipo. Kwa hiyo, mfumo huu ni mzuri, lakini unatakiwa uambatane na Taasisi nyingine ili uweze kuwa mfumo unaoeleweka na unaweza kuwasaidia wakulima. Hakuna Taasisi za fedha huko Vijijini. (*Makofit*)

Kwa hiyo, unakuwa na Chama chako cha Msingi kizuri, au Chama Kikuu kizuri, lakini Taasisi hazipo. Lakini kwa sababu mmesema kwamba kitu cha kwanza itakuwa hiyo. Lakini siyo hilo tu, kumekuwepo na matatizo makubwa hasa pengine, njama za namna ya kutathimini mazao katika *godown* hapo naona napo pana matatizo. Kwa sababu nakumbuka miaka ya nyuma Vyama vingi vya Msingi na hata Vyama Vikuu vilikuwa vinapata matatizo namna ya kulinganisha mazao kati ya Chama cha Msingi au Chama Kikuu na Shirika la Serikali au Mamlaka za Mazao.

Kwa hiyo, hapo katikati pana ubishi. Watu wa Vyama au wakulima watakuwa wanasema kwamba mazao niliyoleta ni kilo 40, mtu wa *godown* naye atasema kwamba umeleta pungufu ya kilo 20. Kwa hiyo, ni nani hapa atakayesimamia kutatua mgogoro utakaojitokeza kati ya mkulima na mtu wa godauni? Kwa sababu hawa wote wana *interest* zao pale! Wanasema labda wakati wa kuja, mazao yamepungua njiani, kuna upungufu na kadhalika. Kwa hiyo, nani atakayekuwa hapa katikati? Hilo naona litakuwa ni tatizo kufanya *reconciliation* ya Bodi hizi mbili. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wameshaeleza wenzangu lakini inaonekana kwamba kama kweli Serikali itakuwa *serious* kusaidia kujenga magodauni, maana hawa watu wanaojenga magodauni binafsi wanaweza wakawa na *interest* ya kujenga maeneo yale tu ambayo yana miundo mbinu inayoeleweka siyo kwenye maeneo mengine ambayo miundombinu yake ni mibovu. Kwa hiyo, labda Serikali ikiingia huko itakuwa imesaидia.

Hata haya magodauni kuna historia katika nchi hii kwamba magodauni mengi sana ya pamba yalikuwa yanachomwa moto, watu wanayaunguza mazao. Sasa sijui kama usalama wake utakuwepo! Mnawenza kusema labda kuna Bima (*insurance*) ya mazao, lakini mambo haya yanapokwenda kwenye Bima kama inaonekana moja kwa moja kwamba hiki ni njama Bima nazo zinakataa kwamba sisi hatuwezi kulipa fidia hii, wakati tunajua ni njama. Kwa hiyo, utakuta kutakuwa na matatizo. Kwa hiyo, *security* ya kitu hiki tunatakiwa kujua.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile hizi *documents* zitakazotumika zижлике, maana siku hizi kuna wajanja. Nimeeleza kwamba matatizo mengi yanatokana ya kusimamia siyo sheria. Sheria ipo nzuri sana. Lakini siku hizi kuna *forgesies* nyingi sana. Maana watu wana-forge hata *cheques*. Kwa hiyo, labda kuwepo na utaratibu, siyo vikaratasi bandia tu, hapana. Pawe na vitu ambavyo vinaweza kueleweka kwamba hii ni *certificate* ya *consignment* au *certificate* ya mazao ambayo siyo haya tuliyokuwa tunatumia sisi kwenye Vyama Vikuu. Nadhani ile ya kusafisha mazao,. Nadhani kuwe na kitu ambacho kinalelewaka, vinginevyo tutapata matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni elimu yenyewe. Nimefurahi sana Waziri amelizungumzia hapa kwamba watakuwa wanajaribu kuwa-*train* watu wa kwenda Vijiji kuelezea mambo ya ushirika mpya na hiyo *reform* ambayo mnaifanya. Kwa hiyo, kwa kweli hili labda litasaidia sana katika kujenga hii elimu, inatakiwa sana. Kama ndugu yangu mmoja alivyozungumza hapa sasa hivi, kwamba kwenye korosho watu hawaamini. Lakini elimu tunayoizungumzia hapa mmeizungumzia hiyo, wataelezwa wale kwamba tunawapa *certificate* hii. Hiki ni kitu cha thamani sana uweke nyumbani usubiri. Kwa hiyo, haya ndiyo mambo kama yatakuwa na matatizo. Kuna mambo mengine *of course*, labda kama walivyosema wenzangu kwamba mfumo huu hasa kuwapata wataalam maana yake hapa kuna Bodi ya Makongoro inayohusu mambo ya *stores*. Sasa kuwapata hawa watu wenye *qualifications* za hii kitu ni ngumu sana kwa sababu mmesema *registered Warehouse*. Kwa hiyo, kutakuwa na *registered* hawa *store*. Kwa hiyo, nayo naona ni *challenge* kubwa kwa nchi nzima kufanya *training* na mambo haya yaweze kuwa sawa sawa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine nilikuwa nafikiri kwamba sasa hivi Wizara yetu imesimama vizuri, mimi kwa kweli ninajaribu kila siku kuzunguka kusoma namna mnavyotaka kuingia kuweka ushirika sawa sawa, nafikiri sasa mmeanza nawapongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo nawaondoa wenzangu wasiwasi kabisa kwamba sasa hivi ushirika tunaouzungumzia ni mpya, maana tusiwe bado tunaendelea kuzungumzia ushirika yaliyotokea huko nyuma. Kuna mzungumzaji mmoja amezunguka hapa kasema Mashirika ya Umma mengi yamekula hela nyingi. Sasa kuliko haya ya kumsaidia mnyonge, hakuna nyingine ya kufika ng'ambo ya pili bila hapa katikati kuliwa na mamba lakini ni ushirika tu. Mamba akiona watu wengi wamekaa pamoa wanavuka anakimbia.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hivyo, ushirika hoyee!! Naunga mkono hoja hii. Ahsante sana. (*Makofi/Kicheko*)

**MHE. PHILEMON NDESAMBURO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie katika Muswada huu ambao ni ukombozi wa Watanzania. Kwanza, niwashukuru walioandaa Muswada huu, maana yake kitu kinacholeta ukombozi katika nchi lazima tuwashukuru waliofanya kazi hiyo. Hii *bill* ambayo inazungumzia mambo ya *Warehouse Receipts* ni mfumo uliokuwepo kwa miaka mingi katika dunia ya sasa, lakini unataka utaalami namna ya kutumia *Warehouse Receipt*. Ni ukombozi kwa sababu mkulima badala ya kuweka ardhi yake rehani ili apate pesa na kupoteza ardhi yake kama hakuweza kuikomboa sasa anatumia kile alichonacho ambacho ni mazao yake. Kwa hapo unamlinda mkulima asipoteza ardhi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona huko nyuma *Cooperative Societies* ambao walikuwa na mashamba, hata Viongozi wengine wameyanunua na kuwadhoofisha zaidi wakulima. Lakini *bill* hii inazuia, lakini inamfanya mwenye mazao aweze kuyauza na aweze kuyatumia na ku-*raise* pesa za kumsaidia. (*Makofi*)

Labda kuna matatizo kwa sababu hatujailewa vizuri hii *bill*. Kwa kweli hatujailewa vizuri kwa sababu unapoweka mazao yako katika *Warehouse* wanasema unapata *negotiable receipts* ambayo unaweza kuipeleka kwa mtu mwenye pesa akainunua halafu akakupa fedha. Si lazima uende Benki. *Bill* haijasema lazima uende Benki, kwa yeote yule ambaye anaweza *ku-provide finance*. Haijasema Chama cha Msingi kisiwe na *Warehouse*, wala hakijasema mkulima asiuze peke yake moja kwa moja. Hii ni *provision* ya kumsaidia mkulima. Ni njia mojawapo kama alivyosema Mheshimiwa Kolimba, ni *another door, another window* ya kumfanya Mtanzania aweze kuinuka aachane apate utajiri kidogo. (*Makofi*)

Kwa hiyo, hizi *avenues* ambazo zinamsaidia mtu apate fedha, *MKUKUTA* sijui, tulikuwa tunazungumzia mambo ya *MKUKUTA* lengo la hii ni *MKUKUTA*, kusaidia kuondoa umasikini. Huwa sipendi sana kusema Watanzania ni maskini kwa sababu ni matusi. Watanzania siyo maskini, nchi hii ni tajiri. Lakini kuwasaidia waweze kupata chakula na mlo wao, huu ni ukombozi mkubwa watu hawaangalii, lakini yako matatizo kidogo katika *bill*. Hatujasema mtu mwenye *Warehouse* ye ye kazi yake ni *ku-store* tu au anaweza kutumia hata *receipts* zile kuuza, nani anaiza haya mazao? Yanaka kwenye *store* wewe unachukua? Nimesikia kuchukua *receipt* ukaiweke nyumbani, ukiweka nyumbani haitakuwa na faida na wewe. Hii *negotiable receipt* inataka ukipata, ukii-*negotiate* upate fedha. Kwa hiyo, hutaiweka nyumbani, lazima ui-*negotiate* upate fedha uweze kuendelea na biashara zako za kawaida. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuelewe Tanzania ya sasa siyo tena ile Tanzania ya kufunga macho. Sasa hivi tuko *open market*. Tuko katika soko huru la dunia. Mawazo ya ujamaa tuachane nayo tunapokuwa katika hili. Kama tunarudi katika ujamaa na *bill* hii ipo ni kwamba tunajifunga, tunajidanganya. (*Makofi/Kicheko*)

Dunia ya sasa ni *competition!* Ni lazima tuanze kuwafundisha Watanzania wawe wafanyabiashara. Tunataka fedha zisambae kwa kila mtu hata kama unalipa *rent*, unalipa *interest*, ni mpangilio wa kupanga fedha. Siyo ukae nazo wewe unalima hutaki kulipa kodi. Lazima usambaze fedha kwa watu wote wa Tanzania ili tujue zinachangia katika nchi nzima. *That is the whole concept of this bill.* Ni kujaribu kufanya Watanzania waweze kufaidika hasa wakilima wadogo wadogo. Ukienda Kibaigwa wakati wanapovuna mavuno, utakuta mahindi yote yanachukuliwa na wale watu wenye fedha. Lakini nafasi ya mkulima kuweza kuingia katika soko la dunia ilikuwa hakuna. Lakini *this is the only opportunity* ya mkulima kuweza kwenda katika bei ambayo iko katika Soko la Dunia. (*Makofi*)

Lakini walanguzi watakuwepo wengi sana katika hili. Walanguzi watakuwa ni wengi kwa sababu mimi naweza kumwambia mtu wewe una magunia yako 1,000 umekwishayaweka kule kwenye *Warehouse* nakupa bei ninayotaka lakini najua mimi nitakapouza nitapata nini. Ndiyo maana ya *negotiable receipts*, maana mimi nikishaichukua yule mkulima sijui nilichompa nimempa.

Lakini sasa mimi naweza kwenda kuuza kwa bei yoyote ninayotaka. Sijui hii *bill* itamzuiaje mtu ambaye ana-*negotiable receipts* ambaye ana haki, atakuja kumlipa yule

mtu ambaye amepewa *only 65%*. Maana yake ndiyo tunasema ukipeleka Benki unapata asilimia 65. Lakini akija kuniletea ile *receipt* yake mimi nikainunua labda nitainunuahata zaidi ya hapo, lakini yule mkulima hatapata ile bei ya *world market* kwa sababu mimi ndiyo nitakuja kufaidika ambaye nimenunua ile *receipt*. Kwa hiyo, labda ndiyo pungufu moja katika hii *bill*, sasa sijui tutaifanyaje. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni biashara, watu lazima wawe na elimu ya kibashara. Tunapozungumzia hili, tuwe na uhakika, tuna elimu ya kibashara, tusifikirie mambo ya ujanja ujanja, uwe unajua. Kwa sababu usipofanya hivyo, utajikuta unaingia kwenye hasara kubwa au hutaelewa hii ina maana gani. Maana yake hii ni biashara jamani! Waheshimiwa Wabunge hii ni biashara ambayo ni lazima tuiangalie na tuwe na fikra za kujua tunataka kupeleka pesa kwa wananchi ili waweze kupata pesa za kuendeleza biashara zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekwishesema ya kuwa Serikali inajiondoa katika biashara, lakini katika hili, unakuta kuna Bodi ya Serikali. Tuna urasimu, tunasema Waziri naye ataingilia. Mfanyabiashara akitaka kufanya biashara, hataki kuingiliwa jamani!

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima tuelewe, tutatenganishaje hii. Maana yake mfanyabiashara akiwekewa urasimu na Bodi inayomtawala, na Waziri ataweka *regulations* mnazoziona katika hii *Bill*. Biashara huria, mimi leo nataka kufanya biashara, labda mpaka nikamwone Waziri kesho bei itakuwa imeanguka. (*Makofî*)

Labda tutafute *flexibility* tutafanyaje katika hizi *Warehouse Receipt* watu watatumia namna gani ili sizije zikaleta matatizo. Elimu ya hawa watu wenye *Warehouse* maana yake *Warehouse Receipt* hii ninavyoiona, naona kama *Bill of Lading* ambayo ni *negotiable* unaweza ku-transfer one person to another, ili akafanyie biashara na hizi *Warehouse Receipt* nilivyosoma, naona iko hivyo hivyo. Unaweza ukai-transfer ukampa mtu na mtu akaenda nayo mwininge akaenda huko.

Inatakiwa elimu ya kuwafundisha hawa watu, au watapata hasara sana katika mazao yao. Ni lazima elimu iwe ni msingi wa kuanza hizi *Warehouses* na mimi nadhani tumekuwa tunazungumzia mambo ya ushirika. Ushirika nadhani watakuwa ndiyo wa kwanza kuwa na hizi *Warehouses* kwa sababu wataweza ku-benefit kuliko mtu mwininge yejote. Na wakulima kwa sababu sisi nchi hii hatuna wakulima wakubwa ambao tunao tayari wanaweza kuanza. Mfumo huu ulianzia huko Marekani au kote mnakosema ilikuwa ni kwa ajili ya wakulima wakubwa waweze kupata mikopo ya kuendeleza mashamba yao bila kuweka mashamba yao rehani. Kiswahili cha Wachaga kibovu. Sisi hatukutoka Pwani bwana. (*Makofî/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi nadhani ni lazima jambo la elimu kwa hawa watu wenye *Warehouse* liwe ni la msingi sana. Vile vile, madaraka ya mtu mwenye *Warehouse* naona katika *Bill* yamewekewa matatizo mengi sana. Ukienda kwenye kifungu cha *function* ya *Board* ya hii kitu, inaleta sheria nyingi mno za kupita kiasi ambazo kwa kweli atashindwa labda hata kufanya kazi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nadhani niseme huu ni ukombozi. Watu wasione kama kuna unyanyasaji au labda kuwaonea wakulima wadogo. Hii itamsaidia sana mkulima mdogo na itawasaidia Watanzania kuwaondolea umaskini na kupata pesa za kufanya kazi zao za ukulima bila kuweka rehani mashamba yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo machache, naomba kuunga mkono hoja mia kwa mia. (*Makofi*)

**MHE. DR. DIODORUS B. KAMALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Muswada huu muhimu na napenda niipongeze Serikali kwa kuleta Muswada huu ukizingatia ukweli kwamba Mheshimiwa Waziri miaka miwili iliyopita alijibu swali langu hapa Bungeni kuhusiana na uanzishaji wa *Warehouse Receipts System* na akaniahidi kwamba kabla ya Bunge hili halijamalizika, basi angeleta Muswada huu. Kwa hiyo, naomba kumpongeza kwa kutekeleza ahadi yake kwa vitendo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme kwamba ukiwa ni mtaalam wa kutumia nyundo, unaweza ukafikiri kwamba kila tatizo litakalojitokeza, basi kwa kutumia nyundo unaweza ukapata ufumbuzi. Vile vile ukiwa wewe ni mtaalam wa kutumia kalamu, basi unaweza ukafikiri kwa kutumia kalamu yako unaweza ukapata ufumbuzi wa kila tatizo. Ukiwa na mtazamo wa kuamini katika jambo moja kwamba ni jibu la kila tatizo, basi wewe unakuwa unafikiri kwa utaratibu amba siyo wa kimfumo. Kwa hiyo, pamoja na ukombozi tunaouona katika mfumo huu tunaouanzisha, lazima tuje kwamba yako mambo mengine ambayo lazima tuyatazame ili kuhakikisha kwamba mfumo huu unakuwa wa manufaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaendelea, nimepewa taarifa leo hii kwamba katika Jimbo langu maeneo ya Kyaka, kumetokea upopo mkubwa na Kijiji kimoja migomba yote iko chini na baadhi ya majumba yameanguka. Lakini vile vile nimepewa taarifa kwamba barabara kubwa inayokwenda kule Kata ya Kanyigo, Kata ambayo ina wasomi waliobobea katika fani mbalimbali, haipitiki na wananchi wanalahazimika kuzunguka kupitia maeneo mengine. Sasa kwa kuwa Waheshimiwa wahusika wako humu, basi niwaombe basi baada ya hapa waweze kuyafanya kazi hayo wakati naendelea kuchangia Muswada huu ili hata hayo maghala ya mazao tunayoyajenga yawefe kupita katika barabara hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendelee kuchangia kwa kusema kwamba, mfumo huu lazima tuuangularie kwa mapana. Kwanza, tunapoongelea kuwa na maghala, lazima ujenzi wa maghala uende sambamba na kuwepo kwa masoko. Kwa mfano, unapomwambia mkulima wa mahindi kwamba ataweka mahindi yake kwenye ghala na wakati soko likiwa zuri atauza, haina maana kama mkulima huyo wa mahindi hajawezeshwa kusaidiwa kwa kuwepo soko la kuuza mahindi yake.

Kwa hiyo, soko kubwa tulilojenga pale Kibaigwa nadhani tusiishie pale, basi twende Tanzania nzima tuhakikishe kwamba tunakuwa na masoko mbalimbali ya namna

hiyo ili tunapoongelea kwamba tuna mfumo wa kutumia stakabadhi za maghala, basi wakati huo tuwe tunamwezesha mkulima huyu huyu kuweza kupata soko la uhakika pale anapoamua kuuza zile bidhaa zilizo katika maghala. Ndiyo maana nikasema, ni vizuri kuangalia mfumo huu kwa mapana yake. Kwa hiyo, tuisuangalie peke yake, tujaribu kungalia na mambo mengine. Jambo moja ni hilo kwamba kuwe na masoko ya uhakika ili haya mazao hata kama yako kwenye ghala lazima siku moja tumwekee utaratibu kuwa anapoamua kuuza mazao hayo basi awe na soko. Hilo ni moja ambalo ningependa kulisisitiza.

La pili ni kwamba, tusiongelee tu kuhifadhi mazao kwenye maghala, lakini tuongelee vile vile kuongeza ubora wa mazao hayo kwenye maghala, kwamba tunahifadhi mazao ya namna gani kwenye maghala. Ndiyo tuseme basi unapoongelea kuwa na maghala ya kuhifadhi mazao, lazima wakati huo huo uongelee utaratibu wa kuongeza ubora wa mazao yanayohifadhiwa. Kwa sababu mazao yanayohifadhiwa kwenye maghala yakiwa na thamani kubwa zaidi, mkulima ana uwezo wa kunufaika zaidi pale anapoamua kuuza mazao yake. (*Makofsi*)

Sasa hivi changamoto kubwa iliyo mbele yetu, yapo mazao kama ndizi, kuna utaalim sasa hivi ambao ukiutumia unaweza ukahifadhi ndizi kwa zaidi ya miaka minne, mitano hadi sita. Ukienda kule Karagwe, Sir George anaeleta, yupo kijana mmoja ana kiwanda kidogo, anajitahidi kubadilisha ndizi kuweza kuzihifadhi zikadumu kwa muda mrefu. Ndizi ni zao kubwa kwa Mkoa wa Kagera. Kwa hiyo Muswada huu wa mazao tunapouongelea, basi tufikirie ni kwa jinsi gani tunaweza tukawezesha ndizi hizi zikaweza vile vile kuhifadhiwa kwenye maghala kwa sababu tatizo la ndizi kuna msimu ambapo zinakuwa nyingi na msimu huu zinapokuwa nyingi bei inaporomoka na bahati mbaya huwezi ukazihifadhi katika hali ya kawaida.

Lakini tukiweza kufikiri na tukaogopa kusinzia kwa muda mrefu, tukasinzia muda kidogo, muda mwangi tukautumia kufikiri, basi tunaweza tukamsaidia mkulima vizuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ambayo lazima tuifikirie vile vile ni kwamba, tunaposema itabidi haya mazao yawekewe Bima, lazima tuijulize kwamba mashirika tuliyonayo sasa hivi ni mangapi? Yanatoa *crops insurance?* Jibu lake hakuna. Lakini leo hii tunapitisha Muswada ambao tunasema lazima hayo mazao yatakayokuwa kwenye ghala yawe yamewekewa Bima. Lakini Mashirika tuliyonayo sina uhakika ni Mashirika mangapi yapo tayari kutoa Bima kwenye maghala, nina uhakika na *National Insurance Corporation* kwamba ilikuwa ina utaratibu wa kuweka Bima ya Kudhamini Mazao Kwenye Maghala. Lakini nina uhakika vile vile inapotokea mazao hayo yakaibiwa hawalipwi. Hadi leo hii wananchi wa Buyango Chama cha Msingi waliweka Bima mazao yakaibiwa yenye thamani ya Shilingi milioni moja, hadi leo hii tunavyoongea *National Insurance Corporation* wameshindwa kulipa Bima yenye thamani ya milioni moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tatizo lipo, sote tuliomo humu tuna wajibu wa kufikiri kwamba tunafanyaje ili kuwezesha kuwa na Makampuni yatakayoweza kutoa

Bima kwa haya mazao tunayoongelea kwamba yatapewa Bima. Lakini wakati naendelea hapa, zipo taarifa zimetoka na kwa kuwa taarifa hizo hazijakanushwa, basi ni sahihi kwamba Mheshimiwa Rais amevunja Bodi ya Kahawa na kwa kuwa hazijapingwa, basi tunaweza tukachukulia kwamba ni sahihi Bodi hiyo imevunjwa, labda kama hajavunjwa tutapata ufanuzi baadaye. Lakini matarajio yangu ni kwamba Bodi nyingine zitawenza kuundwa haraka kwa sababu ni vizuri tukawa na chombo muhimu cha kusimamia zao la kahawa na si vizuri kujifagilia mwenyewe, vinginevyo ningeomba basi nifikiriwe kwenye Bodi hiyo ili iweze kusimamia vizuri zao la kahawa. Lakini si utaratibu mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yangu hapa ni kwamba, tulipopitisha Sheria ya Bodi mpya ya Kahawa hapa, tulisema kwamba itakuwa na *Stabilization Fund* kwa nia ya kwamba pale bei ya kahawa inapopomoka, basi ule mfuko uweze kusaidia. Sasa tangu tuitishe sheria hiyo, hadi leo hii ninapoongea sijaona dalili za kuanzisha hiyo *Stabilization Fund* pamoja na ukweli kwamba kwenye sheria tuliyopitisha hapa ina kipengele kinachotoa nafasi ya kuanzishwa *Coffee Stabilization Fund*.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati tunapitisha Muswada huu mpya nilichangia hapa wakati wa Semina kwamba ni vizuri tukafikiria kuwa na *Stabilization Fund* au kuwa na chombo kingine kitakachofanana na hicho ambacho kitawezesha mabenki kuwa na imani na utaratibu huu kwa sababu sote tunafahamu uchumi wa mazao ni kwamba bei zake siku zote hupanda na kushuka. Kwa hiyo, hata mabenki haya yanafahamu hilo. Msije mkashangaa siku moja mabenki yakasema hayapo tayari kutoa asilimia 90 ya thamani ya mazao, bali watatoa asilimia 40 ya thamani ya mazao yaliyo kwenye ghala. Ikifikia hapo huu utaratibu utakuwa hauna maana yoyote. Ndiyo maana nasema haya mambo ni ya kufikiri na kujaribu kuangalia tufanye nini ili tuweze kuboresha mfumo huu uweze kuwa wa manufaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hoja ambayo mimi bado inanisumbua na wale wote wanaotoka kwenye eneo linakozalishwa kahawa huwa wanauliza mara nyingi. Kuna swali moja huwa tunaulizwa kwamba inakuwaje Mganda akija pale Kagera anatoa bei nzuri ya kahawa lakini sisi tunashindwa kutoa bei nzuri? Kwa hiyo, nikiwa kule wananchi nawajibu vizuri sana kwa sababu pale wananchi hawatofautishi kama wewe ni Mbunge au ni Serikali, wananchi wanachojua Wabunge wa CCM ndiyo wewe Serikali. Kwa hiyo, huwa natumia nafasi hiyo kujibu maswali magumu ambayo nisingependa saa hizi kuchukua nafasi hiyo kuanza kuyajibu hapa kwa sababu Serikali ipo. Ila nikiwa kule kwenye ziara hakuna Serikali, nabeba kofia mbili, wewe ndiyo Serikali kwa sababu ni Mbunge wa Chama Tawala lakini nikiwa humu sina haja ya kubeba kofia ya Serikali kwa sababu Serikali ipo.

Ninachotaka kuongea hapa ni kwamba tatizo moja la wakulima wa kahawa, wamekuwa wakiuliza mbona makato yanakuwa mengi? Kuna makato ya kukoboa na kuna makato ya kusafirisha. Sasa haya yote Mganda akija anayakwepa, ndiyo maana anaweza akatoa bei nzuri zaidi. Kwa hiyo, Muswada huu tunapopitisha leo hii utaleta makato mengine. Makato ya leseni, makato ya *inspection fee*, makato ya *receipt fee* na makato ya *storage fee*. Haya makato yote kwa yule mkulima atakayeama kuhifadhi

mazao yake kwenye ghala, tutake tuisitake hizo gharama atabebeshwa mkulima. Wakati tunatambua kwamba haziwezi kuepukika moja kwa moja. Lakini natambua vile vile gharama hizi zinaweza zikapunguzwa.

Nimejaribu kuangalia Sheria ya kuanzisha *Warehouse Receipt System* ya Marekani, nimekuta wao hawana Bodi, waliweka Sheria na Sheria hiyo inasimamiwa na *Agriculture Research Department* moja kwa moja bila kuwa na Bodi, kwamba kuna wataalam wameajiriwa kwenye Wizara wanafanya kazi hiyo *permanently*. Nikajaribu kuangalia ya Canada wana *Warehouse Receipt System* ya kahawa na wao hawana Bodi, wana Sheria iko pale na Wizara inayohusika inasimamia moja kwa moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo letu hapa Tanzania tulishaingia kwenye kasumba ya Bodi kwamba hakuna kitu kinachoanzishwa bila kuwa na Bodi. Huu ugonjwa tunao, mtu yoyote ukimwambia anzisha kitu, kitu cha kwanza kufikiria ni Bodi. Kwa hiyo, tuna ugonjwa wa Bodi, Bodi, Bodi. Sasa na ugonjwa wa Bodi maana yake ni kuongeza gharama za uendeshaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapoongelea utandawazi heshima mojawapo ya Serikali katika utandawazi ni kuwa na Serikali ndogo inayoendeshwa kwa gharama nafuu kwa niaba ya wananchi. Hiyo ni sifa mojawapo ya utandawazi. Lakini leo hii huu Muswada ninavyouona pamoja na kwamba tunasema ni wa kutuingiza kwenye utandawazi, lakini una sifa nyingine ambayo haiendani na kwenye utandawazi, kwamba unaongeza gharama nyingine za uendeshaji ambazo ningekuwa mimi kwa kweli nina uwezo ilikuwa sioni umuhimu wa Bodi.

Tunao Wataalam, tuna Katibu Mkuu, ana Wasaidizi wake, ana Wakurugenzi, hii Bodi inakaa kufanya nini? Maana Bodi watalipana posho, watacaa na matokeo yake ndiyo Rais anapata kazi ya kuvunja Bodi kila siku. Hatujui ya Kahawa amevunja kwa nini, lakini kwa sababu ya kuwa na Bodi nyingi nyingi tu zisizokuwa za lazima. Kwa hiyo, wakati tunafikiria kwamba huu Muswada tunaopitisha, basi tufikirie vile vile jinsi ya kupunguza gharama za uendeshaji ili mkulima tusimbebeshe gharama sizizokuwa za lazima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu utatusaidia vile vile na Waziri wa Kilimo na Chakula nadhani ajaribu kuliangalia hilo kwamba tuna *National Grain Reserve* ya kuhifadhi chakula. Kuna wakati tulikuwa tukisikia hapa kwamba tatizo la nchi yetu siyo chakula, tatizo ni kukisafirisha kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine kwamba sasa tumenunua mahindi Sumbawanga, tunasafirisha kupeleka sehemu nyingine. Sasa kwa kutumia *receipt system* Serikali itakuwa haina haja ya kubeba gharama kubwa sizokuwa za lazima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa sasa maghala yatakuwa katika maeneo mengi, basi Serikali itakachofanya ni kununua zile *receipts* tu. Haitahitaji kuingia gharama kubwa ya kununua mazao. Kwa hiyo, ndiyo inakuja hoja ya kuwa na maghala

maeneo mengi, kwamba hata kama sehemu fulani kuna maghala yana magunia 500, pamoja na uchache wake Serikali itakachofanya ni kununua *receipt* tu. Waziri wa Kilimo na Chakula akija hapa Bungeni na *briefcase* akisema, *grain reserve* hii hapa, ataonyesha *briefcase* yenye *receipt* tu za thamani ya mazao aliyonunua.

Kwa hiyo, mimi naona kuna haja ya Waziri wa Kilimo na Chakula na Waziri wa Ushirika na Masoko kushirikiana kwa karibu katika kuhakikisha kwamba mfumo huu unafanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naunga hoja mkono mia kwa mia. (*Makofî*)

**MHE. ISMAIL J.R. IWVATTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi na mimi nizungumzie juu ya huu Muswada.

Mheshimiwa Naibu Spika, sina mambo mengi, nilikuwa na mambo machache tu ambayo nataka kuyazungumza kama mambo matatu. Kwanza naomba niunge mkono hoja hii. (*Makofî*)

Lakini nilikuwa nataka niseme kwamba tumeleta huu Muswada hapa Bungeni tukiwa na matumaini kwamba wakulima wadogo wadogo watanufaika. Lakini hasa katika huu Muswada watu watakaohusika sana ni yule pereta mwendeshaji wa yale maghala na ikiwezekana labda na wale ambao watakuwa *wana-own* haya maghala kama mali zao au kama ni majumba yao.

Mkulima mdogo mdogo ambaye ni Mtanzania tunayemfahamu wa kajembe kabegani, Wazungu wanasema *peasants* hapa hatafaidika sana. Kwa hiyo, nilikuwa naomba tu Serikali iwe angalifu kwa maana ya kwamba wakati huyu *Operator* atakapokuwa anafanya kazi zake yeye ndiyo atakayekuwa na *contact* ya Benki na ndiye atakayekuwa na uwezo wa ku-negotiate zile *receipts* kuweza kupata hizo pesa ili aweze kuendelea kununua mazao na kisha kuyauza. Nasema hapa Serikali iwe angalifu kwa maana ya kwamba huyu *Operetor* asije akachukua nafasi hii kwa kuwakopa hawa wakulima wadogo wadogo. Yeye anakwenda Benki anapata pesa lakini anapokwenda kwa mkulima anakwenda anamkopa. Kwa hiyo, nilikuwa naomba hapa Serikali isaidie kuona kwamba hawa watu hawaonewi.

Lakini vile vile kama wenzangu walivyozungumza, hii ni biashara mpya au ni shughuli mpya tunayotaka kuianzisha. Kwa vyovytote vile, huko Kijiji ambako kunatoka, haya mazao aina ya maghala yanayotakiwa na huu Muswada hayatakuwepo. Nashukuru kwamba Waziri katika kutoa maelezo amesema watahamasisha, basi na pale inapowezekana basi naomba wasaidie kujenga haya maghala ili hii shughuli iweze kufanikiwa. Lakini na lile suala la elimu kama alivyozungumza yeye mwenyewe Mheshimiwa Waziri, naomba waendelee kulitoa na yale maghala watakayoyajenga, basi yawe kama ni maghala ya mfano ili na watu wengine waweze kufuata.

Lakini labda vile vile nitaomba Mheshimiwa Waziri atutoe tu wasiwasi kwamba hivi sasa katika mazao kama ya mahindi na mazao mengine, kuna wafanyabiashara hawa

wadogo wadogo na wana maghala yao. Je, itakapofika wakati wa kutumika hii sheria, hawa wafanyabiashara wetu wa siku zote na maghala yao yale ya matembe sijui na maghala ya majumba ya matope watapigwa marufuku hawataruhusiwa ama itakuwaje? Ama wao watakuwa hawaguswi na hii Sheria, watakuwa wanaruhusiwa kuendelea na utaratibu wao? Nilikuwa naomba hili Mheshimiwa Waziri atusaidie kulifafanua.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya pili, nilikuwa naomba nizungumzie katika upande wa mabenki. Kwa sehemu kubwa sana mabenki yatahusika katika utekelezaji wa hii sheria na nchi yetu Benki ambayo ina mtandao mkubwa ni *NMB* na kwa sehemu kubwa sina uhakika kama wamehusishwa katika huu Muswada.

Mheshimiwa Waziri alipokuwa anatoa maelezo yake, ametolea mfano wa *Exim Bank* na Benki nyingine ambayo bahati mbaya sikuweza kuisikia. Sasa nilikuwa naomba kama tunataka hii Sheria iweze kutekelezwa vizuri, basi huduma ya hizo Benki ambazo tayari zipo katika huu mfumo ienezwe katika maeneo mengine ambako hakuna ili kweli utekelezaji wa hii Sheria uweze kufanyika. Vinginevyo, kama tunategemea *NMB* hii ya sasa ambayo kwa sasa hivi ndiyo kwanza katika baadhi ya maeneo wameanza kutoa mikopo midogo midogo, tena kwa watu ambao wapo karibu nao, watu ambao wanaweza wakawafutilia kwa karibu mikopo yao kwa zile fedha ambazo wamewakopesha, kwa hiyo nina wasi wasi kwa shughuli kama hii ambayo itafanyika mbali na pale mabenki yalipo. Hii *NMB* haitakuwa tayari.

Sasa nilikuwa naomba kwa suala la mabenki liwekwe wazi kwamba je, hii huduma ya mabenki itapatikana kisawasawa ili huu utekelezaji wa hii Sheria usiwe na matatizo?

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya tatu ni ile sehemu ya sekta ya Bima. Mheshimiwa Dr. Kamala amezungumzia hapa habari ya *NIC* na uwezo wake. Hii sheria inamtaka kwamba *Operator* kuanza ku-*insure* mazao ambayo wataweka katika lile ghala. Lakini hata lile ghala lenyewe linalotakiwa kuweka hayo mazao na lenyewe linatakiwa kukatiwa Bima. Sasa hapa naomba Serikali vile vile iangalie uwezekano wa kusema kwamba na ile Kampuni ya Bima itakayojingiza katika hii biashara, basi ithibitishe uwezo wake wa kulipa pale kutakapokuwa kumetokea matatizo. Yaani ithibitishe kwamba itakuwa tayari kufanya *indemnity*, vinginevyo kama tutategemea Shirika letu la *NIC* hili lililopo, sasa uwezo wake kwa kweli ni mdogo, kama alivyotolea mfano Mheshimiwa hapa.

Leo hii ukienda *NIC* nina uhakika kabisa kuna watu wengi wanadai hata kwa zaidi ya miaka miwili, mitatu, minne au hata zaidi ya hapo hawajalipwa. Sasa kama tutalitegemea hilo, kuna uwezekano wa utekelezaji wa hii Sheria kukwama. Kwa hiyo, nilikuwa naomba Serikali hapo iseme wazi kabisa kwamba Kampuni ya Bima itakayojingiza katika hii Sheria basi ithibitishe uwezo wake wa kufidia hizi hasara zinapojitokeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho kabisa ni kwamba hii shughuli kwetu ni mpya. Kama kutakuwa na wasiwasi juu ya baadhi ya vyombo vyetu katika utekelezaji

wa hii Sheria, kuna Makampuni ambayo yameanza kujiingiza humu nchini kutokana na huu utandawazi na soko huria wa biashara kama hizi ambazo leo tunazungumzia katika huu Muswada. Sasa Makampuni kama hayo tukiwa na mashaka na vyombo vyetu, basi tufungue milango kwa haya Makampuni ili yaweze kutusaidia katika utekelezaji wa hii Sheria.

Mheshimiwa Naibu Spiki, baada ya kusema hayo, naomba kurudia kusema kwamba naunga mkono hoja hii. Nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi. (*Makofi*)

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kuweza kunipa nafasi nami niweze kuchangia katika Muswada huu muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile nilikwishazungumza kabla, basi nitaomba niendelee tu kwa kutoa mchango wangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, madhumuni makubwa wa Muswada huu kimsingi ni kusimamia mfumo wa kutumia stakabadhi za mazao kwenye maghala. Kwa hiyo, hayo ndiyo madhumuni makubwa. Kwa hiyo, kilicho mbele yetu Waheshimiwa Wabunge ni mpango mpya wa utumiaji wa stakabadhi kwa kuhifadhi mazao katika maghala na hatimaye kumwezesha mkulima kuweza kupata fedha zake au bei nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, faida kubwa kwanza kwa mkulima katika mpango mzima huu ni kwamba kwanza utamwezesha kuhifadhi mazao yake ili aweze kuvuta subra na kuweza kupata bei mzuri. Maghala haya ambayo yatatumika ni maghala ya kisasa ambayo yatahakikisha kuweza kuendeleza ubora wa mazao ya mkulima wakati akisubiri kuweza kupata soko na bei mzuri. (*Makofi*)

Maghala waliyokuwa nayo wakulima Vijijini, maghala yetu ni dhai fu sana kwa mkulima mmoja mmoja. Haya ni maghala tunayoyafahamu yako katika nyumba zetu zinazovuja na kwa hivyo hatuwezi kutumia maghala hayo kuhifadhi mazao kwa muda mrefu. Lakini vile vile ni maghala ambayo kwa kweli ni madogo hayawesi kukidhi mahitaji. Kwa hiyo, ni vyema sasa wakulima wetu wakafahamu na wakaelekezwa na wakazoweshwa kutumia maghala ya kisasa kwa manufaa hayo. Lakini ni mpango ambao vile vile utakuwa unamlinda mkulima kwa sababu stakabadhi hizi sasa zitakuwa ni stakabadhi zinazolindwa na mpango wa Sheria kikamilifu, zitatambuliwa kisheria, zitaheshimika kisheria na kama wataalam wengine wanavyozungumza katika lugha ya kibashara ni *negotiable instrument* chombo ambacho unaweza ukakitumia ukamkakabidhi mtu kama karatasi na ye ye akaidhamini akakupa fedha utakazokuwa unahitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, hizi stakabadhi pia zitamwezesha mkulima kuweza kupata fedha kwa haraka za kuweza kujikimu wakati akiwa anasubiri bei zipatikane au soko zuri la mazao yake liweze kupatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu huu pia ndiyo utaratibu pekee sasa ambao kwa kweli utamweka mkulima karibu zaidi na mnunuzi wa mazao kwa maana ya kwamba sasa wale wanaofanya kazi za uwakala katikati watapungua na kwa hivyo mkulima atapata nafasi ya kuweza kuwa karibu na mnunuzi na kwa hivyo anaweza akapata bei ya uhakika zaidi kutoka kwa mkulima moja kwa moja badala ya bei hizo kupitia kwa wakala ambao watakuwa wanamkata na yeze akawa anatumia nguvu nyingi, lakini fedha anazopata ni kidogo kuliko wale wakala wanaokaa katikati yake. Hili ili liweze kufanyika, basi kuna haja ya kuongeza elimu kwa wakulima wetu.

Moja ambalo limekwishaanza kufanya ni hili ambalo Wizara imechukua hatua ya kufanya utaratibu huu kwa majoribio katika baadhi ya maeneo na kwa bahati nzuri mafanikio yameonekana. Wakulima katika baadhi ya maeneo wamependa utaratibu huu na wameridhirika kwamba utaratibu huu ni mzuri na wanaipongeza Wizara na wanaomba kwamba utaratibu huu uendelezwe.

Sasa unapomsogeza mkulima kuwa karibu sana na mnunuzi wa mazao yake, kuna elimu ya ziada ambayo lazima aipate. Lazima mkulima aeewe tunapozungumzia soko la nje au bei ya masoko ya nje maana yake ni pamoja na gharama za ziada. Bei anayoififikiria mkulima ni bei itakayomwezesha yeze kufidia gharama zake za kazi aliyoifanya ya kilimo, lakini vile vile gharama za kusafirisha mazao yale kutoka katika shamba lake hadi kuyafikisha katika ghala. Bei hiyo ni tofauti na bei inayozungumziwa kwamba ni bei ya soko la nje kwa sababu hiyo itajumlisha na gharama nyingine za ziada ambazo inawezekana mkulima hazifahamu. Lazima sasa tuchukue hatua ya kumwelewesha mkulima aeewe tofauti hiyo.

Gharama za ziada ambazo mara nyingi wakulima wengi hawafahamu hasa kwa mazao yanayouzwu nje ya nchi ni pamoja na gharama za kusafirisha mazao yale kutoka katika bandari zetu iwe ni ya Tanga, Dar es Salaam, Mtwara ipakiwe katika meli na kusafirisha kuipeleka huko aliko mnunuzi, inawezekana ni Singapore, maeneo mengine kama vile Japan, Uingereza, au katika nchi nyingine yoyote na bandari nyingine yoyote katika nchi za Kiarabu. Hapo kuna gharama za kusafirisha kwa meli. Lakini yule anayelipa bei ya kununua mazao hayo huko nje aliko, maana yake attachanganya gharama zote hizo pamoja na hizi za kufikisha mazao yale katika bandari yake ya Singapore.

Kwa hiyo, lazima mkulima wetu aeewe utaratibu huu wote, aeewe maana ya gharama ambazo kwa kizungu wanasema FoB (*free on Board*), aeewe kwamba yeze gharama zake ni kuhakikisha tu mzigo unaingia Bandarini. Baada ya hapo gharama zote anachukua yule mnunuzi. Lakini zipo taratibu nyingine ambazo gharama zake zinasema wewe unayesafirisha vile vile lazima ulipie gharama nyingine zile za usafiri pamoja na gharama za Bima. Kwa hiyo, mkulima wetu lazima apate elimu ya kutosha kabisa, aeewe *terms* zote za biashara kabla hajapata bei au fedha zake za malipo ya mazao anayoyaiza nje. Jambo hili ni muhimu sana. Kwa hiyo, kuwa na Sheria peke yake haitoshi. Lazima kuambatane na kuwaelimisha wakulima waelewe taratibu za kibiashara na hasa biashara za mazao yanayosafirishwa nje ya nchi ambapo kuna wanunuzi kutoka

nje ya nchi. Kwa sababu sasa atakuwa karibu na wanunuzi hao lazima ajue taratibu zote zinazohusiana na biashara hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu huu ni nyongeza ya njia kadhaa zilizopo ambazo mkulima anaweza kuzitumia kuweza kuuza mazao yake. Kwa hiyo mkulima ana hiari kabisa ya kutumia aidha utaratibu huu kwa hifadhi ya *receipt* za maghala au anaweza akatumia utaratibu mwingine wowote ambao upo na zipo taratibu nyingine nyingi. Kwa hiyo utaratibu huu ni wa hiari kabisa ambapo mkulima atapaswa kuchagua. Ili uweze kumnufaisha mkulima, utaratibu huu unakuwa na manufaa sana kama utakuwa unatumiwa na vyombo kama Vyama vya Ushirika ambayo vinajumuisha idadi kubwa ya wakulima kuliko mkulima mmoja mmoja peke yake.

Kwa taratibu zinazotumika katika hifadhi za maghala, gharama za kuhifadhi mazao katika ghala zinawekwa kwa kutazama wingi wa mazao uliyokuwa nayo na wakati mwingine ni kwa kutazama eneo tu maalum, watakwambia *square meters* 20 ni gharama Sh.300,000/=. Sasa kama wewe una madebe matano ya korosho au magunia 50 ya kahawa kwa kuchajiwa kwa kiwango hicho, inaweza ikawa ni gharama kubwa kwako kama uko peke yako, mkulima peke yake. Lakini kama mtakuwa mmejiunga kwa pamoja, maana yake kwa kiwango hicho hicho cha *square meters* 20 kwa gharama hizo hizo Sh.300,000/=, mtagawana nyinyi wote mliopeleka magunia yenu kama kikundi au kama Chama cha Ushirika. Kwa hiyo kwa mmoja mmoja gharama zenu zitakuwa za chini sana. Sasa hili lazima wakulima walielewe ili waweze ku-take advantage ya hiyo nafasi ya kutumia Ushirika au vikundi mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuanzishwa kwa Sheria hii kunamlinda mkulima. Kwa hivyo atakuwa na uhakika wa usalama wa mazao yake, lakini vile vile atakuwa na uhakika wa usalama wa malipo yake kwa sababu pamoja na ghala kushirikishwa katika kuhifadhi mazao yake, Benki nayo imeshirikishwa kama chombo cha fedha. Lakini ni vizuri hapa sasa tunapoishirikisha Benki, basi tuwe na uhakika kabisa bila wasiwasi kwamba Benki zetu hizo ndani na sheria hizi zinatajwa na Benki hiyo kisheria na zenyewe zinakuwa *binded* kuthamini hizo stakabadhi za mazao. Ni kweli kuna Benki zimekwishaonyesha kwamba zinaweza zikafanya kazi kwa utaratibu huu. Lakini sheria inasemaje juu ya Benki hizo? Je, kesho na keshokutwa wakibadilisha mawazo? Sheria yetu inasemaje? Bado wakulima wetu wataendelea kutumia Benki hizo!

Ni vizuri tukaainisha Sheria yetu na mahitaji haya ya kisheria katika matumizi ya Benki. Mpango huu sisi wananchi wa Wilaya wa Muheza tunaukubali sana. Pamoja na kwamba si wakulima wa kahawa lakini sisi pia ni wakulima wa chai. Kwa hiyo, tuna matumaini makubwa vile vile kwamba wakulima wadogo wadogo wanaolima chai na kuuza katika viwanda vya chai vilivyopo, watapata nafasi nyingine ya pili ya uwezo wa kuuza chai kama mpango huu nao utakuwa unashirikisha wakulima wa chai na hasa katika Wilaya ya Muheza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hilo, upo mpango wa kuanzisha hili soko la Kimataifa la matunda na mbogamboga katika Mkoa wa Tanga. Sisi tuna imani kabisa kwamba utaratibu huu utatusaidia sana wakulima wa Wilaya zilizoko katika Mkoa wa

Tanga ikiwemo Wilaya ya Muheza, Korogwe, Lushoto, Handeni, Pangani, Tanga na Kilindi yenyewe, hasa wakulima wa matunda na mbogamboga. Katika kipindi ambacho msimu uko juu na masoko yameja tutaweza kwenda kuhifadhi mazao yetu katika soko la aina hii ili kuweza kusubiri bei nzuri. Tuna imani masoko ya Kimataifa yatakayokuja, yatakuwa na vifaa vitakavyosaidia kuweza kuhifadhi mazao yanayoharibika kwa haraka yaweze kukaa kwa muda mrefu. Kwa maana hiyo tuna uhakika tutapata bei nzuri na tunaukaribisha sana mpango huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi kuwa wa mwisho niweze kufunga utaratibu huu kwa siku hii ya leo na mimi nafunga kwa kauli hiyo kwamba ninaunga mkono hoja hii. Ahsante sana. (*Makofî*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, kwa leo tumefikia hapo. Ningependa tu kuwataarifu kwamba kwa wale wote ambao wameomba kuchangia, orodha iliyobaki ni ya wachangiaji 21. Kwa hiyo, usione leo hukutajwa lakini humo kwenye orodha.

Baada ya maelezo hayo, sasa naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho Saa Tatu Asubuhi.

*(Saa 01:39 Usiku Bunge lilahirishwa mpaka Siku ya Jumatano  
Tarehe 20 Aprili, 2005 Saa Tatu Asubuhi)*